**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Sita – Tarehe 4 Novemba, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Sammuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu utendaji usioridhisha wa Kampuni ya *Tanzania International Containers Terminal Services (TICTS).*

Taarifa ya utekelezaji wa Azimio la Bunge juu ya utendaji Usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania (*TRL*) uliofanywa na Kamapuni ya *Rites* ya India.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):**

Taarifa ya mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Benki ya Rasilimali kwa kipindi kilichoanzia tarehe 1 Januari, 2007 hadi tarehe 31 Desemba, 2007*(The Annual Report and Audited Financial Statements of the Tanzania Investment Bank Limited for the the Period 1st January, 2007 to 31st December, 2007).*

Taarifa ya Benki Kuu kuhusu Uchumi kwa robo mwaka iliyoishia tarehe 31 Disemba 2007, chapisho Namba 39(4) (*The Economic Bulletin for the Quarter ending December, 2007 Vol.* XXXIX No. 4.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 69

**Uwekezaji Nchini**

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inatekeleza mkakati wa kuwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuinua uchumi na kuboresha maisha ya Watanzania:-

(a) Je, ni wawekezaji wangapi waliowekeza hapa nchini?

(b) Je, wameongeza pato la Taifa kwa kiasi gani?

(c) Je, wameingiza nchini wafanyakazi wangapi wa kigeni na ongezeko la ajira kwa Watanzania likoje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, UTARATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Chaurembo Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli tunawakaribisha wawekezaji wa nje na kuhimiza pia uwekezaji wa ndani ili wawekeze hapa nchini. Mikakati ya kuvutia imewekwa na sheria ya uwekezaji *Tanzania Investment Act, No. 26 of 1997)* ambapo usajili wa miradi umeongezeka maradufu. Miradi yawawekezaji iliyosajiliwa ni 4,084 ambayo imetoa ajira kwa watu 654,577. Thamani yake ni shilingi trilioni 23,301.33. miradi mipya ni 2,793 na ile ya upanuzi ni I,291 kati ya yote iliyosajiliwa katika kipindi cha miaka 10 hadi 2007. Katika miradi hiyo miradi ya wageni ni 1033 na ya Watanzania ni 1,1941 na ya ubia ni 1,110.

(b)Mheshimiwa Spika, pato la Taifa limekuwa likiongezeka kila mwaka na pia uzalishaji mali katika miradi iliyoanzishwa. Pato la Taifa limekua kutoka shilingi bilioni 5,977.7 (1999) hadi shilingi bilioni 14,995.25(2006) kwa bei za miaka husika. Michango ya sekta zilizoingiza wawekezaji wengi imeongezeka, mfano ujenzi kutoka asilimia 5.2 (1998) hadi 7.9 (2006) uchimbaji madini kutoka asilimia 1.4(1998) hadi 3.2 (2006) na sekta ya mawasiliano na uchukuzi kutoka asilimia 1.1 (1998) 2.1(2006).

(c)Mheshimiwa Spika, taarifa ya kituo cha uwekezaji inabainisha kuwa kati ya mwaka 2000 hadi 2007, wafanyakazi wageni waliopewa vibali vya kufanya kazi katika miradi iliyosajiliwa nchini ni 12,625 na michanganuo ni kama ifuatavyo:-

Wafanyakazi *Class B* mwaka 2000 walikuwa 262, Mwaka 2001 ni 611, Mwaka 2002 wafanyakazi 984, 2003 wafanyakazi 1,945; Mwaka 2004 wafanyakazi 1,912; mwaka 2005 wafanyakazi 1974; mwaka 2006 wafanyakazi 2644 na 2007 wafanyakazi 2593. Jumla ya wafanyakazi waliopata vibali walikuwa wafanyakazi 12,625.

Mheshimiwa Spika, Watanzania waliopata ajira katika miradi iliyowekezwa kwa kipindi cha miaka 10 yaani 1997 hadi 2007 ni 659,577. Hii inatoa wastani wa ajira 65,960 kwa mwaka.

**MHE. ANNIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kwa kuwa kuna baadhi ya wawekezaji hapa nchini takribani miaka kumi iliyopita wapo chini, Wawekezaji hawa kila siku baadhi yao wanadai kwamba wanapata hasara na hawapati faida, lakini Wawekezaji hao hawako tayari kuachia maeneo ambayo wanayamiliki ili kutafuta Mwekezaji mwingine.

(a)Je, Serikali inasema nini kuhusu wawekezaji wa aina hii.

(b)Je, Serikali iko tayari kulieleza Bunge hili mafanikio yaliyopata (EPZ) *Economi Process Zone* na (*SEZ*) *Special Economic Zone* ni faida gani na hasara gani zimepatikana toka vianzishwe hapa nchini.

**WAZIRI WA NCHI, WAZIRI MKUU SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa wale wawekezaji ambayo wanasema kwamba huwa wanapata hasara wakati wote, Serikali imeshaligundua hili na kama tutakumbuka wakati wa kipindi cha Bajeti mwaka huu Mheshimiwa Waziri wa Fedha alishaweka kiwango cha kodi kwa wawekezaji wa aina hiyo, kwa sababu pamoja na kwamba wanapata hasara lakini kwa kuelewa kwamba shughuli au biashara zao zinaendelea basi kuna kiwango cha kodi kilichokadiriwa kwa mujibu wa sheria ya fedha ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *EPZ*, tukumbuke kwamba dhana ya *EPZ* ni ngeni kidogo hapa nchini kwetu na eneo ambalo sasa hivi tunatarajia kwamba litakuwa na mafanikio makubwa ni eneo la Benjamin Mkapa lililopo Mabibo ambalo kwa sasa wakati wowote ule Wawekezaji wanaweza wakawekeza kwa sababu miundombinu yote imekamilika na maombi yamepokelewa kwa wingi sana na eneo la pili ambalo tunatarajia baada ya hapo itakuwa ni eneo la Mbegani kule Bagamoyo ambapo wawekezaji wengi sana wanaonesha nia ya kujenga Bandari, uwanja wa ndege na hata reli kati ya Mbegani hadi Mlandizi.

**SPIKA:** Nakaribisha maswali mafupi sana mawili Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, halafu Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kuna baadhi ya wawekezaji hasa Wachina huingia nchini hapa na kusaini kwamba watafanya biashara kubwa kubwa, lakini kinyume chake Wachina hawa na baadhi ya wawekezaji wengine hufanya biashara ndogondogo za wamachinga pale Kariakoo kama kuuza vyombo na kadhalika?

Je, Serikali inaliona hilo na kama inaliona inachukua hatua gani kwa wawekezaji hawa?(*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, WAZIRI MKUU SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu wageni ambao wanafanya biashara ndogo ndogo ikiwa ni pamoja na Wachina wanaotajwa.

Lakini tukumbuke kwamba sheria yetu inaruhusu ubia na wageni hawa wameingia kwa vibali ambavyo vimekubalika kisheria isipokuwa kitakachofanyika sasa ni kuwa waangalifu zaidi wakati wa kutoa leseni ili kuhakikisha kwamba ni Watanzania tu ndiyo wanaopewa leseni hasa kwa biashara za rejareja.

**MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, nina wasiwasi kidogo na takwimu zilizotolewa za ile miradi mipya 2793 pamoja na ongezeko la Wafanyakazi kuanzia mwaka 2000 mpaka 2007 nilikuwa nataka kujua.

Je, idadi hii na takwimu ni kwa mujibu wa Tanzania nzima pamoja na Zanzibar imehusika au kwa mujibu wa Tanzania Bara wakati mwuliza swali amekusudia kwa Tanzania nzima?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MKUU, SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, inawezekana Waheshimiwa Wabunge au hata Wananchi kuwa na wasiwasi na takwimu hizi kwa vile sheria inalenga wawekezaji wa aina mbalimbali hasa wale wa ndani ambao wanaweza kuwa na mtaji unaofikia dola laki moja au shilingi milioni mia moja, ambao wamejisajili kwenye kituo cha uwekezaji. Kwa hiyo, ukiangalia Watanzania ambao wana mtaji wa kiasi hicho wameajiri watu wangapi, takwimu hizi ni sahihi, la msingi tukumbuke kwamba kwa upande wa Zanzibar kuna kituo pia cha uwekezaji. Kwa hiyo, takwimu hizi ambazo zinahifadhiwa na kituo cha uwekezaji cha Tanzania Bara hazihusishi takwimu za Zanzibar.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge wakati tunaendelea na maswali nawakumbusha kwamba baadhi yenu hamuendi kwenye visanduku *pegion hole* kuondoa barua, *pegion hole* zimejaa inashindikana hata kuweka nyingine na pili mnaweza kukosa ujumbe muhimu ambao mara kwa mara unaweza kutokea. (*Makofi*)

Na. 70

**Uwekezaji Mkoani Singida.**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, uwekezaji katika sekta mbalimbali ni njia mojawapo ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na soko huria a kwa kuwa, Mkoa wa Singida una eneo la kutosha la uwekezaji katika sekta za Madini na Kilimo:-

(a)Je, Serikali imefanya juhudi gani kuusaidia Mkoa wa Singida katika kuvutia wawekezaji kupitia *TIC?*

(b)Je, ni wawekezaji gani hivi sasa waliopo Mkoani Singida wamewekeza katika sekta zipi?

(c)Je, Serikali inatoa msaada gani kwa wawekezaji wa ndani ambao mitaji yao ni midogo na wawekezaji katika viwanda vidogo vidogo?

**WAZIRI WA NCHI, WAZIRI MKUU SERA, UTARATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jumaa Hassan Kilimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya suala zima la Uwekezaji katika sekta mbalimbali kama njia ya kusukuma na kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi. Juhudi za Serikali kupitia kituo cha Uwekezaji Nchini (*TIC*) ni mpango shirikishi wa kukuza uwekezaji Mikoani wenye lengo la kuibua fursa za uwekezaji na kuzinadi kwa wawekezaji kwa kushirikiana na viongozi wa Mikoa husika yaani *Regional Partnership Program*. Mpango huo utatekelezwa katika Mikoa mingine Nchini.

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Mkoa wa Singida umechaguliwa kuwa miongoni mwa mikoa mitano ya majaribio ambayo tayari semina ya maandalizi ya kuwajulisha viongozi wa Mkoa namna mpango huo utakavyofanya kazi ili kwishafanyika Dodoma tarehe 12 Septemba, 2008 ambapo Viongozi wa Mikoa husika pamoja na Wabunge wa Mikoa hiyo walihudhuria. Mpango huu husika ukiwemo Mkoa wa Singida katika Kuibua fursa za uwekezaji zikiwemo sekta za madini na kilimo ambazo zina fursa nyingi za uwekezaji katika Mkoa wa Singida. Mikoa mingine ya majaribio ni Kagera, Tabora, Rukwa na Tanga.

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa kituo cha uwekezaji kimesajili miradi minne (4) Mkoani Singida na miradi hiyo ipo kwenye sekta za Kilimo, Viwanda na Mafuta kama ifuatavyo:-

| **Na. Jina la Kampuni/Mradi** | **Sekta ya Uwekezaji** |
|---|---|

1. *Africommerce International Ltd*. Mafuta-*Fuel Storage Facilities*.
2. Sasa *Grain Milling Ltd.* Viwanda-*Agro Processing*.
3. *Bio-Sustain Tanzania Ltd.* Kilimo-*Product of Cotton and*
4. *Oryx Oil Co. Ltd.* Mafuta–*Fuel Storage Facilities*.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa baadhi ya matatizo yanayowakabili wawekezaji wa ndani ni pamoja na kuwa na mitaji midogo. Sasa upo utaratibu wa kuhamasisha wenye miradi midogo ya uwekezaji wapeleke taarifa za miradi yao *TIC* ili kutafutiwa wabia. Mara *TIC* wanapopata taarifa hizo, hutumia kwa kuzinadi kwa wawekezaji wanaotafuta wabia wa kuwekeza nao yaani "*Joint Venture*". Kituo cha Uwekezaji kina utaratibu wa kuandaa mikutano ya wawekezaji inayofanyika Nje na Ndani ya Nchi ambapo wawekezaji wageni hupewa nafasi ya kukutana ana kwa ana na wamiliki wa miradi hiyo inayohitaji wabia hapa nchini. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge hili Tukufu kuwa tukitumia utaratibu uliopo tutavuna fursa nyingi za uwekezaji kwa kuwa lengo ni kuwaletea wananchi Maendeleo.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri na hasa naishukuru sana Serikali kwa kuuweka Mkoa wetu kuwa kati ya Mikoa mitano ambayo inafanyiwa majaribio ya uwekezaji, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Mheshimiwa Waziri akijibu ameeleza na kuitaja miradi minne ambayo sasa itafanyiwa majaribio kule Mkoani Singida, lakini miradi hii ameisema Singida kwa ujumla, Je, kati ya miradi hiyo minne ni miradi gani ambayo imeonekana imekuwa-*identified* kwenda Jimbo la Iramba Magharibi hususan kwa Wilaya nzima ya Iramba.

(ii) Mheshimiwa Waziri wakati akijibu kipengele (c) amezungumzia naomba ninukuu kidogo "sasa upo utaratibu wa kuhamasisha wenye miradi midogoya uwekezaji wapeleke taarifa ya miradi yao *TIC* kutafutiwa wabia" kama hali yenyewe ndivyo ilivyo, Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kupokea taarifa kutoka kwangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwamba kuna wawekezaji wadogowadogo wa sekta ya mafuta ya alizeti na sasa hizo taarifa atazipeleka *TIC* ili waweze kusaaidiwa. (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, miradi yote minne niliyoitaja ipo katika makao makuu ya mkoa pale Singida, lakini kwa ujumla Mkoa wa Singida una fursa nyingi sana, kwanza kijiografia upo kati kati, makao ya Wilaya zote Manyoni, Kiomboi, na Singida kuna umeme wa uhakika, barabara zinaunganisha Mkoa na mikoa mingine, kwa hiyo fursa bado zipo japo kuwa wawekezaji wengi wamevutika kuwekeza pale Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema fursa bado zipo kwa hiyo niko tayari kupokea miradi ambayo inaibuliwa kutoka Iramba na Wilaya zingine Mkoani Singida.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na nikiona na pongezi alizotoa

Mheshimiwa Mbunge mwenye swali la msingi, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, kipindi cha Bajeti Serikali iliahidi kutuletea wawekezaji Mkoani Singida kwa ajili ya kusafisha mafuta ya Alizeti, Je, mkakati huo wa kuleta mwekezaji wa kujenga kiwanda kusafisha mafuta ya alizeti umefikia wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, sina hakika juu ya Mwekezaji aliyetajwa wakati wa Bajeti, lakini katika orodha niliyotaja ya wawekezaji waliowekeza Mjini Singida mojawapo amewekeza katika eneo la kukamua mafuta ya alizeti, pengine huyu ni mojawapo. Kama nilivyosema Mkoa wa Singida una fursa nyingi sana kwa ajili ya jiografia yake na uhakika wa umeme na miundombinu, kwa hiyo Wabunge na viongozi wa Mkoa wajitahidi kuibua miradi hasa ile ambayo itawanufaisha wananchi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, mimi napenda kumwuuliza swali moja dogo la nyongeza, kwa kuwa Mkoa wa Singida umekosa firsa nyingi sana za kupata wawekezaji kutokana na tatizo kubwa sana la miundombinu, na hivi sasa barabara ya kutoka Dodoma kwenda Singida bado inasuasua, Singida - Babati inasuasua pamoja na uwanja ule wa ndege na hivi ni vigezo vikubwa sana kwa Mkoa wetu kupata wawekezaji. Je, Waziri anawahakikishia vipi Wananchi wa Mkoa wa Singida kwamba tatizo hilo litakwisha ili wajihakikishie na wawekezaji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni lazima tukiri kwamba Wawekezaji katika nchi zetu wapo katika sehemu chache sana, Dar es Salaam, Arusha, na Mwanza kwa hiyo siyo kweli kwamba mikoa ambayo iko nyuma kwa uwekezaji ni Singida pekee, ni mikoa mingi sana ndiyo maana kituo cha uwekezaji kimeanza kwa majaribio kuweka mkazo uwekezaji katika mikoa ambayo ipo nyuma. Mkoa wa Singida una fursa na una bahati sana kama nilivyoeleza kwanza kuna umeme wa uhakika, lakini pia kuna mazao ya kilimo ya kuweza kusindikwa na barabara nyingi zipo mbioni kujengwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma –Singida sasa hivi wakati wowote inaweza kukamilika, Mkandarasi anaweza kwenda kwenye site wakati wowote wa barabara ya Singida mpaka Katesh na mwingine ataanza Katesh mpaka Dareda na mwingine Dareda mpaka Minjingu. Kwa hiyo, tunatarajia wakati wowote kuanzia sasa barabara ya Dodoma Singida itakamilika na wakati wowote kazi ya kuiwekea lami barabara ya Singida Arusha itaanza.

Na. 71

**Wabunge kupewa Orodha ya Miradi na Fedha za Halmashauri**

**MHE. CLEMENT B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa *D by D* ulioanzishwa na Serikali ni Mzuri sana kwani unawshirikisha wananchi na Serikali zao kuanzia ngazi za Kijiji, Tarafa, Wilaya hadi

Taifa na kwa kuwa ngazi ya Taifa ndiyo yenye uamuzi wa mwisho wa miradi itakayotekelezwa kulingana na uwepo wa fedha na kwamba uamuzi huo unaweza kusifanane kwa asilimia zote na maamuzi ya ngazi za chini:-

(a)Je, Serikali haioni kuwa ni busara Waheshimiwa Wabunge wapewe orodha ya miradi yote na fedha zote zilizoainishwa ili kuwarahisishia kufuatilia utekelezaji na matumizi ya fedha za Halmashauri.

(b)Je, Serikali haioni kuwa Watendaji wa Serikali wanaweza kubadilisha matumizi yaliyoamuliwa na Serikali bila kuwashirikisha Wabunge.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clement Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Serikali za Mitaa mapato na matumizi yote ya Halmashauri hutolewa taarifa katika vikao halali vya Halmashauri yaani katika Kamati ya Fedha na Mipango na katika Baraza la Madiwani. Hivyo, orodha ya miradi yote inayotekelezwa kwa mwaka ikionyesha kiasi cha fedha kwa kila mradi vimo ndani ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri. Aidha, Bajeti hiyo inawsilishwa katika kikao cha Kamati ya Fedha na Mipango. Kwa maana hiyo kwa taarifa zilizopo katika Halmashauri ya Kilosa kikao hicho kilifanyika tarehe 12 April, 2008 na kikao cha Baraza la Madiwani kilifanyika tarehe 13 Aprili, 2008.

Mheshimiwa Spika, taarifa za utekelezaji za miradi ya Maendeleo zinawasilishwa katika vikao nilivyovitaja kwa kila robo mwaka. Aidha, Waheshimiwa Madiwani wanaowajibu wa kufanya ufuatiliaji/ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Hivyo ni dhahiri kuwa kwa utaratibu huo kila Mbunge anafahamu au taarifa ya miradi ya maendeleo na matumizi ya fedha katika eneo lake.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa, pale inapoonekana kuwa kuna sababu ya kufanya mabadiliko katika matumizi ya fedha za Serikali uko utaratibu wa kufanya hivyo, katika Serikali Kuu kila Wizara au Mkoa unafanya *Re-allocation* na kupeleka maombi hayo Wizara ya Fedha. Aidha, katika Halmashauri yafuatayo yanafanyika:-

(i) Mapendekezo ya mabadiliko huwasilishwa katika kikao cha Watalaam (*CMT*).

(ii) Mapendekezo ya *CMT* huwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Fedha na Mipango kupata ridhaa.

(iii) Mapendekezo ya Kamati ya fedha Mipango huwasilishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani kupitishwa.

(iv) Mapendekezo hayo huandikiwa barua na kupelekwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya Kupata ruhusa ya kufanya mabadiliko na nakala hutumwa OWM-TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kwa utaratibu huo mabadiliko yoyote yanayofanyika Baraza la Madiwani lazima Baraza hilo lipitishe.

**MHE. CLEMENT B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa katika ngazi ya Serikali ya Wizara zinaidhinishwa Kiwilaya.

(a)Je, hakuna uwezekano katika ngazi ile kwa kutumia *software* iliyoko katika Wizara ika-*breakdown* matumizi ya Wilaya katika matumizi ya miradi iliyoidhinishwa kijimbo ili iwe rahisi kwa Wabunge kufuatilia kila katika jimbo lake kwa urahisi zaidi?

(b)Katika baadhi ya vikao alivyovitamka Mheshimiwa Naibu Waziri vya Baraza la Madiwani tuliarifiwa kwamba *software* inayotumika katika Wizara haiwezi ku-*generate data* zinazoonyesha *sector wise balance* ya fedha zilizobaki katika *quarter* ili kwa kila sekta na kwamba haiwezi pia ku-*carry forward balance* ile kwenye *allocation* ya *quarter* inayofuata *automatically* jambo ambalo lina utata wa kufanya vitu hivyo *manually*. Je, Serikali haioni kuna haja ya kuboresha *software* hiyo kama taarifa hizo ni za kweli? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Waziri hujajibu napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuchanganya sana Kiswahili na Kingereza ni kinyume cha kanuni unatakiwa useme lugha. Sasa kunaweza kuwa na neno moja la kitalaam sawa. Lakini kusema balance *automatically* na nini ndani ya suala la Kiswahili inakuwa ngumu. Lakini kwa sasa nitaliacha kwa sababu tunaendelea kuzoea. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, *concern* ya Mheshimiwa Lyamba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba uniwie radhi.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Naibu Waziri. Shauku.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, shauku ya Mheshimiwa Lyamba sisi wote kama Wabunge tunaiona na ndiyo nadhani anataka pia aweze kuelezwa kule kwenye Jimbo lake yaani tuweke utaratibu ambao utaonyesha kule kwenye jimbo lake yeye ni kiasi gani kimetengwa na kimewekwa katika utaratibu huo kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni ukweli usiopingika kwamba eneo la kufanya mipango haliko katika jimbo, eneo la kufanya mipango liko katika Halmashauri inayohusika ambayo Mheshimiwa Lyamba naye anakuwa ni mjumbe katika kila kikao. Kwa hiyo, kusema unaweza ukatenganisha pale ukawawekea itabidi sasa wafanye kazi nyingine ya ziada lakini utaratibu wa kupitisha Bajeti hapa unaangalia Halmashauri kwa maana ya Halmashauri yenyewe na siyo kijimbo. Kwa hiyo, inakuwa ni kazi sasa ya Mbunge kwenda kuangalia sasa yeye kama Jimbo amepata kiasi gani.

La pili, Mheshimiwa Lyamba anazungumzia kuhusu suala hili la takwimu, ni swali la kitalaam sana analoliuliza hapa ambalo mimi nakubaliana na yeye kwamba wakati mwingine kwa vile kutakuweko na zile zilizobaki kule nyuma na hazikuja zikaonekana mbele kunakuwa kuna hilo tatizo. Lakini kama tulivyojibu hapa utaratibu wa matumizi na mapato unapatikana katika Halmashauri inayohusika.

Hii ni changamoto kwetu sisi wote kama Wabunge, kuangalia kwa pamoja kuona kwamba pale unafuatilia kwa karibu. Lakini nataka nitoe ahadi hapa kwamba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu popote pale Mheshimiwa Mbunge anapoona anapata unafuu katika ufuatiliaji tunaweza tukasaidia katika hili eneo ili takwimu sahihi ziweze kupatikana. (*Makofi*)

Na. 72

**Kukarabati Hospitali ya Kwimba**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kwimba itakuwa kwenye mpango wa kufanyiwa ukarabati mkubwa na kwa kuwa watalaamu wa *Calus Bremer Associates Ltd.* walishafika katika hospitali hiyo na kujionea hali ilivyo:-

(a) Je, nini kilichotokea na kusababisha ukimya mkubwa ambapo hata uongozi wa hospitali na Halmashauri ya Kwimba hawajajulishwa juu ya Maendeleo ya mpango huo?

(b) Je, mpango huo wa ukarabati bado upo au Serikali ina mpango gani mwingine mbadala wa kukarabati hospitali hiyo ambayo bado haina hadhi ya Hospitali ya Wilaya?

(c) Je, Serikali italeta lini watalaam mbalimbali wa afya ili kukidhi mahitaji ya wastani wa wagonjwa 3,600 wanaofika hapo kuhudumiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba watalaam washauri *(Claus Bremer Association Ltd.*) mwaka 2005/2006 walifanya zoezi la tathimini ya Hospitali ya Wilaya na Hospitali Teule 95 na Hospitali ya Ngudu katika Wilaya ya Kwimba ikiwemo. Hivyo naomba nitoe taarifa kwamba zoezi hilo liliwezesha kujua aina na ukubwa wa ukarabati unaotakiwa katika hospitali na hatimaye kuzipanga kwa kufuata mahitaji ya ukarabati ili ziweze kufanyiwa ukarabati kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Kwimba ilijulishwa kuhusu maendeleo ya mpango huo kwa kuwa mwaka 2006/2007 watalaam washauri walifanya vikao kati yao na watalaam kutoka katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba. Madhumuni ya vikao hivyo ilikuwa ni kuwashirikisha na kuwajulisha watalaam ngazi ya Mkoa na Wilaya hatua iliyofikiwa na kazi zinazoainishwa kutokana na tathmini iliyofanywa na watalaam washauri.

Hivyo ni dhahiri kuwa Halmashauri hiyo inazo taarifa hizo. Hata hivyo naomba kumtaarifu Mheshimiwa Bujiku Sakila na Bunge lako Tukufu kwamba *Claus Bremer Association Ltd.* ni watalaam waliofanya tathmini tu na hawatoi fedha yoyote kufanya ukarabati. Halmashauri zinatakiwa kutumia taarifa hizo kutafuta fedha za kufanya ukarabati.

(b)Mheshimiwa Spika, mpango wa ukarabati wa Hospitali za Wilaya bado upo. Fedha za ukarabati zinaweza kutoka katika mpango wa Serikali wa kuzipatia ruzuku Serikali za Mitaa kupitia dirisha maalum la afya *(Health Window)* litakalofunguliwa katika mpango wa kuzipatia ruzuku Serikali za Mitaa kwa mwaka 2008/2009. Vile vile Halmashauri zinaweza kutumia fedha zinazotolewa kupitia Mfumo wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa.

Naomba kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kuweka ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Ngudu katika makisio yake ya Bajeti ya mwaka 2009/2010 kama itaona kuwa ni kipaumbele cha mipango ya Maendeleo ya Wilaya kwa mwaka ili fedha hizo ziweze kutengwa.

(c)Ni kweli Hospitali ya Wilaya ya Kwimba ina upungufu wa watumishi. Kwa mujibu wa mwongozo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Hospitali ya Wilaya inastahili kuwa na jumla ya watumishi 98 kwa maana ya watalaam, vile vile inatakiwa kuhudumia watu kati ya 150,000/= hadi 200,000/= watumishi waliopo kwa sasa ni 30 hivyo kuna upungufu wa watumishi 69. Ajira na uwekaji wa mazingira mazuri kwa watumishi ni jukumu la Halmashauri. Napenda kuiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, kuhakikisha wanaweka mahitaji ya watumishi katika Ikama za Halmashauri ili kujaza nafasi wazi. Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya ili kukidhi mahitaji ya watalaam nchini.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kwa swali la msingi. Ninayo maswali mawili.

(a) Ni kweli Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ina taarifa kwamba hawa hawatoi fedha. Lakini watalaam hawa pamoja na watalaam wa TAMISEMI walikuja Kwimba au Ngudu mwezi Februari, 2007. Kabla ya kuondoka waliagiza uongozi wa Hospitali ya Ngudu pamoja na Halmashauri wasijenge, au kufanya ukarabati wowote katika Hospitali hiyo, mpaka mwezi Mei ambapo wangekuja kuanza kufanya ukarabati. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Spika yanasema kwamba tusubiri mipango mingine.

Je, kwa mawazo ya Mheshimiwa Naibu Waziri Wilaya ya Kwimba tangu mwaka 2007 haijakarabati wala kujenga jengo lolote katika Hospitali. Je, itaendelea kusubiri ule utaratibu utakapoanza?

(b)Upungufu wa watumishi katika Hospitali ya Wilaya nilioutaja katika swali la msingi unaonekana hata kwenye zahanati kwenye zahanati pamoja na vituo vya afya katika Wilaya ya Kwimba. Maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni mazuri na ndiyo kitu ambacho Wilaya ya Kwimba imekuwa ikifanya kwa miaka yote. Sasa naomba kuuliza. Je, Naibu Waziri yuko tayari kutusaidia ile ikame tunayoiomba kwenye Wizara ya Utumishi itusaidie angalau tuweze kupata kama tunavyoomba ili mahitaji yafike mpaka kwenye zahanati ya vituo vyetu vya afya? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali yalikuwa marefu kidogo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hii kampuni ambayo tumeizungumzia hapa ni kweli kwamba ilikwenda kule ikufanya tathimini hiyo. Ninataka nimfahamishe Mheshimiwa Bujiku Sakila kwamba hicho kitendo tu cha kwenda kutathimini na kufanya tathimini kwa ajili ya hospitali za Wilaya 95 chenyewe kilikuwa ni mchango mkubwa sana vinginevyo Halmashauri ingetakiwa sasa kazi hiyo ya kufanya tathimini halafu na baadaye ifanye kazi sasa ya kwenda kukarabati kama ilivyokuwa imeelekezwa hapo.

Kwa hiyo, nataka niseme kwamba sisi tumefuatilia jambo hili katika Wizara kwa kweli ilikuwa siyo sahihi kwamba wale wanasema kwamba wale wakae pale ninyi Halmashauri msubiri mpaka hela zitakapokuja waje wakajenge.

Kampuni ile kazi yake ilikuwa ni kufanya tathimini tu na haikufanya kwa Wilaya ya Kwimba ilifanya pia na Wilaya nyingine kama nilivyoeleza hapa 95. Kwa hiyo, nataka niseme sasa kwamba sisi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, tutashirikiana sasa kuona kwamba tufanyeje ili tuweze kusaidia suala la ukarabati. Ndiyo maana nimependekeza katika majibu ya msingi kwamba kwenye Bajeti ya mwaka 2009/2010 tuhakikishe kwamba tunaingiza kule ili tuweze kusaidiana kwa pamoja tuwaondoe wananchi katika haya matatizo ambayo wanayapata.

Hili la pili, nimekiri kabisa hapa kwamba idadi ya watumishi walioko pale tena hawa tunazungumza ni wale watalaam pale hatujaingiza hata na wale wengine wa kufanyakazi ya kufyeka majani. Tunakiri kwamba kuna upungufu mkubwa pale wa watumishi.

Tunachofanya sisi kama Wizara ni kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuona kwamba tunapata watumishi wengi zaidi ili hili tatizo la Mheshimiwa Bujiku Sakila analolizungumza liweze kutatuliwa.

Kwa hiyo, naomba nimwahidi kwamba tutashirikiana tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Afya ili tuone kwamba idadi hiyo inaongezeka. (*Makofi*)

Na. 73

**Kuboresha Taratibu za Upandaji wa Miti**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka kadhaa kumekuwepo na kampeni mbalimbali za upandaji miti na uhifadhi wa mazingira hapa nchini na kwa kuwa katika upandaji miti kumekuwa na kutozingatia ubora wa miche uwekaji wa mbolea, umwagiliaji na kutokuwa na usimamizi madhubuti wa mamlaka husika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha kanuni za upandaji miti kwa kuzingatia vigezo mbalimbali kama ubora wa miche, umri wa miche, utunzaji wake na kadhalika?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama zilivyo nchi nyingi duniani inakabiliwa na tatizo la kupungua kwa idadi ya miti na maeneo ya misitu. Inakadiriwa kuwa takribani hekta 92,000 au asilimia 0.2 ya maeneo ya misitu hapa nchini hupotea kila mwaka kwa sababu ya shughuli za binadamu. Ili kukabiliana na changamoto hii Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuunda sera ya taifa ya misitu, sera ya taifa ya hifadhi ya mazingira, waraka wa Serikali namba 1 wa mwaka 2000 kuhusu siku ya taifa ya upandaji miti na mkakati wa taifa wa kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa sera na miongozo hii changamoto kadhaa zimejitokeza ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa mwongozo ulio madhubuti juu ya aina ya miti inayofaa kupandwa katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kukidhi mahitaji na matumizi mbalimbali.

Katika kukabiliana na changamoto hizi na kuhakikisha kwamba kunakuwepo uoteshaji wa miche bora ya miti pamoja na utunzaji wake, Serikali imechukua hatua zifuatazo kukabiliana na changamoto hiyo.

- Kutoa tamko na kupiga marufuku upandaji miti isiyofaa katika vyanzo vya maji na kuhamasisha upandaji wa miti ifaayo katika maeneo hayo.

- Kubainisha aina ya miti inayofaa kupandwa katika maeneo mbalimbali ya vyanzo vya maji nchini.

- Kuendesha kampeni ya kuondoa miti isiyofaa kwenye vyanzo vya maji katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia wakala wa mbegu za miti Tanzania mwaka 2007 ilitoa kitabu cha mwongozo wa miti inayofaa kupandwa Tanzania na ukuzaji wake. Kitabu hiki kinachopatikana katika vituo vya wakala wa mbegu za miti vilivyoko Morogoro, Lushoto na Iringa, kinatoa mwongozo wa uchaguzi wa miti ya kupanda maeneo mbalimbali, namna ya kuanzisha vitalu vya miche, upandaji na utunzaji wa shamba la miti na uvunaji wa miti. Aidha, huduma ya ushauri na mbegu kutoka katika vituo hivyo husaidia upatikanaji wa mbegu bora ambazo huzalisha miche ya miti inayokusudiwa kupandwa.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji wa mwaka 2006 unabainisha wadau wa utekelezaji wa shughuli za upandaji miti ambao ni Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Makamu wa Rais. Mamlaka hizo zinasimamia kikamilifu zoezi la upandaji miti na utunzaji wake nchini.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tarehe moja kila Januari kila mwaka ni siku ya upandaji miti hapa nchini na kwa kuwa Halmashauri zetu hutumia fedha nyingi katika kununua miche na kupanda, lakini usimamizi ni mbaya.

Kwa hiyo hupelekea Serikali kutumia fedha nyingi kila mwaka lakini tija haionekani. Je, Serikali inasema nini juu ya utumiaji wa fedha ambazo zisizoleta tija? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**): Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Januari ni siku ya kupanda miti duniani na ni siku ambayo inatambuliwa kimataifa ni kwa ajili ya uhamasishaji wa upandaji wa miti. Ndiyo sababu kwamba kila Wilaya inabidi na yenyewe ihusike na ifanye shughuli hiyo kwa hiyo tarehe 1. Lakini kila Wilaya inatakiwa iwe na mikakati yake madhubuti ya kuhakikisha kwamba kila kipindi cha mvua wapande miti ya kutosha na kwa sasa hivi ni kwamba baadhi ya Wilaya zinafanya vizuri na baadhi ya Wilaya hazifanyi vizuri. Lakini napenda nipongeze Mkoa wa Iringa Wilaya zake zote zinafanya vizuri sana katika upandaji wa miti. Kwa hali hiyo basi napenda kutoa wito kwamba Wilaya zingine zote, Halmashauri zisimame imara na kuhakikisha kwamba zoezi hilo linafanyika vizuri na tarehe 1 hiyo itumiwe kwa uhamasishaji lakini kazi iendelee katika siku za mvua kama inavyotakiwa. (*Makofi*)

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa. Pia nimefurahishwa na mtandao mkubwa wa Wizara ambao unawajibika katika suala zima la upandaji miti. Duniani leo nchi nyingi zina mkakati wa kupanda miti hasa katika miji mikubwa ili kuboresha mazingira na kutoa sura nzuri ya miji hiyo na miti inayopandwa sasa siyo ile midogo midogo kama tunayopanda sisi wanapanda miti mikubwa kama utalaam wa Kichina unavyoonyesha.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa utaalam huu utasaidia kupunguza gharama kwa sababu unapopanda mia moja midogo midogo inaweza ikafa nusu yake, lakini mikubwa mara nyingi ukisimamia vizuri inaota yote. Anaonaje Serikali ikaanzisha mpango huo ambao utasaidia kuboresha mazingira yetu na kupunguza gharama? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nchi nyingi duniani zina mkakati mzuri wa kupanda miti na hata hivyo kwa upande wetu Tanzania hatuko nyuma. Tuna mikakati mbalimbali ya kupanda miti aina mbalimbali, kama nilivyosema katika jibu la awali kwamba tunapanda miti ya aina mbalimbali kwa kufuatana na sehemu ilivyo na pia kuhimili na hali yetu ya nchi pamoja na kuhimili mazingira zaidi katika sehemu za vyanzo vya maji.

Kwa hali hiyo, napenda niseme kwamba kwa Tanzania tuna mikakati hiyo ya kupanda miti ya asili na pia mikakati ya kupanda miti ya kibiashara na kupanda miti ya aina mbalimbali kwa kufuatana hali maalum inavyopendekeza. Napenda pia kushukuru kwamba kwa ushauri wake lakini ni mojawapo ya mikakati tuliyonayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 74

## Ahadi ya Kushughulikia Kero za Muungano

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi mambo mengi katika mikoa mbalimbali hapa nchini na kwa upande wa Zanzibar aliahidi kuchukua hatua madhubuti kuimarisha Muungano wetu kwa kuongeza kasi ya kushughuli kero za Muungano.

(a) Je, ni hatua gani madhubuti zimechukuliwa hadi sasa za kuimarisha Muungano wetu?

(b) Je, kero zipi zilizoshughulikiwa hadi sasa?

(c) Je, kwa nini kero zilizoshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi hazitangazwi hadharani kwa wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Viti Maalum, lenye vipengele a, b na c kama ifuatavyo:-

(a)Hatua madhubuti zilichukuliwa hadi sasa katika kuimarisha Muungano wetu ni pamoja:-

(i)Rais aliunda Kamati ya pamoja ya SMT na SMZ kushughulikia masuala ya Muungano chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(ii)Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliipa muundo mpya Kamati ya pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano na kuifanya kuwa chini ya Uenyekiti na Uongozi wa Mheshimiwa Makamu wa Rais.

(iii)Kamati ya pamoja imeshafanya jumla ya vikao vinne tangu ilipoundwa. Vikao hivi vilitanguliwa na vikao vya Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watalaam wa SMT na SMZ.

(b) Baadhi ya kero zilizoshughulikiwa hadi sasa na kukamilika ni kama zifuatazo:-

(i) Mgawanyo wa mapato yatokanayo misamaha ya mikopo ya fedha kutoka *IFM*.

(ii) Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imepitishwa na inafanyakazi pande zote mbili za Muungano. Aidha, Tume ina ofisi Unguja na ipo katika mpango wakufungua Ofisi nyingine kule Pemba.

(iii) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaweza kukopa sasa kwenye soko la ndani.

(iv) Sheria ya mamlaka ya Kusimamia uvuvi katika Bahari Kuu ya mwaka 1998 imepitishwa na imeanza kutumika rasmi katika pande zote za Muungano kuanzia tarehe 1 Juni, 2008.

(v) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashirikishwa katika masuala mbalimbali ya kimataifa kuanzia hatua za awali.

(vi) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashirikishwa katika masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kikamilifu ikiwemo kupewa fursa ya kuwa na miradi ya maendeleo.

(vii) Sheria ya *Merchant Shipping Act* 2003 imeendelea kutekelezwa katika masuala yote yanayohusu uchukuzi na usalama wa njia ya majini katika mikataba yote ya kimataifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Aidha, *International Maritime Organization (IMO)* imekubali Zanzibar *Maritime Administration (ZMA)* iliundwa chini ya ya Sheria ya *Maritime Transport Act, 2006*, itekeleze baadhi ya majukumu kulingana na mikataba ya Kimataifa chini ya mwamvuli wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Kero zinazoshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi zimekuwa zikitangazwa kwa wananchi mara kwa mara na Mawaziri wenye dhamana ya kuratibu masuala ya Muungano kwa kuzungumza na vyombo vya habari. Aidha, taarifa hutolewa wakati wa kujadili utekelezaji wa shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mwisho hata hivyo bado kero kadhaa zimo katika mchakato wa kujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo kwa kweli sikuridhika nayo.

Mheshimiwa Spika, nina imani kwamba Mheshimiwa anazielewa vizuri kero za msingi za Muungano wetu na kwa mujibu yake inaonekana zile kero za msingi hakuzigusa na ndiyo maana nikasema sikuridhika. Kwa mfano kwa mujibu wa makubaliano yetu yaani kwa mkataba *(Article of Union)* ya Muungano wetu sasa kuna matatizo ambayo yamejitokeza ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuondolewa madaraka yake ya kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ni kero kubwa na ya msingi.

(a)Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusiana na hilo?

(b)Mheshimiwa Waziri katika Bunge lililopita wakati akijibu swali aliliahidi Bunge lako Tukufu kwamba wanasheria wetu wakuu kutoka SMT na SMZ wangekaa na

kutafuta au kutafakari tafsiri halisi juu ya vifungu vya Katiba. Je, kazi hiyo hadi sasa imeanza na imefikia wapi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la dada yangu Riziki kama ifuatavyo:-

Nia yangu ni kumridhisha sasa Mheshimiwa Riziki mazuri na ya kumfurahisha lakini bahati mbaya hakuridhika naomba samahani sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, suala la nafasi ya Makamu wa Rais limekuja baada ya mfumo wa vyama vingi kuja hapa nchini na ilifanya hivyo kwa nia njema kabisa. Lakini nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, kwamba nafasi hii imebadilishwa baada ya ridhaa ya Wabunge hapa hapa Bungeni na ni maamuzi ya Wabunge wa Zanzibar na Wabunge wa Bara. Kwa hiyo, kama anafikiri Mheshimiwa Riziki anataka mabadiliko haya sasa atoe hoja nyingine ili ije Bungeni hapa tubadilishe basi hapana shida yoyote. Lakini haya ni maamuzi ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili amezungumza kwamba nilitoa ahadi kwamba wanasheria wa SMZ na SMT watakutana, sikusema mimi, alisema labda Waziri Mkuu, mimi sikusema hivyo. Lakini la msingi ni kwamba vikao vya Serikali mbili hizi vinaongozwa na Makamu wa Rais. Katika vikao hivyo ndiyo mahali ambapo tunakaa tunazungumza matatizo mbalimbali yanayoikabili nchi yetu na kuyarekebisha. Kwa hiyo, nasema jambo la msingi si kukutana wanasheria wawili tu, basi ni muhimu kukutana viongozi na Mawaziri wa Serikali mbili za Serikali ya Muungano na Serikali ya SMZ. (*Makofi*)

Na. 75

**Mgao wa Fedha za MCC kwa Mkoa wa Singida**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuwa Mkoa wa Singida ni wa mwisho wa pato la mtu kwa mwaka *(per capital income)* nchini;

(a) Je, ni vigezo gani vilivyotumika katika kugawa fedha za *MCC* zilizotolewa na Rais George W. Bush (Bil. 700) na kuacha Mkoa wa Singida kuwa wa mwisho kwa umaskini bila mgao wa fedha?

(b) Je, kwenye mgao huo wa fedha Mikoa kwa ujumla ilihusishwa vipi kabla ya kufikia maamuzi yaliyotolewa kwa mikoa mingine kupata na mingine kutopata mgao huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyotumika katika kugawa fedha za *MCC* zilizotolewa na Rais W. Bush wa Marekani ambavyo vilitolewa na Serikali ya Marekani yenyewe vilikuwa ni kama ifuatavyo:-

(i)Miradi inapendekezwa iwe ni miradi ya vipaumbele na ambayo maandiko yake ya kitalaam *(feasibility studies)* yamekamilika.

(ii)Miradi hiyo iwe na manufaa na utekelezaji wake utainua uchumi wetu.

(iii)Iwe ni miradi yenye nafasi ya kunufaisha watu wengi.

(iv)Iwe ni miradi itakayoweza kukamilishwa ndani ya kipindi cha miaka mitano.

(a)Mheshimiwa Spika, miradi iliyochaguliwa ni sehemu ya miradi mingi iliyoainishwa na kukubaliwa kitaifa chini ya mpango wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini kwa Tanzania Bara (MKUKUTA) na Zanzibar (MKUZA). Maandalizi ya MKUKUTA na MKUZA yaliwashirikisha kwa kina wananchi ikiwa ni pamoja na mikoa yenyewe. (*Makofi*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi, na siyo Mashariki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Waziri katika majibu yake nadhani anataka kuniarifu kwamba Mkoa wa Singida haukupeleka lile andiko la kitalaam *(feasilibity study)* mapema sambamba na mikoa mingine.

Sasa kama ni hivyo Mkoa huo umekosa fedha hizo za *MCC* kwa maana hiyo kwa sababu hiyo ya kutokupeleka andika la kitaalam. Kama ni hivyo ni hatua gani zimechukuliwa kwa watalaam waliopaswa kufanya hiyo?

(b) Mheshimiwa Spika, *issue* ya MKUKUTA, nadhani MKUKUTA unahusu mikoa yote. Sasa kama kuna miradi ya Mkoa wa Singida imefuata utaratibu wa MKUKUTA ikiwa na lengo la kuweza kuondoa umaskini.

Kama kuna miradi ya mikoa ya Singida imefuata utaratibu wa *MKUKUTA* ikiwa na lengo la kuweza kuondoa umasikini. Sasa kama kuna miradi iliyopelekwa, je ina maana kwamba miradi ya Mkoa wa Singida haikuweza kuzingatia utaratibu wa *MKUKUTA* kiasi cha kuweza kukosa mgawo huo wa fedha? Ninaomba jibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza namwomba radhi Mheshimiwa Lwanji kwa kumtamka kwamba ni Mbunge wa Mashariki. Baada ya hayo ninaomba kujibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwanza sikutamka kwamba Singida hawakupeleka *feasibility studies.* Nilichokisema ni kwamba *fesibility studies* zilizowasilishwa zilikuwa ni nyingi, na milioni 700 sio pesa nyingi ukilinganisha na matatizo tuliyonayo Tanzania. Kwa maana hiyo inawezekana kwamba Singida na wao walikuwemo katika kuwasilisha lakini kwasababu ya ufinyu wa fedha zenyewe tumeshindwa kuweza kuwapatia mikoa yote kwa mujibu wa maombi yao.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la *MKUKUTA*, miradi yote ambayo imeandaliwa ndani ya mikoa yetu imeandaliwa kutokana na *MKUKUTA*, mpango mzima wa kupunguza makali ya umasikini Tanzania.

Lakini nataka niseme tu ili Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge, wengine waweze kutufahamu, miradi hii inafadhiliwa kupitia vifungu au mafungu matatu ya fedha, kwanza tuna *General Budget Support* ambayo ni pesa zetu za ndani pamoja na wafadhili ambao wanatuchangia katika miradi hii.

Lakini vilevile kuna miradi ambayo inafadhiliwa kupitia mikopo ambayo Serikali ya Tanzania inakopa kutoka benki ya dunia, kutoka *BADEA*, kutoka *African Development Bank* na Benki nyingine. Lakini vilevile kuna baadhi ya wafadhili wanakwenda *direct* kuzi-*support* sekta zinazohusika. Kwa maana hiyo nataka niseme kwamba bado iko miradi inayotekelezwa katika mkoa wa Singida licha ya kwamba

haikupata fedha za *NCC* lakini imepata fedha kwa kupitia hayo maeneo ambayo nimeyasema.

Kwa maana hiyo bado tutaendelea kuisaidia mikoa ili nayo iweze kukamilisha miradi yake. *(Makofi).*

Na. 76

**Mifuko ya Pensheni Kukopesha Wanachama Wake**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa, watumishi wa serikali na Mashirika huchangia katika mifuko ya *NSSF/PPF* ili kupata mafao yao baadaye wakati wa kustaafu; na kwa kuwa, Mashirika hayo huwekeza katika miradi mbalimbali ili kukuza mifuko yao:-

Je, Serikali ipo tayari kushauri mifuko hiyo iwakopeshe watumishi ambao ni wanachama wao kwa dhamana ya michango yao?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Jeremia Solomon Sumari. Kwa faida ya wageni wetu waliomo humu Wizara hii nayo ina Naibu Mawaziri wawili, aliyejibu mwanzo alikuwa Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na sasa anayejibu kwa Wizara hiyo hiyo ya Fedha na Uchumi ni Mheshimiwa Jeremia Solomon Sumari.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Jimbo la Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba watumishi wa Serikali, Mashirika ya Umma, taasisi za serikali na waajiri binafsi huchangia katika mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii ikiwemo mfuko wa *NSSF, GEPF, LAPF* na *PSPF* kwa ajili ya mafao yao wakati wa kustaafu.

Aidha mifuko hii huwekeza michango hiyo ya wanachama wao katika vitega uchumi mbalimbali ili kupata faida kwa lengo la kutunisha mfuko na hatimaye kulipa mafao kwa wanachama baada ya kustaafu. Mikopo ni eneo mojawapo mifuko huwekeza iwe kwa wanachama au kwa makampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushauri wa kamati mbalimbali za Bunge, hususan Kamati ya Fedha na Uchumi, kwamba mifuko iangalie uwezekano wa kuwakopesha wanachama na michango yao itumike kama dhamana kwa mikopo hiyo, mifuko hii imekuwa ikitoa mikopo mbalimbali kwa wanachama wake hususan ya kununua au kujenga nyumba za gharama nafuu na kwa riba kidogo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mikopo hiyo sheria mpya ya hifadhi ya jamii iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili mwaka huu wa 2008, imetoa fursa kwa wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii kutumia 40% ya michango yao wakiwa bado kazini kama dhamana ya kumwezesha kukopa hata katika taasisi nyingine za fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaliona hili kama njia moja ya kuboresha maisha ya Watanzania hasa wafanyakazi na itazidi kuishawishi mifuko ya jamii, sio tu kutoa mikopo lakini pia kujihusisha zaidi katika huduma za kijamii kama vile afya, elimu, michezo, na kadhalika kwa lengo la kuwasaidia wanachama na Watanzania kwa ujumla.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nina swali dogo moja tu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru jinsi mifuko hii imekuwa ikiwakopesha wafanyakazi ambao ni wanachama. Mimi nilikuwa nina pendekeza, kama Serikali inakubali, kwa kazi hiyo nzuri inayofanya ni kwanini wasijikite zaidi katika kuwajengea nyumba hawa wafanyakazi ambao kipato chao ni kidogo ili watakapokuwa wamestaafu wawe na uhakika wa kuishi katika nyumba zao kuliko hali ya sasa kujiweka katika kuwekeza zaidi? *(Makofi).*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikopo hii inayotolewa kwa wanachama na mifuko yetu na inatolewa kwa mwanachama mmoja mmoja ni moja ya mikakati ya mifuko hii ya kumuwezesha mwanachama kustaafu akiwa na makazi. Lakini mifuko hii ina mkakati wa pili wa kujenga nyumba kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge na kuwauzia wanachama wake. Lakini pia pamoja na wananchi wengine ambao watataka kununua zile nyumba. Mfano mzuri ni mfuko wa *PPF* ambao umejenga nyumba kule Mwanza eneo la Kiseke na kati ya zile nyumba 90% ya walionunua mpaka sasa hivi ni wanachama wa mfuko wenyewe.

Lakini vilevile mfuko wa *NSSF* una mpango wa kujenga nyumba kule Kigamboni, Dar-es-Salaam, Tuangoma pale na Kijichi kwa madhumuni hayohayo. Vile vile *PPF* wana mpango wa kujenga nyumba 300 kule Iringa na lengo ni hilohilo. Kwahiyo namshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa kutukumbusha kwamba ni jambo jema

kwa mifuko hii kujielekeza kujenga nyumba ambazo wanachama na Watanzania wengine washiriki katika mifuko hii waweze kununua. *(Makofi).*

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza; kwa kuwa mifuko hii inawasaidia sana watumishi pale ambapo wakati wa kustaafu ukifikia; na kwa kuwa kuna matatizo mengi ya uwekaji wa kumbukumbu za watumishi wanaopitisha mafao yao kupitia kwenye mifuko hiyo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza akalifahamisha Bunge hili Tukufu kwa matatizo ambayo walikuwa wameyapata watumishi waliokuwa wa Jumuiya ya afrika Mashariki wanateseka kwa ajili ya kupata mafao yao, kumbukumbu zao haziko sahihi kwenye Wizara. Je, kwa watumishi wa mifuko hii aliyoitaja, yuko tayari kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba kumbukumbu sasa zitakuwa sahihi ili watumishi wanapofikia muda wa kustaafu mafao yao wayapate kwa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali Mheshimiwa Maneno, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumuhakikishia kwamba mifuko hii sasa inaweka kumbukumbu sahihi kwa njia za kisasa za mawasiliano na kwahiyo tunaamini kwamba pale mstaafu anapoondoka kazini ataweza kupata kumbukumbu za kuridhisha na zilizo sahihi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wastaafu wa Afrika Mashariki na nyaraka zao, napenda kusema kwamba wale ambao wamelipwa nyaraka zao ni sahihi na wengi wa wale ambao hawajalipwa si kwamba nyaraka zao sio sahihi ni kwamba mara nyingine hazipo. Kwa maana ya kwamba kama hazipo yale mashirika, na sio Serikali, yale mashirika ambayo yalikuwa yamewaajiri yanatuambia ya kwamba huyu hakuwa mfanyakazi wetu. Hatuna ushahidi ambao unaonesha kwamba nyaraka tunazopokea na ambazo zimekuwa msingi wa kuwalipa ni nyaraka ambazo sio sahihi.

Na. 77

**Kupambana na Ugonjwa wa Kifafa cha Mimba**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, akina mama wajawazito hupoteza maisha kabla ya wakati wa kujifungua kwa kupata ugonjwa wa kifafa cha mimba:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kupambana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifafa cha mimba ni moja ya visababisho vinavyoleta shinikizo la damu linaloibukia wakati wa ujauzito. Hali hii ya shinikizo la damu husababisha asilimia 9 ya vifo vya wajawazito vinavyotokea kabla ya kujifungua, wakati wa kujifungua na ndani ya wiki sita baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ujuzi na uelewa wa kisayansi uliopo hapa duniani sasa hivi chanzo cha ugonjwa huu hakifahamiki, kwasababu hiyo basi inakuwa ni vigumu kuweka mikakati ya moja kwa moja ya kuzuwia ugonjwa huu. Lakini kwa vile dalili za awali zinajulikana, msisitizo umejikita katika kuwatambua wagonjwa hawa mapema ili wapewe tiba sahihi ambayo itasaidia kupunguza madhara yanayoweza kutokea kwa mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, dalili za mwanzo kabla mama hajapata kifafa cha mimba ni pamoja na hizi zifuatazo; shinikizo la damu kwa mwanamke ambaye mwanzoni mwa ujauzito hakuwa nalo, protini ndani ya mkojo na kuvimba miguu. Asilimia kubwa ya waathirika ni wale wanaopata mimba kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuhakikisha kifafa cha mimba hakitokei na kupunguza madhara yake kama kitatokea ni juhudi za watoa huduma ya afya pamoja na jamii ya wananchi. Baadhi ya mikakati iliyopo ni hii ifuatayo:-

- Kutoa elimu ya afya kwa umma ili wananchi watambue umuhimu wa mwanamke mjamzito kuwahi kwenda kliniki ya wajawazito ili kuweza kugundua viashiria vya awali vya kifafa cha mimba na hivyo kupewa matibabu mapema.

- Kuelimisha jamii kuwa ugonjwa huu hautokani na kulogwa.

- Kuwahusisha wanajamii kutoa ushirikiano katika kuwahudumia wanawake wajawazito, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia usafiri wa kumfikisha mgonjwa kwenye kituo cha afya.

- Kuwawahisha hospitalini wale wote ambao kwa bahati mbaya watapata kifafa cha mimba wakiwa nyumbani.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza na ninashukuru…

**SPIKA:** Tafadhali inua zaidi hicho chombo, umekiweka chini mno. Naam.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yake mazuri napenda kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, baadhi ya wasichana wengi mashuleni wanapopata mimba huacha shule na kurejea nyumbani. Wanaporejea nyumbani huwa hawaendi kliniki kupata huduma ya chanjo na baadhi yao hufa baada ya kujifungua na kabla ya kujifungua kwa kupata kifafa cha mimba, lakini huwa hawaendi kwa kuona aibu. Je, Serikali kupitia sekta ya afya inaonaje kutoa mafunzo kwa wasichana mashuleni angalao mara mbili kwa mwaka ili wasichana hao wakati wa ujauzito waweze kufika klinini na kupata huduma hasa ikiwa ni mimba ya mara ya mwanzo ili kupunguza vifo vya aina hiyo? *(Makofi).*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo; naomba nichukue ushauri wake na tutajadiliana na wenzetu wa Wizara ya Elimu. Lakini vilevile tuna wasiwasi kwamba tutakuwa kama tunahalalisha kwamba hii shughuli iendelee na tuwape ushauri kabla hawajapata mimba. Nadhani kubwa ni kwamba tujaribu kuzuwia hiyo mimba, lakini elimu itaendelea kwa watu wote ikiwa ni mashuleni au mahali popote.

Na. 78

**Watu Wanaoambukiza UKIMWI kwa Makusudi**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa, *UKIMWI* ni Janga la Kitaifa na kwa kuwa kuna baadhi ya waathirika wa *UKIMWI* huambukiza watu wengine kwa makusudi kwa kuwa na mahusiano yasiyo salama:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu watu hao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, napenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, muswada wa sheria ya kuzuwia na kudhibiti virusi vya *UKIMWI, The HIV/AIDS Prevention and Control Act, 2007,* ulipitishwa na Bunge lako

tarehe Mosi Februari, 2008 na kupata idhini ya Rais, *Assent,* na kuwa sheria ya nchi tarehe 4 April, 2008. sheria hiyo inalenga kuongeza kasi na ufanisi zaidi katika mbinu na mikakati mbalimbali ya kuzuwia na kudhibiti virusi vya *UKIMWI* humu nchini.

Mheshimiwa Spika, sheria hii pamoja na mambo mengine inajikita kwenye masuala ya huduma za afya na kijamii, haki na wajibu wa yatima na wajane, elimu ya afya kwa umma, kuondoa ubaguzi na unyanyapaa, kutunza siri ya mtu anayeishi na *VVU* na kuweka utaratibu wa kisheria wa kuvunja usiri huo pale inapobidi, kusimamia tafiti mbalimbali za *VVU/UKIMWI* na magonjwa nyemelezi, kutoa adhabu kwa waathirika watakaothibitika kuwa wanaambukiza wenzao *VVU/UKIMWI* kwa makusudi, na kadhalika. Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watu wanaoeneza *UKIMWI* kwa makusudi wanatenda kosa la jinai na ikiwa watathibitishwa kuwa wameambukiza wenzao virusi vya *UKIMWI* kwa makusudi, watapewa adhabu kali. Adhabu ya kosa hilo kwa mujibu wa sheria ya kudhibiti *UKIMWI* ni kifungo ambacho siyo chini ya miaka mitano na kisichozidi miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maudhui ya sheria hii yameanza kutekelezwa lakini mengine yanangojea kanuni. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wadau mbalimbali, Wizara yangu ipo katika mchakato wa kuandaa kanuni zitakazotumika katika suala hili la kuambukiza kwa makusudi. Baadhi ya masuala yatakayowekewa msimamo ni kama vile namna ya kuthibitisha kuwa muathirika alijua ana *VVU* na ametenda kosa kwa makusudi au kama mahusiano ya kingono yalikuwa ya maafikiano au mmoja kalazimishwa. Kwa kumalizia naomba nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na wananchi wote kwa jumla tusaidie juhudi hizi kwa kujitokeza na kuwafichua wale wote wenye tabia hii mbaya ya kueneza *VVU* kwa makusudi.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyiongeza. Tangu sheria hii ipitishwe. Je, ni watu wangapi wamehusishwa na kuchukuliwa hatua? Ahsante.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, hatujaweza kumbana hata mmoja. Ahsante.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, hivi sasa hakuna utaratibu wa kuweka bayana kwa wale ambao wana virusi vya *UKIMWI,* na kama wanawekwa bayana imani yangu kwamba hawatarithisha wengine kuathirika kwa maradhi yao hayo.

Huoni kwamba sasa ni wakati muafaka Serikali kuwa na mpango wa kuweka bayana kwa wale wote ambao wana virusi vya *UKIMWI* na kuondoa ile mawazo ya kwamba wanavunja haki za binadamu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nimemwelewa kuwekwa bayana ni kwamba watambulike kwa namna moja au nyingine. Na wakati tunajadili muswada huu kuna wengine walizungumzia habari za kuwaandika kwenye paji la uso ili wajulikane mahali popote wanapokwenda lakini Bunge lilikataa.

Lakini yote hii inaendana na haki za binadamu, tunachotaka ni kwamba watu wajitokeze kwasababu sasa tuna uwezo wa kuweza kuwasaidia. Ikiwa tutaamua kufanya hivyo kwa ugonjwa wa *UKIMWI*, kuna magonjwa meengi sana, mtu akipata kisonono itabidi naye tumuandike, akipata malaria itabidi tumuandike nah ii itafanya juhudi zetu za kufanya wajitokeze na tuweze kuwatibu zitakuwa hazifiki mahali na nia ni kuwafanya wajitokeze tuweze kuwatibu ili tuweze kuzuwia watu kueneza kimya kimya. Ahsante.

Na. 79

**Kuanzisha *Client Service Charter* Kwa Majaji**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, hakuna *Client Service Charter* kwa Majaji na Mahakimu wa Mahakama za Tanzania:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kurekebisha hali hiyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania inayo *Client Service Charter* ambayo inawahusu Majaji, Mahakimu na Watumishi wote wa Mahakama. Hakuna mkataba wa huduma kwa wateja unaowahusu Majaji na Mahakimu pekee, kwani majukumu ya Mahakama hayatekelezwi na Majaji na Mahakimu pekee. Majukumu ya Mahakama hutekelezwa kwa ushirikiano wa watumishi wote wa Mahakama kwa kuzingatia taaluma ya kila mmoja wao.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa kwa niaba ya wananchi wa Kongwa na wananchi wa Tanzania kwa ujumla, swali langu halikujibiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, swali langu linasema kwa kuwa hakuna *Client Service Charter* kwa Majaji na Mahakimu wa Mahakama za Tanzania, kwahiyo na mimi mwenyewe nimesema haipo, swali langu sasa linauliza. Je, Serikali ina mipango gani ya kurekebisha hali hiyo? Swali hilo halijajibiwa. Kwahiyo, naomba sasa Mheshimiwa ajibu swali langu. *(Makofi).*

**SPIKA:** Lakini ninalo jibu ambalo limesomwa hapa linasema. Mahakama ya Tanzania inayo *Client Service Charter.* Nadhani ndio jibu hilo, hakukubaliana na wewe kwamba haina anasema inayo. Sasa tatizo ni lipi sasa?

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu lake lenye sentensi saba tu, sentensi ya tatu anasema hakuna mkataba wa huduma kwa wateja unaowahusu Majaji na Mahakimu pekee. Kwahiyo, anakubaliana na mimi. Na mimi ndicho nilichosema kwamba haupo. Nimeuliza sasa Serikali ina mpango gani wa kurekebisha jambo hilo? Ndilo jambo ambalo hajalijibu, ninamwomba alijibu. *(Makofi).*

**SPIKA:** Nasikitika leo ninahitilafiana na rafiki yangu Job Ndugai, jibu linajitosheleza kabisa kwasababu maelezo yanasema hivi. Majukumu ya Mahakama hutekelezwa kwa ushirikiano wa watumishi wote, ndio maana mkataba wa huduma wa Mahakama ni wa watumishi wote. Yaani upate huduma ya Mahakama, naona linatosheleza. Tunaendelea na swali jingine.

Na. 80

**Gharama za Kusafirisha Watuhumiwa na Mgambo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Namtumbo Wananchi wamekuwa wakilalamikia Mahakama ya Mwanzo juu ya mlalamikaji kulipia gharama za kusafirisha watuhumiwa na Mgambo:-

Je, Serikali inaweza kuchukua jukumu hilo kwani ndiyo yenye dhamana ya usalama wa wananchi na mali zao?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wamekuwa wakilipia gharama za usafirishaji wa watuhumiwa Mahakama za Mwanzo.

Utaratibu huu unatumika si katika Wilaya ya Namtumbo pekee bali karibu nchi nzima. Aidha, ni kweli kwamba yamekuwepo malalamiko mengi kwa wananchi juu ya utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, hali hii imetokana na mvutano uliokuwepo wa nani agharamie usafirishaji mahabusu kati ya Polisi, Serikali za Mitaa au Magereza toka Mahakama za Mwanzo kwenda Mahabusu na kuwatoa Mahabusu kuwapeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Fungu la 70(1) (2) la Sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11, *Magistrate's Court Act Cap. 11,* linaeleza wazi kwamba anayehusika na kuhudumia wafungwa na mahabusu ni Wizara ya Mambo ya Ndani. Hata hivyo kwa kipindi kirefu ulikuwepo utata juu ya nani awasafirishe mahabusu hao kutoka Mahakamani kwenda mahabusu na kuwatoa huko kuwafikisha mahakamani. Baada ya kubaini tatizo hilo imeweka bayana kwamba jukumu la kusafirisha mahabusu sasa liko chini ya Wizara na hasa Idara ya Magereza. Utekelezaji wake umeshaanza kwa awamu kwa kuanzia Mkoa wa Dar-es-Salaam na utasambaa nchi nzima hivyo kumaliza kabisa tatizo hili na malalamiko ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati huu tunaomba wenzetu waangalie uwezekano wa kurejesha utaratibu wa awali wa kuzifanya Halmashauri za Wilaya kuwa Mawakala wao vijijini, wa kutoa huduma ya kusafirisha Mahabusu na wafungwa ili tuweze kuwaondolea wananchi wetu kero hii.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa malalamiko haya ni ya muda mrefu na yamefanya watuhumiwa wengi kuachiwa huru kwasababu ya mtuhumu kukosa uwezo wa kuweza kumsafirisha mtuhumiwa na hivyo kusababisha vitendo vya uvunjaji wa sheria kuweza kuendelea hasa kule vijijini vya wizi wa mazao. Na kwa kuwa, Mwanasheria Mkuu, wakati akijibu swali lake kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, amesema wameomba wenzetu waangalie uwezekano wa kurejesha utaratibu wa awali wa kuzifanya Halmashauri za Wilaya kuwa mawakala wa kutoa huduma hiyo ya kusafirisha mahabusu ili kuwaondolea kero wananchi.

Je, kwa kuwa karibu Serikali nzima ipo hapa, inaweza kutoa tamko na kuziwezesha Halamshauri kifedha kuweza kufanya kazi ya huduma hii kwa utaratibu utakaowekwa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba

nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi tumetoa mapendekezo tu kwa wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ili waangalie uwezekano wa kushirikisha Halmshauri ili nazo ziweze kushughulikia mahabusu kutoka kwenye mahabusu kuelekea Mahakamani na kutoka Mahakamani kwenda mahabusu.

Kwa hiyo, suala hilo la kuwezesha Halmashauri kuweza kulishughulikia tatizo hilo nadhani wenzetu wamelisikia, kwa hiyo watalifanyia kazi.

Na. 81

**Kuanzishwa kwa Mnada wa Upili – Mwanza**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikihimiza wafugaji kufuga kitaalamu ikiwa ni pamoja na kupunguza mifugo; na kwa kuwa, Serikali pia imeamua kuhamisha mnada wa Upili uliokuwa Igoma, Mwanza na kujengwa Misungwi kijiji cha Ng'ombe eneo la Nyamala:-

(a) Je, ni lini mnada huo utakamilika ili wafugaji wa Kanda ya Ziwa wauze mifugo yao hapo?

(b) Je, Serikali itakamilisha lini upungufu wa fedha kumalizia ujenzi wa eneo la kupakilia/kupakulia na kunyweshea mifugo?

(c) Je, Serikali inatoa wito gani juu ya matumizi ya mnada huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa wa Misungwi, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kuhamisha mnada wa Upili wa Nyamhongolo, uliopo eneo la Igoma, katika Jiji la Mwanza kutokana na kusongwa na makazi ya watu ambako kunatokana na kukua kwa jiji hilo. Wizara yangu ilitafuta eneo eneo jipya ambalo lipo nje kidogo ya jiji na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi tuliweza kupata eneo la Nyamatala ambako tuliafikiana mnada huo ujengwe. Hadi sasa ujenzi wa mazizi, eneo la kunadi mifugo, mabona manne ya kuhifadhi ng'ombe wanaoingia mnadani na waliouzwa na ofisi katika mnada huo

umekamilika. Kazi za msingi zilizobaki ambazo zitawezesha mnada kuanza kufanya kazi ni kujenga vyoo, eneo la kushusha na kupakia mifugo na kujenga birika la maji kwa ajili ya mifugo zinazotarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha 2008/2009. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa ujenzi wa mnada wa Nyamatala umegharimu jumla ya shilingi milioni 46. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara yangu imetenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya kumalizia kazi za msingi ili kuwezesha mnada kuanza kufanya kazi.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa wito kwa wafugaji wa Misungwi na mikoa ya jirani na Mwanza kufuga mifugo yao kisasa na kibiashara ili mara mnada utakapokamilika waweze kuuza mifugo yao katika mnada huo na kujipatia kipato kizuri na kuondoa umaskini. Aidha, Wizara yangu inaishauri Halmashauri ya Misungwi kuwahamisha wananchi wakiwemo wafugaji kutunza vyema mnada huo kwa maslahi yao. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumetumia mnada huo kikamilifu na kwa malengo sahihi yaliyokusudiwa katika kuujenga.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninaomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri swali langu la msingi hajalijibu kiusahihi hasa, ni lini mnada huo utakamilika ili wafugaji wa Kanda ya Ziwa wauze mifugo yao pale?

Kwa hiyo, lini hajaeleza, isipokuwa ameeleza kwenye D kwamba ametenga milioni 50, kutenga ni kutenga wakati mwingine hata hizo pesa hazijapelekwa huko, nataka anieleze ni lini na hizo pesa milioni 50 zimeshapelekwa huko? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amekuwa akitutaarifu kuhusu ujio wake wa ziara yake Wilayani Misungwi mara mbili huko akiahirisha bila taarifa za msingi, hebu anihakikishie leo baada ya mkutano huu anasema nini kuhusu ujio wake katika Jimbo la Msungwi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Jacob Shibiliti kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi zilizobaki ni chache na milioni 50 hizi zimetengwa katika Bajeti ya mwaka huu na mpaka sasa tumepata milioni 12 kutoka Hazina na hizo fedha zinatakiwa kutumwa huko wakati wowote, nataka nimhakikishie kwamba mwaka huu mnada huo utaisha na utaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, nataka kumhakikishie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili ……………………..

**SPIKA:** Una maana Mheshimiwa mwaka wa fedha nadhani, maana yake mwaka huu sasa umebaki miezi ……………………..

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nina maana mwaka 2008/2009 mnada huo utakamilika na utaanza kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu b, kweli ni kwamba nimewahi kuandika huko kwamba nitaenda kutembelea Wilaya ya Misungwi lakini kwa sababu ya kazi nyingi sikwenda, napenda kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla ya Bunge lijalo nitakuwa nimetembelea Wilaya ya Misungwi kuona matatizo ambayo yanawakabili wafugaji. (*Makofi*)

Na. 82

**Kazi ya Wavuvi**

**MHE. SHOKA KHAMISI JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa uvuvi ni kazi inayowapatia riziki Watanzania; na kwa kuwa wapo wavuvi wanaovua baharini; kwenye maziwa na kwenye mito lakini wavuvi hao hasa wale wadogo wadogo wamekuwa wanasumbuliwa na kunyanyaswa na vyombo vya dola kwa visingizio vya mazingira:-

(a) Je, ni uvuvi gani unaoruhusiwa kisheria na ni halali kuvua kwenye bahari?

(b) Je, ni uvuvi wa aina gani unaoruhusiwa kisheria; na, ni halali kuvua kwenye maziwa na mito?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamisi Juma, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uvuvi unaoruhusiwa kisheria kuvua kwenye bahari, ziwani, mabwawa na mito ni ule ulioainishwa kwenye Sera ya Uvuvi ya mwaka 1997 na kufafanuliwa kwenye Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2005. Pamoja na Sheria ya Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Deep Sea Fishing Authority Act*) ya mwaka 1989 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2007 sura 388). Aidha kwa

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni Sheria Na. 8 ya mwaka 1988 ikisomwa kwa pamoja na marekebisho ya mwaka 1998.

**MHE. SHOKA KHAMISI JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kabla ya kuuliza maswali ya nyongeza nashukuru kwa niaba ya wavuvi kwa kauli ya Mawaziri iliyotolewa hapa na Mheshimiwa John Magufuli ya kuwaruhusu wavuvi kuweza kuzama kwa kutumia miwani kwa kuogelea na viatu pamoja na mambo mengine aliyoyaruhusu katika kauli yake aliyoitoa hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hiyo nina maswali mawili ya nyongeza, siku ya tarehe 30 Juni, 2008 mnamo saa 11 jioni boti nne ambazo zimewekwa kwenye mialo zilichukuliwa nyavu zao na askari wa vyombo vya dola na kuzipeleka sehemu waliyotaka wenyewe, na kwa kuwa tokea siku zilizochukuliwa nyavu hizo wenyewe mpaka leo hawajakabidhiwa na ni watu maskini na askari hao walidai kuwa wanatekeleza waraka wa Mkurugenzi wa Uvuvi na ambao kuwa hata haukutajwa katika majibu haya aliyonijibu Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa nauliza.

Je, ni lini wavuvi hao watapewa nyavu zao ili wapate kuendeleza maisha yao pamoja na watoto wao? Swali la kwanza hilo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa nyavu hizi zipokuwa zikichukuliwa zilikuwa zimewekwa kwenye mialo na zilizokuwa ndefu hawa askari walizokuwa wanaziona ndefu walikuwa wakizikata ili wapate mapande wayapeleke kwenye magari, sasa nauliza kwa nchi ya sheria kama hii Tanzania kumkatia mtu nyavu yake usiweze kuichukua nzima na ukaikata kipande ukaipeleka kwenye gari, kwa nchi kama hii ya Tanzania tunaofuata sheria pamoja na utawala bora, je, ni haki kumkatia mtu nyavu yake? Na wale waliokata nyavu za hawa wavuvi watachukuliwa hatua gani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Shoka Khamisi Juma kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, taarifa tuliyoitoa Bungeni wakati tukitoa ufafanuzi wa waraka wa Mkurugenzi ulizingatia sheria ya uvuvi, lakini pia katika majibu yetu ya leo tuliyoyatoa hapa yamezingatia sheria namba 22 ya mwaka 2003 ambayo yanahusu sheria ya uvuvi pamoja na kanuni zake za mwaka 2005, lakini pia yamezingatia katika upande wa Zanzibar sheria namba nane ya mwaka 1988 na mabadiliko yake ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukamatwa kwa hawa aliowazungumza wavuvi tarehe 30 mwezi Juni mwaka 2008, kitu kikubwa hapa kinachohitajika ni kuzingatia sheria, tunazingatia sheria katika kuhakikisha kwamba uvuvi haramu hauendelezwi katika maziwa yetu, katika bahari zetu na sehemu nyingine zote.

Mheshimiwa Spika, kukamatwa wanaovua kwa kuvunja sheria wataendelea kukamatwa wawe katika Ziwa Victoria, wawe katika Bahari ya Hindi, wawe katika mito,

wawe katika mabwawa kwa kuzingatia sheria namba 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kama wataona kwamba hao wamekamatwa wameonewa mahakama zetu ziko huru wana haki ya kwenda kufungua kesi na kushtaki kuhusu uonevu wao lakini suala la kuzingatia sheria ili tulinde rasilimali zetu ni lazima tulizingatie.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tu, hivi karibuni tulikuwa kwenye mkutano kule Kampala ukizungumzia masuala ya *Lake Victoria Fisheries Organisation*, samaki aina ya sangara sasa hivi wamepungua sana kutoka tani 750,000 waliokuwepo katika mwaka uliopita sasa wako tani 315,000 katika *research* iliyofanyika mwaka huu na katika viwanda vilivyokuwa katika ukanda wa Ziwa Victoria vilikuwepo 35 sasa vimefungwa 10 na vile vilivyobaki vinafanya kazi chini ya kiwango kwa hiyo ni lazima tuchukue hatua katika kuzingatia kulinda rasilimali zetu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri mambo ni makali kweli kweli na ninaiomba Serikali sasa ifanye *operation* sangara iliyo ya dhahiri ili sangara waongezeke, siyo *operation* sangara zilizo feki feki hizi, tunamalizi swali la mwisho Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi linauzwa na Mheshimiwa Raynald Mrope. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 83

**Kuimarisha Ulinzi Shule za Sekondari ya Wasichana Masasi**

**MHE. RAYNOLD ALFONCE MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali licha ya kuwa na mpango wa kujenga na kuendeleza madarasa mapya nchini chini ya mpango wa kujenga MMES inalo jukumu la kukarabati na kuendeleza shule za zamani za sekondari; na kwa kuwa, Sekondari ya Wasichana Masasi inakabiliwa na tatizo la kukosekana kwa uzio hivyo kuhatarisha usalama, amani na utulivu shuleni hapo.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba majambazi yanaingia na kutoka saa yoyote Shule ya Sekondari Masasi na mwaka huu peke yake yametokea mauaji mara mbili, wizi wa fedha, vifaa vya vitisho vya mara kwa mara vya ukabaji kwa wasichana wa shule hiyo?

(b)Kwa kuwa, kukosekana kwa ulinzi na usalama shuleni hapo kumefanya hata walimu kupigwa na kuumizwa na majambazi na vibaka, wanafunzi kutukanwa na mali zao kuibiwa; je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kuinusuru jamii kwa kujenga uzio?

(c)Je, Serikali itadhibitisha, vipi utoro wa wanafunzi wanaotumia nafasi hiyo ya ujambazi na kutokuwa na uzio kutoroka kwenda kufanya vitendo viovu mjini wakiwa wamefuatwa na wapenzi wao usiku bila kizuizi chochote?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Raynold Alfonce Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu a, b na c naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) imekuwa ikizifanyia ukarabati shule kongwe za Serikali kwa awamu kutokana na ufinyu wa Bajeti. Wakati Serikali inafanya jitihada za kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya shule hii pamoja na shule nyingine zenye matatizo kama hayo, tunashauri Halmashauri na Menejimenti ya Shule na jamii kutafuta namna ya kutatua tatizo la uzio kutokana na vyanzo vyao vingine.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

(a)Serikali inafahamu matatizo yaliyotokea katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi hata kusababisha mlinzi wa shule hiyo kuuawa na hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwemo ya kuvishirikisha vyombo vya dola katika kulishughulikia suala hili.

(b) Ili kukabiliana na tatizo hili la ukosefu wa uzio, Serikalil inashauri Halmashauri na Menejimenti ya shule kutafuta namna ya kutatua tatizo la uzio kutokana na vyanzo vyao mbalimbali, kufanya tamasha au kutafuta wafadhili wa kusaidia. Serikali itashirikiana na jamii ya Masasi katika jitihada hizi.

(c)Serikali inatambua kuwa kujenga uzio kutasaidia kudhibiti utoro wa wanafunzi wanaoondoka shuleni kwenda kufanya vitendo viovu. Hata hivyo suala la kudhibiti utoro liko chini ya Uongozi na Menejimenti ya shule, kwa hiyo uongozi wa shule uweke mikakati thabiti ya kusimamia wanafunzi wasitoroke.

**SPIKA:** Swali fupi la nyongeza Mheshimiwa Raynald Mrope.

**MHE. RAYNOLD ALFONCE MROPE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii, pamoja na majibu ambayo hayakuridhisha sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa niulize maswali mawili kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Sekondari ya Masasi ni sekondari ya Kitaifa na tatizo hili la uzio ni la siku nyingi. Kwa nini Wizara ikwepe wajibu wake wa kutekeleza hili na

kutupia Halmashauri ya Wilaya ambayo kwa kweli haina jukumu hilo.  Kwa nini Wizara isitafute fedha hizo na kufanya kazi hii. (*Makofi*)

Kwa nini Serikali isiwe na mpango maalum wa kuzikarabati shule hizi za sekondari zilizo katika wilaya yangu ya Ndanda, Masasi na Chidya ambazo ziko katika hali mbaya sana hakuna mabweni ya kutosha, maji machafu hasa katika ile Shule ya Sekondari ya Ndanda, madeni mengi hizi shule zote zimeachiwa, sasa hii kazi ifanywe na nani badala ya kufanywa na Wizara ya Elimu, nani wanaotupiwa sasa hivi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mrope kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, jukumu la kulinda, kuzijenga, kukarabati ni la Serikali kuu pamoja na wananchi kwa ujumla shule hizi ni zetu sote na hivi sasa Serikali imegatua madaraka shule hizi zinapelekwa TAMISEMI maana yake ziwe karibu zaidi na wananchi. Kwa hiyo ndio maana tumeelekeza kwamba Halmashauri na bodi ya shule inalo jukumu inaweza kukaa na kutafuta utaratibu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuarifu shule nyingi zimefanywa hivyo na zimefanikiwa, pili anaposema kwamba nini kipaumbele katika kutoa ukarabati, Serikali inao mpango au Wizara inayo mpango wa kuzikarabati shule zote kadri bajeti inavyoruhusu na katika mwaka wa fedha 2008/2009 ziko shule 30 za Kitaifa zitakazo karabatiwa.

Naomba kumshawishi Mheshimiwa Mbunge anao dhamana kubwa, ana uwezo mkubwa wa kushawishi tushirikiane kwa pamoja nami nitamwunga mkono ili shule ile nzuri ya wasichana ambayo binafsi nimeitembelea iweze kupata ulinzi.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo nimalizie.  Ni vema yeye kama Mbunge wa Jimbo lile akapata fursa ya kwenda kutoa nasaha kuwaasa watoto wale wasitoroke inawezekana tukajenga ukuta wakaruka, ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita na maswali yameisha sasa ni matangazo nitaanza kama kawaida na wageni wetu waliomo humu Bungeni leo.

Naanza na wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa , wageni hao mashuhuri ni kutoka Zanzibar ni viongozi wa *SMZ* kama ifuatavyo kwanza ni Mheshimiwa Suleiman O. Nyanga Waziri wa Tawala za Mikoa na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, karibu sana Mheshimiwa Waziri tunafurahi sana kukuona hapa kuendeleza mshikamano wetu katika nchi yetu, ameambatana na Mheshimiwa Hassan Wambi,  Katibu Mkuu wa

Wizara hiyo ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, pamoja nao wapo maafisa mbalimbali wa Tawala za Mikoa kule Zanzibar naomba tafadhali wageni msimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwaona, karibuni sana na pia wamesindikizwa na maafisa wa Wizara ya TAMISEMI, ahsante. (*Makofi*)

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa *Dr*. Milton Mahanga Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ambao ni wanafunzi 30 na walimu sita kutoka Shule ya Awali ya Mtakatifu Scolastika Gongo la Mboto huko Ukonga Dar es Salaam, ahsanteni watoto simameni, kweli hawa Shule ya Awali, ahsanteni sana, naomba walimu *Sister* baada ya hapa wapate chai naona wamechoka sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Gaudentia Kabaka Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambao ni wanafunzi 45 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosoma Shahada ya Udhamili, *Masters in Development Studies* wale wa Chuo Kikuu cha Dodoma naomba wasimame tafadhali, ahsanteni sana, tumefurahi kuwaona hapa wasomi wetu na tunawatakia mema katika kujiandaa kupata elimu zaidi ya kulitumikia Taifa la Tanzania, ahsante sana. Mgeni wa Mheshimiwa Ramadhani Maneno ni Ndugu Mbaraka Tamim ni mjumbe wa mkutano mkuu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya na Mkoa na ni mshauri wa siasa Jimboni. Huu ni utaratibu mzuri sana tena bado kijana kijana tu. Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhani Maneno utaratibu huu unavutia wa kuwa na mshauri wa kisiasa ndani ya jimbo. (*Makofi/Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa Juma Killimbah ambaye ni Ndugu Shaban Rashid Kole, Mwenyekiti wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Iramba, ahsante sana, karibu sana. Wageni wa Mheshimiwa Damas Nakei ambao ni bibi Albina Anthony Mwenyekiti wa Kijiji cha Moyomayoka. Kweli kina mama wanaweza na Bwana John Ombai Mtendaji wa Kijiji hicho hicho cha Moyomayoka. Kwa hiyo, hapa mnaona Mama Albina ndio *boss* wa Bwana John, ahsante pongezi sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mkuu mpya wa Idara ya Siasa na Uchumi kutoka Ubalozi wa Marekani hapa nchini Bwana Carl Fox ameambatana na Bibi Justina Mdobilu, Mr. Carl Fox *you are very welcome to the chamber. We are very happy to see you here,as you kow we have a good relations between the Tanzania and United States so cordially and we wish you well in your general elections today*. Wako wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, Wanachuo cha Mipango wale pale, ahsante sana.

Kwa niaba ya Wabunge ninawatakia mafanikio katika mafunzo yenu. Wapo pia wanafunzi 26 kutoka Chama cha Wanafunzi wanaosoma Sayansi ya Siasa Chuo Kikuu cha Dodoma. Naona wamejitenga na wenzao hawa tayari wameanza ukorofi wa kisiasa, tunawatakia mema na tunadhani mtashughulika zaidi na nadharia ya siasa kuliko kutuandama kwenye majimbo. (*Makofi/Kicheko*)

Kipo kikundi cha walemavu Chinganga *Cultural Information and Entertainment* toka Arusha waliokuja kukutana na Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya uzinduzi

wa filamu inayoitwa Ningekuwa Rais, inayoonyesha matatizo wanayoyapata walemavu Tanzania, sijui wako wapi, ahsante sana na karibuni sana. Bunge hili liko pamoja nanyi katika kuendelea kutatua matatizo mbalimbali yanayowakumba kundi hili maalum katika nchi yetu, karibuni sana.

Mwisho wanafunzi wawili kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao wamekuja Bungeni kufanya utafiti kuhusu *Information Seeking Behaviour of Members of Parliament*, hawa wanatuchunguza siye hawa, *Information Seeking Behaviour*, nao ni Ndugu Chausiku Mwinyimbegu na mwenzie Ndugu Pili Mkuki, Wale pale, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge mshirikiane na watafiti hawa wanaotuchunguza siye nadhani kwa faida ya Bunge na kwa faida ya nchi, karibuni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Matangazo ya kazi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii atika mkutano leo saa tano asubuhi maana yake mara baada ya kipindi hiki cha maswali, Ukumbi Namba 227.

Mheshimiwa Estherina Kilasi, Makamu Mwenyekiti Kamati za Hesabu za Mashirika ya Umma anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma mkutane mara baada ya kipindi hiki cha maswali katika ukumbi namba 231 mara baada ya matangazo haya, Waheshimiwa Wabunge, wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kuna kikao leo saa saba na nusu katika Ukumbi wa Spika.

Katibu anatangaza kwamba wale Wabunge wote ambao walihitaji kukutana Ndugu Carl Fox mara baada ya matangazo haya wakutane nae pale Ukumbi Namba 219 jengo la utawala, nadhani kuna Waheshimiwa walikuwa na miadi maalum basi atakuwa pale Ukumbi Namba 219 mara baada ya kipindi hiki.

Katibu pia ananiomba nitangaze kwamba Waheshimiwa Wabunge wote ambao wangependa kushuhudia matokeo ya uchaguzi wa Marekani shughuli hiyo ambayo itaambatana na kifungua kinywa sijaelezwa hapa kinatolewa bure au ni cha kulipia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaambiwa hapa kuwa ni cha bure. Kitatolewa saa moja na nusu asubuhi kesho. Unajua hapa tofauti za saa ingawa wanapiga kura leo tofauti ipo kama saa nane hivi mpaka saa kumi hivi.

Kwa hiyo, kesho asubuhi ambayo kwa America itakuwa ndio usiku matokeo ndio yatakuwa yanatoka na wenzetu kwa sababu wana ufanisi katika kutumia vyombo vya kisasa *electronic system.* Wakati huo itakuwa kila *State* au kila jimbo litakuwa linaonyeshwa jinsi ambavyo limepiga kura.

Kwa hiyo, kuanzia saa moja na nusu mtaona matokeo pale *New Dodoma Hotel* kesho tarehe tano saa moja na nusu asubuhi. Mheshimiwa *Dr*. Binilith Mahenge, Katibu wa Wabunge wa Mkoa wa Iringa ameniomba nitangaze kwamba mara baada ya matangazo haya kutakuwa na kikao cha Wabunge wote wanaotoka Mkoa wa Iringa kwenye Ukumbi Namba 133.

Zoezi la uteuzi wa Uchaguzi wa uwakilishi wa Bunge kwenye mabaraza ya vyuo ni kama ifuatavyo hadi jana saa kumi mwisho wa kupokea maombi ya wagombea kwa Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili ambayo ni nafasi moja aliyejitokeza ni mgombea mmoja tu, Mheshimiwa Pindi Chana. Kwa hiyo, kesho tutapiga kura za ndiyo au hapa au mtakavyoamua. Kwa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo tunahitaji watatu wamejitokeza wanne.

Kwa hiyo, ninawatamka ili kampeni ziendelee rasmi sasa. Wabunge hao ni Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa *Dr*. Luka Siyame, Mheshimiwa *Dr*. Ali Tarab Ali na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Sasa ni ruksa kufanya kampeni mpaka kesho ndio tutakapopiga kura. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, *CDA* yaani Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu watakuwa na zoezi la kuuza viwanja kwenye eneo la Itega, eneo zuri sana hewa safi kilimani, kilimani hivi. Itakuwa siku ya Alhamisi tarehe sita mwezi huu yaani kesho kutwa.

Waheshimiwa Wabunge, bei ya mita ya mraba ni shilingi 2,300/= tu na ukubwa wa viwanja ni kati ya mita 32 kwa 50 na 50 kwa 70, vikubwa sana hivi. Masharti kwa kila mwombaji atatakiwa kulipa asilimia 25 siku ya kwanza yaani tarehe sita na hii kwa Wabunge sharti gumu kidogo sijui kama linaweza kulegezwa.

Lakini si unajua tena Wabunge ndio hivyo hivyo mishahara yetu hivyo hivyo, lakini asilimia 25 na unatakiwa uwe umekamilisha malipo ndani ya kipindi cha miezi mitatu.

Kwa hiyo, Alhamisi tarehe 6 Novemba, 2008 itabidi tufanye utaratibu wa *min bus* ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufika eneo la mnada kutakakouzwa hivyo

viwanja. Ni vizuri kujipatia viwanja hivi kila mara hukosei katika ardhi kwa sababu ardhi inapanda tu thamani.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwishowa matangazo na sasa nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata ya shughuli za leo kwenye *Order Paper*. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kutoa Fidia kwa Wafanyakazi wa Mwaka 2008 (*The Workers Compensation Bill, 2008)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wasemaji wangu ni wane, ninaanza na Mheshimiwa Gosbert Blandes badala ya Mheshimiwa Abubakar, kwa sababu amepata udhuru na inambidi mwenzetu aende nyumbani Karagwe ni mbali. Kwa hiyo, baada ya hapo basi ndiyo atakuja Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, halafu Mheshimiwa Pindi Chana, tutamalizia na Mheshimiwa John Cheyo.

Sasa namwita Mheshimiwa Gosbert Blandes.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu. Awali ya yote, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Juma Athuman Kapuya, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. Nampongeza pia Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, kwa kumsaidia vizuri Waziri wake na pia Katibu Mkuu na Watumishi wote ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kama kuna Miswada mizuri imewahi kuletwa Bungeni, huu ni mmojawapo na umenifurahisha sana.

Mimi leo nitachangia maeneo machache kidogo na la kwanza ambalo nataka nilizungumze ni kuhusiana na fidia kwa wafanyakazi wanaoumia wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, kuna jambo moja ambalo limenivutia sana kwamba, kuna mabadiliko yanakuja ndani ya Muswada huu. Siku za nyuma mfanyakazi alipokuwa akiumia kazini au akipata ajali alikuwa anahangaika sana, anatoka ofisi moja hadi nyingine, anaanzia wakati mwingine kwa *Labour Office*, wakati wanamwambia aende kwa Daktari, anazunguka mpaka anafika mahali hata ile haki yake inakuwa imechelewa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Muswada huu uliopo mbele yetu ambao tunategemea iwe Sheria, nimefurahishwa kuona kipengele kinachohusiana na *one stop centre* kwamba, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji *(Director General),* itakuwa na uwezo mkubwa sana wa kupokea malalamiko au *claim* za wafanyakazi walioumia kazini hapo

hapo na kuzifanyia kazi bila mfanyakazi kuhangaika kwenda Ofisi nyingine. Hili limenifurahisha mno. *Director General* kwa kushirikiana na Bodi vilevile atakuwa na uwezo wa kuhakikisha kwamba, wale walioumia wanatatuliwa matatizo yao kwa haraka sana, hili ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ambalo ninataka niliseme ni kwamba, tunachojaribu kukifanya hapa tunajaribu kuunda chombo kimoja cha kushughulikia fidia za wafanyakazi. Ninaposema chombo ni kimoja nina maana ya chombo kimoja kwa nchi nzima, badala ya kuwa na vyombo vingi au kuwa na utitiri wa vyombo vingi vya kushughulikia matatizo au ajali za wafanyakazi, ambacho kitasaidia sana kuondoa urasimu.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu tumekuwa na vyombo vya Mifuko ya jamii kwa mfano, *NSSF*, *PPF* na kadhalika. Ukienda *NSSF* wao wamekuwa na Mfuko mmoja unaoitwa *Employment Injury Benefits*. Mfuko huu umekuwa ukisaidia wafanyakazi wanaoumia makazini, lakini hawa wanaosaidiwa kwa upande wa *NSSF* ni wale ambao ni wanachama wa *NSSF* peke yake, kwa yule ambaye si mwanachama Mfuko huu haumsaidii.

Ukiangalia chini ya Mfuko huu ambao nadhani umeanzishwa takriban miaka kama saba au minane iliyopita, nilikuwa najaribu kufanya *research* ndogo, nimekuta wafanyakazi chini ya Mfuko huu wa *NSSF* kama 100 au pengine hawajafikia idadi hiyo, ndio ambao wanasaidiwa. Sasa ukiangalia wafanyakazi 100 na idadi ya wafanyakazi tulionao nchini, ambao wanaumia ni wengi sana. Kwa hiyo, idadi ya kusaidia wafanyakazi 100 ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mfuko huu unakuja kuwa mkombozi mkubwa sana kwa wafanyakazi wote nchini watakaopata matatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kwamba, tumekuwa na wafanyakazi wa aina mbalimbali, ukiwa na kondakta wa daladala ni mfanyakazi, ukiwa na mtumishi nyumbani ni mfanyakazi, ukiwa na Hakimu ni mfanyakazi, pamoja na watu wengine hata wa viwandani. Sasa watu wengi wamekuwa wakiumia makazini lakini kwa bahati mbaya hawapati mafao yao vizuri.

Ukienda kwa mfano Hospitali ya Muhimbili *(MOI)*, utakuta kuna wafanyakazi wamelazwa hapo, lakini ukimuuliza ni wapi mafao yake atapata hawezi kujua. Ukienda kwenye hospitali kama Amana, kuna watu wameumia wapo wengi, mwingine alikuwa anasafiri ameumia sasa katika hili niseme kwamba, tukishakuwa na Mfuko mmoja huu ambao utaangalia wafanyakazi wa nchi nzima, tutakuwa tumepiga hatua nzuri sana ya kumkomboa mfanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natofautiana kidogo na Waheshimiwa Wabunge waliozungumza kwamba, ni vizuri fedha hizi au fungu hili likawa kwenye Mifuko ya Jamii. Mimi nasema hapana, kwa sababu Mifuko ya Jamii mingi inakuwa kama

nilivyosema ni kwa ajili ya wanachama wake tu, lakini huu Mfuko wetu tunataka uwe wa wafanyakazi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Kazi na nchi yetu ya Tanzania ambayo ni mwanachama wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO)*, kuna taratibu zake ambazo zimewekwa ambazo na sisi tumeziridhia; mojawapo ni kwamba, Sheria za Kazi Duniani zinaondoa uwezekano wa mfanyakazi kujilipia fidia yake anapoumia akiwa kazini.

Ukiangalia kwenye Mifuko yetu ya Jamii ni kwamba, mfanyakazi anachangia 10% na mwajiri wake naye anachangia 10%. Sasa tukiruhusu kwamba, tuwe na utaratibu huu, maana yake ni kwamba, mfanyakazi atakuwa anachangia gharama zake za kuumia kazini wakati hii ni kazi ya mwajiri wake. Ninasema hivyo kwa sababu ni kazi ya mwajiri kumhakikishia mfanyakazi anafanya kazi katika mazingira ya usalama. Sasa Shirika la Kazi Duniani linapinga utaratibu wa mfanyakazi kuchangia fidia wakati atakapopata ajali.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi na kwa kuwa sisi ni wanachama wa Shirika la Kazi Duniani, ninaungana kabisa na wenzetu ambao wameleta Muswada huu mzuri, ambao utaondoa ukiritimba wa kuwafanya wafanyakazi wetu wachangie hii Mifuko ya Jamii, wapeleke fedha zao wakati kazi hii ni ya mwajiri. Ndiyo maana naendelea kusisitiza kwamba, huu Muswada ni mzuri mno, utaondoa ukiritimba huo.

Mheshimiwa Spika, wakati napitia Muswada huu, kuna jambo moja limenivutia sana; hii ni namna ya kumpata Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Muswada huu imeonyesha kwamba, kutakuwepo na vigezo vingi vya kumpata Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko huu. Kigezo kimojawapo kinakuwa ni uadilifu kwamba, huyu mtu atapimwa kwa uadilifu wake; ana uadilifu kiasi gani tuweze kumpa nafasi ya kushika Mfuko wetu huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, mifuko yetu ya jamii, mara nyingi imekuwa ikienda tofauti na malengo yake; mara nyingi imekuwa haikidhi mahitaji ya wanachama wake, hiyo yote ni kutokana na uadilifu. Sasa katika hili tunakusudia kuwa na Mkurugenzi Mtendaji, ambaye tutampima kwa kigezo cha uadilifu wa hali ya juu sana na siyo yeye peke yake, pamoja na Bodi yake yote kigezo kikubwa kitakuwa ni uadilifu.

Mimi ndiyo maana nilianza kusema kwamba, Muswada huu ni mzuri mno kwa sababu tukishaanza kuingia kwenye uadilifu wa Bodi na *Management,* mimi nina imani kubwa sana Mfuko huu utafanya kazi nzuri na Watanzania wote tutafaidika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia lingine ambalo limenifurahisha ni kwamba, Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Bodi, watakuwa wanawajibika kwa Serikali. Vilevile kutakuwepo na *Regulatory Authority* ya kuwa inawaangalia katika kufanya kazi zao. Kwa hiyo, kwangu mimi wasiwasi wa kwamba labda fedha hizi zitatumika vibaya mimi naona haupo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limenivutia sana, nilikuwa nasoma kifungu cha 17 cha Muswada huu tunaoupendekeza kuja kuwa Sheria, kifungu hiki ukiangalia kwa makini kinaupa uwezo Mfuko huu utakaoundwa wa kutoa ruzuku kwa taasisi nyingine ambazo zinajihusisha na shughuli za kusaidia kuimarisha usalama wa wafanyakazi na afya zao kazini. Kipengele hiki ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ruzuku kwa mfano, ikitolewa kwa chombo kama *OSHA* ili iwasaidia wale kwa sababu wanajihusisha na usalama kazini na afya za wafanyakazi, itasaidia kuzuia kuliko kutibu. Sisi hatutaki wafanyakazi wapate ajali sasa kama, tuna Mfuko ambao utasaidia wafanyakazi wasipate ajali wakae salama na afya zao salama, basi hii ruzuku itakuwa imeelekezwa mahali pazuri na pa usalama.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama nilivyosema, leo sikuwa na mengi sana, wengi wamechangia sitaki kurudia na Kanuni zinakataza. Nazidi kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Athuman Kapuya na timu yake yote na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Blandes na ninakutakia safari njema huko Karagwe.

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, wakati huo huo Mheshimiwa Pindi Chana ajiandae.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unasema kwamba ni *Workers Compensation Act*, sasa kwa Kiswahili tunaweza kutafsiri tukasema ni Fidia kwa Wafanyakazi. Sasa ukilinganisha maudhui ya Muswada huu na ukichukua ile Sheria ambayo tunataka kuifuta, yaani sura ya 263, utaona kuna tofauti kubwa sana kwa sababu inaelezea kwanza wafanyakazi ni nani na pia ilikuwa inaelezea ikiwa mfanyakazi ataumia sehemu moja ya kiwiliwili chake, basi fidia yake itakuwa namna kadha na kadha. Kwa hiyo, kulikuwa kuna kipimo ambacho kilikuwa kimeshawekwa.

Bahati mbaya katika Muswada huu hakuna kipimo, mfanyakazi atakapoumia basi kipimo hicho kimewekewa watu wengine kabisa, hili ni suala ambalo si barabara sana.

Mheshimiwa Spika, nitaelezea baadaye ni watu gani ambao wamewekewa vipimo hivyo na nini matatizo yake.

Mheshimiwa Spika, lakini tukija katika Muswada huu kwanza, tuje katika kifungu cha 6, ambacho kinaanzisha uteuzi wa *Director General.* Hili ni suala zuri, lakini pia hapa pana upungufu kidogo kwa sababu ikiwa kutakuwa na *Director General*, mimi nafikiri ni vyema tukawa na msaidizi wake, kwa sababu huyu ni binadamu na wakati mwingine binadamu anaweza akapatwa na matatizo. Katika Muswada wote huu, hakuna

msaidizi wa *Director General*.  Sasa mimi nilikuwa nafikiria kwamba ni vyema kukawa na Msaidizi wa *Director General,* ambaye anaweza akafanya shughuli zile wakati wowote ule ambapo *Director General* atakuwa hayupo.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kifungu cha 16, nahisi kina matatizo hivyo hivyo kwa sababu pale amezungumzia *adequate and equitable compensation*. Kwa mtazamo wangu, inaposema kwamba ni *adequate and equitable compensation* hii ni *subjective test*; nani anayeweza kusema kwamba hii ni *adequate* na hii ni *equitable*?  Sasa wazo langu ni kwamba, hapa tunge-*define* vizuri zaidi ili tatizo hili lisije likawapata wafanyakazi wetu wakati wa kulipwa mafao yao.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 pia kina matatizo, kwa sababu ukisoma katika Ibara ya (2) wanasema kwamba, mfanyakazi ambaye ametenda kosa lile au amefanya kitu kwa bahati kitu kile kikawa ni *willful misconduct*, basi yeye hatolipwa.  Lakini kuna *exception* wanasema mfanyakazi huyu atalipwa ikiwa ile ajali ime-*result in permanent total disablement* au *the employee dies as a result of the accident.*

Sasa nilikuwa najiuliza; ikiwa huyu mtu amekwenda katika *frolic of his own* na halafu akapata ajali na sisi tukamlipa; je haitafungua mlango kwa mfanyakazi yeyote ambaye ametumwa na tajiri wake lakini akaona kwamba bado anayo *time* na akafanya shughuli nyingine ambazo zinaweza zikaleta hasara na baadaye ikabidi alipwe kwa mujibu wa kifungu hiki?  Sasa nafikiri ikiwa mfanyakazi amekwenda *out of his own* bila kuchukua maagizo ya mwajiri wake, basi ni vyema tukakitazama kifungu hiki kwamba yeye hafai kulipwa mafao haya.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 31 hapa wanazungumzia suala la ku-*recover compensation*, ambapo *Director General* anaweza akapeleka kesi Mahakamani, ikiwa ataona kwamba kesi ile ina uzito fulani wa kupata yale mafao ambayo yameshalipwa kwa mfanyakazi yule. Sasa wasiwasi wangu ni mmoja tu kwamba, Mahakama mara nyingi wanazungumzia masuala ya kisheria, lakini wakati mwingine wanazungumzia masuala ya *technicalities*.  Sasa ikiwa masuala ya *technicalities* yamezungumzwa hapa na kesi ile ikatupwa nje ya Mahakama; je, fedha hizi zitapatikana kwa njia gani?

Mheshimiwa Spika, wazo langu ni kwamba, suala kama hili ni bora tukafungua *Health Insurance System*, zitakazo-*guarantee* zile fedha ambazo watalipwa wafanyakazi na *Insurance* wanaweza wakalipa fedha hizi bila kupitia Mahakamani.  Sasa kifungu hiki cha 31 ni sambamba na kifungu cha 62(1) na 62(2), kwa sababu ukisoma kifungu cha 62(1) na 62(2) hapa pia kuna matatizo.  Imeelezwa hapa kwamba, kutakuwa na suala la *reasonable cost* kabla huyu mtu hajalipwa; je, ni nani ambaye ana-*determine reasonable cost;* na ni kitu gani ambacho kita-*determine reasonable cost*?

Mheshimiwa Spika, pia hii nahisi ni *subjective test*, ambayo isingefaa kuwepo katika Sheria, vinginevyo hii itaruhusu mlango mkubwa sana wa huyu *Director General* au mtu mwingine, kuweza kutoa fidia ambazo yeye mwenyewe atahisi.  Kwa mfano, anaweza akaenda mtu ambaye ni jamaa yake au ana uhusiano naye, *reasonable cost* zile

ambazo ataziweka hapa kutokana na sura ya mtu aliyekwenda, zinaweza zikawa ni tofauti na *reasonable cost* alizozifikiria kwa mtu mwingine ambaye hajulikani. Kwa hiyo, suala hili nahisi lina tatizo na hili suala la kuweka *subjective test* katika kila kifungu cha sheria, mimi nahisi ni kibaya; ni vyema tukaweka *test* ambazo zinakuwa *generalised* kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 48 hasa ukitazama *schedule* ya pili ya kifungu hicho; *Director General* amepewa uamuzi wa kukisia ni *percentage* gani ya maumivu ikiwa haikuwekwa katika Sheria. Ukiisoma sheria hiyo, utaona kwamba, kuna baadhi ya maumivu ambayo yamewekewa *percentage* zake, lakini anasema kwa mujibu wa *schedule* namba 2, kifungu cha 48, pale ambapo maumivu hayapo katika sheria hii, *Director General* anaweza tu akakisia *percentage* ya maumivu yale. Mimi nahisi hili pia ni tatizo, kwa sababu *Director General* hana msingi wa mambo ya afya, hata ukitazama katika kifungu cha 10, *Director General* ameanzisha *Advisory Board* yake lakini haikuzungumza ni watu wa aina gani ambao wanaweza wakateuliwa, yaani ni watu wa afya, madaktari au ni nani.

Sasa mimi nahisi kwamba, utaratibu huu si mzuri na ni vyema *Director General* akaondolewa dhamana hii na akapewa Daktari ambaye anahusika. Kama maumivu yale hayakuwekwa katika sheria, basi Daktari ambaye anahusika aweze kusema maumivu yale ni *percentage* gani ya maumivu na namna gani anaweza akapewa fidia yake.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 83 nacho nahisi kina matatizo, kwa sababu hapa kunaanzishwa *investments* nyingine katika Mfuko huu. Mimi nahisi tukianzisha *investments* katika shughuli hizi, tunaweza tukawapa matatizo wale watu ambao wanahusika na Mfuko huu. Matatizo yenyewe ni kwamba, tukiweka fedha nyingi katika *investments*, inaweza ikatokea matatizo ambapo wafanyakazi wengi wameumia na ikawa fedha zote zimeshakwenda katika *investments*. Tatizo kubwa tunaloliona siku hizi, kwa mfano *National Insurance Corporation (NIC)*, imeanzisha *investments* nyingi ambazo sasa zinatoa matatizo kwa wale watu ambao wanadai fidia zao. Kwa hiyo, hili nafikiri ni jambo lingine la kutazamwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 94 nacho nahisi kina matatizo, kwa sababu Waziri amepewa jukumu la kukadiria malipo hayo. Mimi nafikiri hili ni kosa, tusimruhusu Waziri kukadiria makadirio ambayo mfanyakazi anapaswa kupewa. Mimi nafikiri utaratibu wa zamani ambao umewekwa katika sheria, kwa mfano, mtu atakikatika mkono, tunajua kwamba mshahara wake unazidishwa kwa miezi fulani halafu unagawanywa kwa namba Fulani, hiyo ndiyo *compensation* yake. Mimi nafikiri utaratibu ule ni mzuri, kwa sababu mtu atajua kwamba, anapopata matatizo haya utaratibu wa kulipwa utakuwa namna hii.

Kwa hiyo, ukitazama vifungu hivi na vingine vingi, kuna matatizo kidogo ya kuifanya Sheria hii iwe sivyo ambavyo mfanyakazi angelipenda iwe. Kwa maana hiyo, sheria hii ingawa lengo lake ni zuri, lakini nafikiri bado kuna vifungu vingine ambavyo vingepaswa kurekebishwa ili iweze kukidhi haja ile ambayo mfanyakazi anatakiwa hasa aipate.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, wajaribu kutazama vile vifungu ambavyo ni muhimu kama hivyo nilivyovitaja na vinginevyo ili viweze kuboreshwa na vitakapoboreshwa. Naamini kwamba, Sheria hii inaweza ikasaidia wafanyakazi wetu pale ambapo wanapata matatizo au pale ambapo wanapata ajali na kuumia katika mwili wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, ahsante sana kwa uchambuzi wako mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Pindi Chana, atafuatiwa na msemaji wa mwisho kwa leo Mheshimiwa John Momose Cheyo.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu unaohusu kuwafidia wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni ya wakulima na wafanyakazi, mara nyingi tumekuwa tukizungumzia habari za wakulima na vivyo hivyo sehemu kubwa ya wananchi wetu ni wafanyakazi na wachache sana ni wafanyabiashara. Hivyo, Muswada huu ni muhimu sana katika nchi yetu kwani utasaidia sana kuboresha shughuli mbalimbali.

Nina ushauri kidogo kwa Wizara na Serikali kama ifuatavyo:-

Ningeshauri chombo hiki, yaani ule Mfuko kama jinsi ambavyo Muswada umeeleza kwamba upo chini ya Wizara lakini kwa kiasi fulani unaojitegemea au kwa lugha nyingine wanasema, *Government Agency*. Kwa hiyo, wanawajibika chini ya Wizara Fulani, lakini ni Mfuko ambao unajitegemea *(Government Agency)*.

*Government Agency* hiyo iwe na utaratibu wa *decentralisation* katika *system* yake ili kuwezesha hata watu wa Mikoa mbalimbali kama Mikoa ya Iringa na Wilaya mbalimbali kama Wilaya ya Ludewa, waweze ku-*access* huduma hiyo kwa urahisi zaidi, isiwe *centralised Head Office* Dar es Salaam na kila kitu Dar es Salaam kwa sababu bado katika nchi yetu masuala ya miundombinu ya barabara na mawasiliano kama ya *internet* yanakwenda polepole. Kwa hiyo, tuki-*decentralise* kwa Mamlaka atakayokuwa nayo huyu *Director,* itasaidia zaidi ili hata shughuli mbalimbali zitakapokuwa zinafanyika, basi watu waweze kupata huduma hiyo kwa urahisi zaidi.

Ninapenda kuanza kwa maswali mawili madogo ambayo ningeomba Wizara itafakari. Nilikuwa ninajiuliza, tunaposema *Workmen Compensation Act* ni kwa ajili ya wafanyakazi; wapo wafanyakazi ambao ni waaajiriwa, wapo wafanyakazi ambao wamejiari wenyewe, yaani *Self Employed*, sasa kwa hawa ambao wamejiajiri wenyewe; je, Mfuko huu unaweza ukawazingatia? Unaweza ukaweza vigezo ambavyo wale waliojiajiri wenyewe kama mtu ana *workshop* yake, anafanya kazi mwenyewe, iwe ni *Engineer* ameumia maana yake ni kazi; sasa huyu mtu aliyejiajiri mwenyewe Mfuko huu unaweza ukazingatia? Si hilo tu, lazima tuseme ni waajiriwa na waajiri wa aina gani.

Kwa mfano, kuna watu wengine wanafanya kazi viwandani, labda kuanzia watano na kuendelea na kuna wengine wanafanya kazi chini ya wastani, yaani wengine wawili na wwengine watatu; je, huu Mfuko utazingatia mwajiri na mwajiriwa katika makundi hayo?

Tunazo pia taasisi mbalimbali ambazo watu wake wanafanya kazi, sijajua huu Mfuko kama umeweza kuwazingatia. Taasisi hizi ni pamoja na Bunge la Jamhuri ya Muungano, Wabunge ni wafanyakazi wa wananchi ambao wamewapa ridhaa kuwawakilisha. Utakuta Mbunge anafanya kazi, anafanya ziara na kadhalika, katika huduma hizo za kufanya kazi za kuwawakilisha wananchi amepoteza kiungo chake, kwa mfano, mkono, mguu au ameumia akiwa kazini, sasa huu Mfuko unaweza ukalizingatia hilo maana yake kadiri siku zinavyokwenda mambo yanaboreshwa? Nilidhani hayo ni mambo ambayo tungeweza kuyazingatia.

Ushauri wangu mwingine ni masuala ya uharaka wa kushughulikia utaratibu huu wa fidia, azma ni nzuri sana na malengo yake ni mazuri sana; ni kumrudisha mtu ambaye alikuwa mzima na sasa amepata ajali katika sehemu yake aliyokuwepo kabla ya ajali. Ndiyo lengo la mfuko, tunaposema *compensation* angalau yule mtu aonekane kama yupo katika sehemu yake ya mwanzo kabla hajapata ajali.

Sasa wakati mwingine shughuli hizi huwa zinachukua muda mrefu sana, maana lazima aende mtu anayeitwa *assessor* akakague hiyo ajali imetokeaje, sababu ni nini na kadhalika. Sasa ndio maana nimesema Mfuko uwe chini ya Wizara, lakini ujitegemee ili waweze kuajiri wataalamu, waweze kupata *consultation* kutoka kwenye *insurance company* na maeneo mengine ili waweze kufanya kazi zao kwa haraka na kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu wakati mwingine ajali ikitokea, unahitaji sana kuweza kusema kwamba, hiyo ajali ipo katika maeneo ambapo fidia inazingatiwa ama haipo? Kwa mfano, mtu yupo kazini imetokea ajali ambayo sababu yake sio yeye mfanyakazi na wala sio mwajiriwa, ni kwamba hiyo huduma alipokuwa anaifanya kulikuwepo na mtu wa tatu *(Third party)*, anayefanya ile kazi, labda anaweka ujenzi Fulani, ikatokea huyu mwajiriwa amepata ajali labda mtu anajenga jiwe likamdondokea akaumia, sasa mwajiriwa hajasababisha na mwajiri hajasababisha ni *third party* aliyesababisha. Mambo kama haya ni muhimu sana yakazingatiwa.

Ombi langu kwa Wizara, ajali ikitokea kazini bila ya kujali nani amesababisha, ninaomba wafanyakazi hawa wazingatie kulipwa. Naomba niseme vizuri kwa Lugha ya Kiingereza kwa idhini yako Mheshimiwa Spika, tuseme: "*Fault is not an issue;* nani amesababisha *fault* hiyo *is not an issue so long as* ameumia huyu mtu." Tafadhali sana tuzingatie, maana yake ndiyo lengo la kumpa fidia.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu umeeleza kwamba, endapo sababu ya ajali hiyo itakuwa ni yule mtu wa tatu sio mwajiriwa au mwajiri, basi huu Mfuko utakwenda Mahakamani kumshtaki yule mtu wa tatu aliyepelekea ajali ile kutokea. Wasiwasi wangu ni kwamba, atakapokuwa amekwenda Mahakamani na ameshindwa,

haki ya huyu aliyeumia inakuwaje? Maana huwezi kusema tumekwenda Mahakamani kumshtaki yule ndugu na ameshinda kesi hivyo hustahili kulipwa. Kwa hiyo, naomba sana mwajiriwa ilimradi ajali imetokea katika eneo lake la kazi na wakati wa saa za kazi, basi aweze kupata haki yake maana fidia ni haki na ni haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile wakati mwingine inaweza ikatokea wakasema ni kweli ajali imetokea lakini inatokana na uzembe wake yeye binafsi, hasa ukiangalia upande wa pili wa shilingi hata kama ni uzembe wa yule mwajiri, alipaswa kuwa makini kuhakikisha ubora wa mazingira ili ajali ile isitokee. Kwa hiyo, wasije wakasema kwamba ni uzembe wake, kwa lugha ya Kiingereza wanasema *misconduct*. Naomba sana suala la *fault* katika eneo la kazi, isiwe sababu ya huyu anayefanya kazi kutopewa haki yake.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo ningependa kuyazungumzia ni vifungu vifuatavyo, ambavyo vimeelezea juu ya makosa ambayo yanatambulika kwa mujibu wa Muswada huu. Kwa mfano, vifungu vya 32(2), 34(3), 35(3), 36(3) na kifungu cha 45, vifungu hivi vimetajwa kwamba yapo makosa katika Muswada huu endapo jambo moja, mbili, tatu likifanyika; lakini adhabu yake ni nini vifungu hivi havijaeleza. Ukienda kifungu cha 46(5) kinaeleza kwamba, kufanya hivi ni kosa na kwa kuwa ni kosa basi adhabu yake itakuwa ni jambo Fulani.

Ningependa tu kujua kwamba, mtu akipata ajali anatakiwa kutoa taarifa ndani ya muda gani? Sheria imeeleza wazi kwamba, anatakiwa kupeleka madai yake katika Mfuko au moja kwa moja au kupitia kwa mwajiri wake ndani ya miezi 12, yaani wanasema *limitation of time* ni miezi 12. Sasa kulikuwepo na suala la taarifa, kabla ya kupeleka madai unaweza ukapeleka taarifa. Muda wa kupeleka taarifa bado haujazungumziwa katika sheria, nadhani wakati mwingine inakuwa ni muhimu maana inaweza ikatokea mtu akaumia leo akapeleka taarifa baada ya miaka miwili; sasa sijui huyu tutamzingatia au vipi?

Mheshimiwa Spika, hakika kwa mara nyingine naunga mkono Muswada huu; ni mzuri, una maana sana kwa maendeleo ya nchi yetu na maboresho na naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Pindi Chana, kwa uchambuzi huo. Mzungumzaji wa mwisho ni Mheshimiwa John Momose Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, naomba ruhusa yako ya kuzungumza maneno mawili hivi ya utangulizi. La kwanza kabisa ni juu ya Bunge. Nashukuru kwamba, ulinipa nafasi ya kwenda Uingereza kwenye Kongamano ambalo lilikuwa linahusu *Enhancement or Effectiveness of Parliament,* yaani kuimarisha Bunge.

Nataka kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, baadhi ya watoa mada, walilitolea mfano Bunge la Tanzania kama Bunge ambalo linajitahidi sana katika kujiimarisha na

wakataja kuna *driver and drivers*. Natumaini walivyokuwa wanasema *driver* walikuwa wana-*refer* kwa Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo, tuendelee na mipango yote ambayo inaweza kuliimarisha Bunge letu na Wabunge ambao tuliokutana nao, wanategemea sana Mkutano wako wa *CPA* ambao utakuwa Arusha, kwa hiyo, jitayarishe vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, kwa kuwa mimi ni Mbunge ambaye natoka Kanda ya Ziwa, nataka kutumia nafasi hii kuiomba Serikali iangalie utaratibu wa mbegu za pamba kwa hivi sasa. Tumeuza pamba kwa shilingi 500 kwa kilo, leo tunauziwa mbegu kwa shilingi 500 kwa kilo, sasa ni afadhali labda tungezichambua zile mbegu sisi wenyewe tukazibakiza badala ya kuuza pamba. Hali hii haihamasishi wakulima kulima pamba. Kwa hiyo, naomba Serikali ichangamkie hili kwa sababu jambo la wakulima wa pamba ni la maana sana hasa wakati huu wa kupata fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, nimesoma huu Muswada, nafikiri una matatizo na tatizo hili wengi wamelizungumza hapa lakini mimi naona hata namna ya kupata fedha ya kuweza kutoa *compensation* au fidia kwa wale ambao watakaohusika wafanyakazi ni matatizo. Mfuko wenyewe unamtegemea mtu anayeitwa Mkurugenzi Mkuu au *Director General,* afanye tathmini ya mtu anayeajiri *(an assessment of the employer)*. Sheria haisemi kabisa ni kiwango gani mtu ambaye anaajiri anapaswa kutoa kwa ajili ya Mfuko huu na kama ni mambo ya kuomba, mimi nakukadiria kiasi hiki ndio kusema kwamba mwanzoni kabisa panakuwa na utata. Maana ukinikadiria fedha zilizo nyingi zaidi nitakataa na sio kukataa tu, tatizo ambalo ninaliona kubwa zaidi, huu Muswada unaashiria watu wengi kutafuta njia ya kuidanganya Serikali. Kwa sababu ukiusoma huu Muswada, pamoja na *section* 75 ambayo inazungumzia juu ya makadirio, kuna faini pale usipolipa yale makadirio ya shilingi milioni 50; tunazungumzia watu gani nchi hii. Labda kama Muswada ungelikuwa umeweka tabaka mbalimbali za waajiri kwamba, waajiri ambao *turnover* yao au fedha ambazo wanazipata kwa mwezi ni bilioni kadhaa au labda bilioni 50 ndio wanaweza wakawa watu ambao wanapaswa kukamatwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, lakini kama wewe unazungumzia juu ya mtu ambaye anauza nyama kwenye duka la nyama na ana wafanyakazi halafu unamwambia asipolipa makadirio wewe unaweza ukamtoza faini mpaka shilingi milioni 50; unazungumzia kitu gani? Wote tutaishia jela la sivyo watu wote hawatatoa habari kwenye Mfuko huu.

Nimeona hata kwenye sehemu ya huyu bwana ambaye anaitwa Mkurugenzi Mkuu kutoka *section* ya 7; nashangaa huyu ni mtu wa namna gani ambaye ana mamlaka ya kila kitu. Yeye ni Polisi, anaweza kuamua mtu kuingia ndani ya Ofisi ya aina yoyote kuchukua *document* na hana mtu anayeweza kumzuia yeye mwenyewe, ndio anaamua nani alipwe nani asilipwe halafu baadhi ya maneno ambayo yanayotumika hapa ni maneno ya jumuiya tu *in English "wholly financially dependant."*

Sasa kwanza hapo kama mnasema anayemtegemea kikamilifu, mtu ambaye aliyefariki, mkianza kuzungumza hayo *only financially dependent,* tayari pale pale nawajua Wanasheria wanavyojua, wataanza hapo hapo ni nani kweli ambaye ni

mtegemezi wa yule mtu ambaye ameathirika.  Sasa nashangaa ni nani atakayeweza kutumia huduma inayotolewa na Muswada huu?  Watu ambao tunawazungumzia ni wafanyakazi wanyonge, ambao wana mshahara mdogo, hawana uwezo hata wa kutafuta Mawakili, lakini kutoka mwanzoni kabisa ni mashauri ya mtu mmoja tu; *Director General.*  *Director General* ndiye ana mamlaka ya kila kitu.  Afadhali ningefikiria kwamba, aidha kwa upande wa makadirio ya fedha ambayo yanalipwa na wafanyabiashara na waajiri, pangelikuwa na Bodi wakati ambapo mtu anapeleka kwamba anataka kulipwa kiasi hiki, Bodi inayomfikiria mtu mmoja na anatuma watu wengine, yeye ana mamlaka yote hayo.

Mimi nimeshangaa kwamba, hata masomo ya demokrasia katika nchi hii sijui yamepitia wapi au katika Wizara hii; labda hawana somo hilo, maana hakuna kabisa mahali popote ambapo inazungumziwa kuna uwakilishi wa aina yoyote; mtu aliyeathirika; au mtu ambaye anaombwa alipe fedha.

Kwa hiyo, naona Muswada huu utakaa kwenye vitabu, Bunge lako lilivyo ni vigumu sana kukataa Muswada na leo kama ningekuwa mmoja wa watu ambao ningeweza kushawishi, ningesema huu ni Muswada ambao ungepaswa kurudishwa ili wakaufikirie zaidi katika maeneo mbalimbali.  Kwa mfano, *section 71 - keeping register,* yaani kuweka tu kumbukumbu; mimi ni Mwenyekiti wa *Public Accounts Committee, employer* hapa aliyezungumzwa au mwajiri mkubwa hapa ni Serikali, ukiangalia tu kumbukumbu za Serikali haziridhishi hata kidogo.  Sasa unaposema usipofanya hivyo wewe utapata faini ya shilingi milioni 50, sijui ni ujumla au vipi, Serikali ndiyo itakuwa inalipa shilingi milioni 50 na *Principal Secretaries* wasipofanya hivyo waende jela au namna gani, Muswada huu haupo bayana.

Kama tunazungumzia wafanyabiashara, mimi nakwambia kwamba, wafanyabiashara ndio mahali pa kujificha hapa.  Sasa hii tena inapingana na dhana nzima ya watu kutengeneza biashara ndogo ndogo ili waweze kuajiri watu inapingana na dhana nzima ya kuongeza ajira, utaongeza ajira bila ya biashara?  Kama unataka kufanya biashara, tayari hapa usipopeleka *register* tu, usipoweka zile kumbukumbu unamlipa nani na vitu kama hivyo.  Jamani hizi fedha ninyi mnazifikiria au ni ufisadi; zinachukuliwa mahali shilingi milioni 20, 50 kila kitu milioni, milioni tu; hivi faini za shilingi 50,000 zimepotelea wapi?  Katika vitabu vya sheria faini za shilingi mia ngapi zimepotea halafu utakwenda jela miaka mitano.  Kwa hiyo, naona watu aidha wataamua kudanganya, watalipa rushwa au hawatafanya biashara, sasa tunatengeneza kitu gani?

Kwa hiyo, kwa maoni yangu, Muswada huu kama utapita basi ni vizuri Mheshimiwa Waziri aangalie zaidi hiyo *section* 71 kupunguza kabisa hizo faini.  *Section* 77 kupunguza hiyo faini ya shilingi milioni 20, *section* 75 kupunguza kabisa faini ya shilingi milioni 50 na hiyo *section 7* iangalie namna ya kupunguza madaraka ambayo amempa huyu bwana mkubwa anayeitwa *Director General,* bila kufanya hivyo, huu Muswada hautusaidii.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, walioomba kuchangia katika Muswada huu sasa wamekamilika na ni zamu ya mtoa hoja. Nadhani atatanguliwa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Bahati mbaya nina wageni, ambao ni lazima nionane nao saa sita kamili; kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Jenista, Mwenyekiti, aweze kuja ili amalizie ngwe iliyobaki na hatimaye kuendelea kwenye Azimio la Mbuga ya Manyara hapo jioni. Ahsante.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. VUAI ABDALLA KAHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina pingamizi na Muswada huu uliowasilishwa Bungeni ulioeleza vipengele vingi na vizuri. Naipongeza Wizara kwa usimamizi wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ukipitishwa, naiomba serikali chini ya Waziri wa Wizara, usimamiwe vyema na utekelezwe vizuri ili haki itendeke kuepuka madai makubwa ya fidia ya vijana na wazee, haki za kazi zinazotokana na ajira kwa wananchi wa Tanzania ya leo, hasa awamu hii ya nne. Naomba ushirikiano mwema Muswada upite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Magogoni na wapiga kura naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JUMA H. KILIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Athumani Kapuya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara.

Muswada ni mzuri, kwani unatoa fursa kwa wafanyakazi kuwa na uhakika wa kufanya kazi hasa kwa kazi zile za hatari kwa imani kwamba, pale inapotokea hitilafu na kusababisha uharibifu wa mwili basi sheria itatoa unafuu wa kifuta machozi (kwa maana ya fidia), kwa mwathirika, pamoja na ubora wa Muswada. Nina mchango ufuatao:-

Katika kutoa fidia kwa mwathirika, lazima sheria izingatie ni athari ya aina gani iliyomwathiri mhusika; hivyo madhara lazima yatofautishe mfano; Madhara ya kudhuru mwili kwa kuangukiwa au kukatwa kisha kupoteza kiungo; madhara yatokanayo na sumu *(chemicals);* na madhara yatokanayo na mionzi hatari yenye kuleta ulemavu wa kudumu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria izingatie juu ya waajiri binafsi wasiozingatia sheria itakayowekwa. Hatua kali zichukuliwe na ikiwezekana kufikishwa mahakamani au kufungiwa shughuli zake ama vyote kwa pamoja, hii itawafanya waajiri kuwa na tahadhari za uhakika za kuwalinda wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ipige marufuku juu ya mionzi *(X-Ray)*, zinazotumika migodini kuchunguza wafanyakazi watokapo kazini kwa dhana ya kudhani wanaiba madini na kadhalika.

Kadhalika, vifaa muhimu vya kutendea kazi hasa zile za harubu lazima viwepo sehemu zote muhimu za viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua mipaka ya matumizi ya sheria hii.

*Sections 2(1) and (2)*, kwa mawazo yangu zimeshindwa ku-*cover* wafanyakazi wa upande wa Tanzania Visiwani, wanaofanya kazi kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sheria imesema; *"This Act shall apply to Mainland Tanzania and those in the public service of the Government of Tanzania in Mainland Tanzania."* Je, wale watumishi wa Muungano ambao ni Wazanzibari na wanaishi Zanzibar; watakuwa chini ya sheria ipi?

Naomba ufafanuzi, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichangie Muswada huu kwa njia ya maandishi.

Kwanza kabisa, napongeza kwa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria hii, lakini suala ambalo ningependa kujua ni juu ya fidia kwa mfanyakazi wa nyumbani (*House girl, house boy* au wafanyakazi wa namna hiyo), ambao wengi sana wameajiriwa kienyeji, yaani si kisheria; je, waumiapo wakiwa kazini inakuwaje? Je, Wizara inazo takwimu za vijana hawa? Je, inatoa elimu kwao au watajuaje haki zao? Pili, je, vibarua mbalimbali wanapata haki hiyo?

Jambo lingine; je, mfanyakazi anayeumia kazini kwa mwaliko wa chombo fulani toka alikoajiriwa; akiumia njiani inakuwaje? Mfano; kijana Hamisi Msengi wa chombo fulani cha habari aliyeumia akiwa kazini kwa mwaliko wa Vodacom na sasa yupo South Africa kwa matibabu, je, atalipwa na nani? Je, endapo atapata kilema cha maisha ataendelea na kazi au itakuwaje? Ahsante.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo, kwa vijana kuuleta Muswada huu.

Naomba tahadhali ya kifungu cha 36(3) kinachosema: *"An employer who fails within a period of twenty one days to comply with the provisions of subsection (20) commits an offence."*

Swali langu; je, kifungu hiki kimezingatia mazingira ya mahali alipo mwajiriwa huyo kiasi tu cha kuonekana anatenda kosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge, nimepata pia mchango wa nyongeza hasa kuhusu maumivu ya ndani kwa ndani kutokana na kazi.

Sasa hivi ni jambo la kawaida, mwajiri hasa *private sector* mfano *NMB*, hivi karibuni kumhamisha mke wa mtu kumpeleka mbali bila hata kuwashirikisha wanandoa hao. Maumivu kama hayo ya kumfikiria mume/mke ni ya saikolojia. Je, hayo nayo yameangaliwa vipi?

**MH. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Mahanga, Katibu Mkuu, Dr. Komba na Wataalam wote wa Wizara kwa hotuba nzuri na mchanganuo mzuri na kuleta sheria kwa wakati.

Kwa kuwa kuna wafanyakazi wengi hawapewi haki kwenye sehemu zao za kazi, Mfuko huu sasa ni mkombozi wa wafanyakazi wa chini. Hivyo, Kanuni au Mfuko usimamie mambo yafutayo ili kusiwe na ubabaishaji wa kuvunja imani kwa wachangiaji kama ifuatavyo:-

- Elimu itolewe kwa wafanyakazi kabla ya kuanza Mfuko huu.
- Kila kiwanda kiwe na chama cha wafanyakazi ambao watawakilisha wenzao watakaopata matatizo au watakaotaka fidia.

- Chama kiangalie haki za wafanyakazi kwenye maeneo husika hasa kwa vitendea kazi, mishahara na aina ya vifaa vinavyopatikana.

- Kwa mfano, Kiwanda cha Nyuzi Tabora tulipotembelea wafanyakazi walilalamika hakuna chama cha wafanyakazi wala vitendea kazi.

- Wafanyakazi kwenye kanuni wapewe kipaumbele kwenye eneo la Afya wapimwe afya zao, mara kwa mara.

- Kiwanda cha Nyuzi Tabora kichunguzwe.

- Fidia isiwekwe sawa kwa yeyote anayeumia, mdai aangaliwe anachodai na kuumia kwake.

- Urasimu uliopo uangaliwe ili kuwaondolea adha wafanyakazi walioumia, hasa wanaofariki kazini na kuacha warithi wao kukata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wanapofika wakabidhiwe kanuni za kuchangia Mfuko, iwe lazima sio hiari yao.

Matibabu yasifanyike kwenye kutofautisha wageni na wenyeji wote wapewe haki sawa. Iwekewe faini au adhabu kwa wale watakaokiuka. Sheria iangalie wafanyakazi waliokaa kazini kwa muda mrefu bila ya kuthibitishwa kazini, kwa kuwa vibarua tu; na wale wasiotoa barua za ajira ya kudumu wachukuliwe hatua ili kuondoa migomo isiyo ya lazima

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Waziri kwa kuleta Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu. Muswada huu utakapokuwa sheria, utakuwa mkombozi mkubwa kwa wafanyakazi. Kwa ujumla, Muswada ni mzuri. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya upungufu wa Sheria ya Fidia ya Mwaka 1949 ni taratibu ndefu za malipo ambazo zinasababisha baadhi ya wadai kukata tamaa. Hata hivyo, katika muswada huu sehemu ya 9(1) – (4) na sehemu 10(1), zinazungumzia uteuaji wa *assessors* na Bodi ya Madaktari *or medical advisory panels.* Vyombo vyote hivyo viwili vitahusika kwa namna moja au nyingine, kupitia madai ya watakaoumia au kufa kazini. Hapa naomba pawe na muda maalum wa kushughulikia madai hayo, vinginevyo ucheleweshaji wa malipo unaweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 20 na 21, zinaeleza mtu atakayepata ajali atakuwa katika mazingira ya kazi ambayo ameajiriwa. Hata hivyo, naomba pia Muswada umtambue mtumishi yeyote atakayepata ajali akiwa njiani kwenda au kurudi kazini, atambuliwe kama vile amepata ajali akiwa katika utekelezaji wa majukumu ya ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa mengine yanatokea kwa sababu tu waajiri hawazingatii usafi wa maeneo ya kazi na wakati mwingine wafanyakazi hupata magonjwa kwa sababu ya mazingira machafu. Naomba kuwe na ukaguzi wa mazingira. Pili, magonjwa mengine hutokana na wafanyakazi kufanya kazi kwenye mazingira ya moto mwingi au joto jingi.

Naomba waajiri watoe vyakula/vinywaji kama vile maziwa ili kuwalinda watu hao. Tatu, sheria itilie maanani suala la upimaji afya kwa wafanyakazi mara kwa mara. Hili likifanyika vizuri, tutapunguza sana magonjwa kwa watumishi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 25(2) inasema; mfanyakazi anaefanya kazi kwa muda nchini Tanzania kwa zaidi ya miezi 12, huyo atachukuliwa kama mfanyakazi wa kawaida wa Tanzania na kwa maana hiyo atastahili malipo ya fidia endapo ataumia kama mfanyakazi mwingine. Hata hivyo, rai yangu ni kwamba, miezi 12 ni mingi sana,

nashauri ipunguzwe hadi miezi sita kwani magonjwa mengi yanaweza kuambukizwa kati ya miezi mitatu hadi sita.

Mwisho, Muswada ni mzuri; muhimu zaidi ni usimamizi na utekelezauji mzuri baada ya kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Spika, nafikiri sasa tunaendelea. Ninaomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri na baada ya hapo, nitamwita Mheshimiwa Waziri ili tuweze kuona tunaumaliziaje Muswada wetu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada ulioko mbele yetu wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenilinda sana na kuniwezesha kuanza kurudi kwenye hali yangu ya kawaida, baada ya kuugua kwa miezi kadhaa. Nawashukuru vilevile Waheshimiwa Wabunge, ambao waliniombea na baadhi yao wakaja kuniona pale nyumbani Segerea. Nawashukuruni sana, naendelea vizuri na afya yangu kama mnavyoweza kuona. Kwa namna ya kipekee, nawashukuru wapiga kura wangu na wana-CCM wa Jimbo la Ukonga, ambao kwa muda wote walikuwa na mimi kwenye maombi; misikitini na makanisani na wakaja nyumbani kuniona. Maombi yao yamesikilizwa na Mwenyezi Mungu na sasa naendelea vizuri. Nawashukuruni sana na tupo pamoja katika kulijenga jimbo letu la Ukonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Charles Mwera, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Tarime. Niseme toka mwanzo kwamba, naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. Katika kuchangia hoja hii, nitagusia baadhi ya hoja, maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Wabunge; hoja chache mtoa hoja au Waziri wangu atakuja kumalizia. Mimi nigusie tu baadhi ya hoja zilizotolewa na maoni nikianzia na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, ambaye mojawapo ya hoja zake na maoni ilikuwa kwamba, sheria ingetambua wale waajiriwa wanaoumia wanapokuwa njiani kwenda au kurudi kazini. Niseme tu kwamba, sheria imelitambua hilo na katika kifungu cha 20, ukisoma pale utaona kwamba, mfanyakazi ambaye anaumia akiwa njiani kwenda ama kurudi kazini, anatambulika kwamba yupo kazini na sheria inamlinda.

Vilevile Mheshimiwa Zambi alizungumzia na kutaka kuwepo na ukaguzi na kuzuia magonjwa yatokanayo na uchafu au mazingira ya maeneo ya kazi kama moto au joto au jengo lenyewe na kwamba waajiri waweze kutoa vyakula kama maziwa. Ushauri wa Mheshimiwa Zambi ni mzuri na umezingatiwa katika Sheria ya *OSHA* ya Mwaka 2003 na haya yote yamezingatiwa. Aidha, Mheshimiwa Zambi, alizungumzia suala la waajiriwa au wafanyakazi wageni wanaokuja kufanya kazi Tanzania kwa muda na

akasema kwamba, hawa katika kifungu namba 25(2) muda ungepunguzwa kutoka miezi 12 iliyoelezwa kwenye sheria ikawa miezi sita. Sasa pendekezo lake ukiliangalia, linakwenda kinyume na matakwa ya Mikataba ya Sheria ya Kazi Duniani, ambayo kwa kiasi kikubwa, tumezingatia sana matakwa ya Mikataba ya *ILO* katika kutunga sheria hii. Kwa hiyo, ukipunguza wale *temporary employees* kutoka nje kwamba iwe miezi sita badala ya 12, tutakuwa tunakwenda kinyume na Mikataba ile ya *ILO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mwingine ulitoka kwa Mheshimiwa Mwanne Mchemba, ametoa ushauri mzuri sana na tumeuzingatia ushauri wote alioutoa. Alizungumzia kwamba, Mfuko usimamiwe vizuri ili kuondoa ubabaishaji; ni kweli na tumezingatia kwamba elimu itolewe kabla ya kuanza kwa sheria. Kwamba, kila kiwanda kiwe na Chama cha Wafanyakazi kitakachotetea haki na kuwasilisha matatizo; hilo tumelizingatia na katika Sheria za Kazi na ile ya Ajira na Mahusiano Kazini hili limezingatiwa. Akazungumzia vilevile kwamba kanuni zizingatie au ziweke kipaumbele kwenye eneo la afya; hili limezingatiwa vilevile kwenye Sheria ya *OSHA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Martha Mlata, naye alikuwa na maoni kadhaa na akazungumzia kwanza fidia kwa wafanyakazi wa majumbani inakuwaje na vibarua mbalimbali wanapataje haki yao. Mimi niseme tu kwamba, kama mwajiri atakuwa amejisajili katika Mfuko, waajiriwa wake wote watastahili fidia pindi watakapoumia na itakuwa kazi ya Bodi kuangalia kwamba, ajira zote hizi zikiwa ni pamoja na baa, zinasajiliwa ili wale waweze kupata haki zao kama wameajiriwa kiutaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mlata, vilevile amezungumzia wafanyakazi wanaoumia njiani; kama ambavyo nimejibu kwa Mheshimiwa Zambi, hawa wamefikiriwa na wamezingatiwa katika kifungu namba 20.

Mheshimiwa Profesa Mtulia, alitoa ushauri mwingi mzuri tu, lakini vilevile alizungumzia suala la kuimarisha afya na usalama katika sehemu za kazi. Ushauri huu umezingatiwa. Ukiangalia kifungu namba 17 cha sheria kinavyopendekeza katika Muswada huu, haya yamezingatiwa na utaona katika sheria hiyo na kifungu hicho ama Bodi itaanzisha vitengo vya aina hiyo au vile vilivyopo kwa mfano, *OSHA* vitatambuliwa na kifungu kinakwenda mbele kwamba, Mfuko huu unaweza kutoa ruzuku kwenye vitengo au taasisi ambazo zimeanzishwa ambayo itasaidia katika kufanikisha sheria hii iweze kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni, naye alitoa ushauri mzuri tu kuhusu suala la *OSHA*. Tuiongezee nguvu *OSHA* iweze kusaidia ajali na magonjwa kazini yapungue. Ushauri huu tumeuzingatia katika kifungu namba 17, lakini vilevile kwenye Sheria ya *OSHA* ya Mwaka 2003, haya mambo yamewekwa vizuri sana na ushauri wao huo unazingatiwa.

Mheshimiwa Mwinchoum, aliendelea kuzungumzia fidia kwa wale wanaoumia kutokana na viumbe wa baharini. Sheria inatambua watu wanaoumia katika mazingira hayo na fidia italipwa, mradi tu mwajiri husika anachangia katika Mfuko. Alikwenda

mbele zaidi, akazungumzia majanga mengine au ajali zinazoweza kutokea. Ukiangalia jedwali la pili, karibu mambo yote mengi yamezingatiwa, lakini chini ya jedwali hilo utaona kwamba, linampa nguvu Mkurugenzi Mkuu kuweza kufikiria ajali nyingine yoyote ambayo haikutajwa.

Sasa Mheshimiwa Mwinchoum aliposema sehemu nyeti hakutaja hasa ni nini; alisema yale ambayo yanamfanya mtu aitwe Mwinchoum. Sasa kama haipo kwenye jedwali hilo lililofanywa aitwe Mwinchoum, basi Mkurugenzi Mkuu kwa kuiangalia pale namba tatu atakuwa na mamlaka ya kuona kuwa hilo halikutajwa na kama halikutajwa atalifikiria katika fidia. Michango yake mingine kuhusu tu mafunzo ya mara kwa mara kwa waajiri na wafanyakazi, tumeizingatia katika sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Salim Abdallah Ali, alizungumzia tafsiri ya neno "*actually*" na "*employer"* kwamba, hazieleweki sawa sawa. Tuseme kwamba, kusudio halisi la sheria na sio hii tu, sheria zote; sio kutoa tafsiri halisi, yaani ile *dictionary meaning* ya maneno husika, kwa sababu hii sheria sio *dictionary;* sasa tunafundisha maana halisi ya Kiingereza. Nia huwa ni kutoa tafsiri kutokana na maneno hayo, kama yalivyotumika kwenye sheria iliyohusika. Sasa ukitaka kujua *actually* ni nini; unaweza ukaenda kwenye *dictionary* ukajua kama unataka kujua maana yake kwa Kiingereza. Ukiangalia vilevile kifungu namba 86(1), kwa kuangalia kazi zake, *actually* utajua kwamba huyu ni *valuer* wa hizi *funds*, ambaye atakuwa anatathmini hizo *funds* kama zina uwezo wa kujiendesha zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Said Amour Arfi, naye alitoa mapendekezo mazuri tu ambayo tumeyazingatia. Moja ni suala la kipindi cha mpito kwa matibabu kwa mfanyakazi aliyeumia. Sasa katika hili, utaona kwamba, kipengele namba 67 kwa makubaliano na *Director General*, anaruhusiwa kutibu mfanyakazi na baadaye akafidiwa na Mfuko kwa mujibu wa kifungu hicho cha 67.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, alizungumzia mambo mengi, ushauri mzuri tu kwanza kuzingatia kinga kuliko kusubiri kutibiwa. Hilo ni kweli na katika vifungu namba 17 na 74, utaona kwamba haya yamezingatiwa vizuri na sisi tunakubaliana kwamba ni vyema kinga kuliko tiba. Kuhusu kufanyika *medical check up* hiyo Sheria ya *OSHA* inaeleza vizuri sana ile ya mwaka 2003, inataka waajiri wawafanyie wafanyakazi wao uchunguzi wa afya mara kwa mara. Elimu kwa wafanyakazi imezingatiwa katika kifungu namba 17 na itatekelezwa na Sheria ya *OSHA* imezingatia.

Amezungumzia uwezo wa *OSHA* kwamba, inapewa fedha kidogo, ingawa tunakubali lakini tukumbuke tu kwamba, *OSHA* nayo inatakiwa ijiendeshe. Kwa hiyo, ile *scheme* ya *retention* imeruhusiwa kwamba yale makusanyo yanayopatikana wanaweza kuyatumia. Kuna fedha za ruzuku vilevile kutoka Serikali Kuu, kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi na matumizi mengine ya kawaida. Ukiangalia sheria hii, kifungu namba 17 kinamhusu *Director General* kutoa ruzuku kwa taasisi kama ya *OSHA* pale itakapoonekana kwamba, uwezo upo, kwa sababu ni taasisi ambayo itasaidia sana sheria hii kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Missanga, alikuwa na wasiwasi vilevile kwamba, katika kuweka viwango vya mwajiri kuchangia, rushwa inaweza kutumika. Suala la rushwa ni mtambuka na ni suala gumu. Tunasema kwamba, uadilifu katika kigezo cha kupata watumishi wa Mfuko huu ni suala la msingi sana na ndiyo maana unakuta mchakato wa kumpata *DG*, kwanza, anateuliwa na Rais, lakini mpaka kuna Kanuni ambazo Waziri atazitumia katika kupendekeza majina matatu ya kupeleka kwa Rais. Kwa hiyo, anategemewa kuwa mtu mwadilifu sana.

Sheria ya *OSHA* Mheshimiwa Halima Mdee imezingatiwa na Sheria ile ya *Labour* na *Employment Relation Act* kama kifungu namba saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja. Mheshimiwa Waziri, atakuja kumalizia mengine. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali, ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa, wakiongozwa na Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii. Kwanza, naishukuru sana Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii kupitia kwako, kwa jinsi ambavyo umekuwa msaada mkubwa katika kuuchambua Muswada huu na mpaka kufika hapa tulipofika; *inputs* zenu zimekuwa ni za hali ya juu sana. Kwa hiyo, nawashukuruni sana mimi na Wizara yangu. *(Makofi)*

Pili, naomba nimshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ambaye alikuwa katika Kamati yetu na alikuwa anatoa michango mizuri na hata alipochangia hapa amechangia mambo ya msingi kabisa, kwa hiyo nampongeza sana. Vilevile naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamepata nafasi ya kuchangia ama kwa maandishi au kwa kuzungumza moja kwa moja. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa John Momose Cheyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza moja kwa moja ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Salum Abdallah Khalfan, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa John Momose Cheyo na Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia, yapo mambo ya msingi ambayo yamejitokeza na michango ya Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Kamati yetu ya

Maendeleo ya Jamii imekuwa ni mizuri sana. Kwa muda tuliopewa, inawezekana mengine tusiweze kuyafikia katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nataka niwahakikishie kwamba, tutakapokaa na Kamati yangu, tunaweza kuzingatia mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Tukianza na hoja ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kuwepo na matumizi ya neno *may* badala ya *shall*. Kama Kamati ilivyoshauri, Wizara inatambua kwamba, kuwepo kwa Kanuni ni hitaji muhimu katika kutekeleza Sheria; hivyo, Wizara haioni kwa nini Waziri mhusika achelewe kutengeneza Kanuni, kwani bila Kanuni Sheria hii haiwezi kutekelezwa. Kwa hiyo, kuna ubishano kati ya *may au shall*. Kwa kuwa Sheria hii haiwezi kuanza bila Kanuni kutengenezwa, iwe na mimi au mwingine atakayekuja, haiwezekani kabisa aache kutengeneza kanuni kwa sababu vinginevyo Muswada huu utakuwa hautekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie kwamba, *shall na may* haitaathiri utekelezaji wa Muswada huu. Tafsiri ya neno *formal hearing* kwenye orodha ya misamiati iliyotumika katika Sheria hii, tumeuzingatia katika *Schedule of Amendment* na tumetoa tafsiri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyombo vya Majeshi visihusishwe; kwa hili tumezingatia ushauri wa Kamati. Mchakato wa kumpata Mkurugenzi Mkuu, ufanywe kwa kushauriana na Bodi. Mchakato wa kumpata Mkurugenzi Mkuu utaainishwa katika Kanuni zitakazoandaliwa kwa kushirikiana na wadau kwa maana ya Bodi hizo na utatu; na kama mnavyofahamu ni kwamba Bodi zetu ni Bodi za tatu. Kwa hiyo, mchakato ni mzito ambao utamfikisha Waziri kufikia majina matatu yatakayopelekwa kwa Mheshimiwa Rais.

Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi, uzingatie uwiano wa asilimia 50 kwa 50 kati ya wanawake na wanaume; ushauri utazingatiwa. Kuongezwa kifungu kidogo kuelezea muundo wa sifa za juu za vigezo vya kuwateua Wajumbe wa Bodi; ushauri umezingatiwa katika *Schedule of Amendment*. Wajumbe toka vyombo huru kama vyuo vikuu kuwepo katika Bodi, ushauri vilevile umezingatiwa. Kwa hiyo, haya ni baadhi ya mambo ambayo Kamati ya Maendeleo ya Jamii imechangia na sisi tumekubali ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango, yapo mambo ambayo unaweza kuyaita ni ya jumla. Moja ni kuhusu Muundo wa Mfuko. Kwa kawaida jukumu la kuamua aina ya Mfuko ni suala la kiutawala, linaloamuliwa na Bodi ya Wadhamini ya Mfuko husika, kulingana na mahitaji. Suala la Muundo si la kisheria na halipaswi kuwemo ndani ya Sheria. Haiwezekani Sheria iainishe kwamba, atakuwepo *Director General* katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata au Kijiji. Haya ni mambo ambayo Bodi itakapokaa, itaangalia ni namna gani ambavyo inaweza ikafanya kazi hizi kwa ufanisi zaidi. Kwa hiyo, tumeiachia Bodi na watazingatia michango ya Waheshimiwa Wabunge, kuona kama kweli chombo hiki kinachoundwa kinakuwa na ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mkurugenzi Mkuu kupewa uwezo mkubwa kiutendaji, ili kuondoa ukiritimba na urasimu unaolalamikiwa katika Sheria ya sasa. Mfuko unaopendekezwa, ufanye kazi kwa utaratibu wa *one stop centre*. Hapa nizungumze kwamba, huyu Mkurugenzi Mkuu anayetajwa hapa si Mkurugenzi Mkuu kama mtu mmoja; ni taasisi hiyo kwa sababu anavitendea kazi vyake vingi ambavyo vitamwezesha kufanya kazi hiyo. Kwa mantiki hiyo, Sheria imetoa madaraka ya kutosha kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko. Aidha, kifungu cha 7(2) kinamtaka Mkurugenzi Mkuu kupata mwongozo au idhini ya Bodi katika kutekekeleza majukumu yake yote. Kwa hiyo, utakuta kwamba yeye kama yeye, ndiyo anaamua moja kwa moja. Hii ni taasisi lakini vilevile hata anapofikia uamuzi kwa kushauriwa na taasisi hiyo, lazima apate kibali cha Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi ifanywe na Mifuko ya Jamii. Hizi ni Sheria mbili tofauti kabisa; Sheria ya Hifadhi ya Jamii na Sheria ya Fidia. Fidia ni haki ya msingi kwa kila raia wa nchi hii. Hifadhi ya Jamii ni kitu ambacho anaamua ajiunge au asijiunge. Hii tunayofanya hapa, tunatekeleza Haki za Binadamu; ni kitu ambacho anaamua. Kwa hiyo, huwezi ukafananisha hivi vitu viwili. Ndiyo maana tunasema ni vyema Mfuko ukaruhusiwa kuanzishwa ili kuweza kutekeleza jukumu hili ambalo ni pana zaidi la kutengeneza haki za binadamu.

Vilevile ukumbe kuwa, wanaohudumiwa na Hifadhi ya Jamii ni wale wanachama tu. Huu Mfuko ambao tunauanzisha sasa utahudumia wafanyakazi wote; walio wanachama na wasio wanachama wa Hifadhi ya Jamii. Vilevile Mfuko huu malipo yake ni endelevu zaidi, kuliko malipo ya Hifadhi za Jamii. Ndiyo maana tunasema huu Mfuko ni tofauti sana na Mfuko wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kumchaya, anasema viwango vya fidia vitamkwe wazi katika Sheria na hili lilimpa shida hata Mheshimiwa Missanga kwamba, inakuwaje tumwachie tu Waziri atamke peke yake, bora lingetamkwa katika Sheria. Kipo kiwango ambacho kimetamkwa cha zile asilimia, lakini zile asilimia ni malipo ya muda ule mtu anapokuwa amepata janga lile. Vilevile kwa sababu gharama za maisha zinabadilika kila siku na thamani ya fedha inabadilika kila siku na ndiyo maana sisi tumeona tusilitamke hapa, vinginevyo tungekuja kukwama kama tulivyokwama na shilingi 83,000 na shilingi 108,000 kwa muda wa miaka 25, kwa sababu ilikuwa katika Sheria.

Ikiwa katika Kanuni kubadilishwa kwake ni rahisi, kwa sababu Waziri kwa kushauriwa na vyombo husika, akiona kwamba maisha yamebadilika, thamani ya fedha imeshuka, inakuwa ni rahisi kubadili kuliko kuweka katika Sheria mpaka tuje tena baada ya muda mrefu sana kuja kubadili sheria hapa. Ndiyo maana tunasema kwamba ni vyema hili likabaki katika kanuni, likamuwezesha Waziri kuwa anabadilisha mara kwa mara kufuatana na hali halisi ya maisha.

Malengo ya Mfuko ni kuwasaidia wanachama sio kuwawezesha. Vitega uchumi ni chanzo muhimu kwa ajili ya kuwezesha Mfuko kuwa endelevu na kutekeleza majukumu ya kuwasaidia wanachama. Kwa sababu Mfuko kama jinsi ilivyokuwa ile

Mifuko mingine, ukiuacha kwa fedha zile za kuchangia tu, jinsi gharama za matibabu zinavyopanda na jinsi gharama za fidia zinavyopanda, unaweza ukafika mahali ukashindwa kujiendesha. Kwa hiyo, ikabidi sasa turudi katika kupunguza kiasi kwamba, wewe bwana unastahili kulipwa shilingi milioni tano, lakini kwa uwezo tulionao tutakulipa shilingi milioni moja. Kwa hiyo, hakuna hiari maana ndizo tulizonazo. Ndiyo maana tumeruhusu masuala ya vitega uchumi ili Mfuko huu uweze kuzalisha, kuhakikisha kwamba, unakwenda sambamba na gharama za maisha, kubadilika kwa pensheni na kubadilika kwa gharama za matibabu.

Je, Mfuko huu utakuwa chini ya chombo cha udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii? Ndiyo Mfuko huu utakuwa chini ya chombo cha udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Wanaoathirika kutokana na kufanya kazi za hatari, malipo yaangaliwe kipekee; hili nalo ni la jumla. Sheria imeweka utaratibu wa kufanya tathmini ya kiwango cha mazingira hatarishi katika sehemu ya kazi. Tathmini hii itatumika kukadiria kiwango cha michango ya mwajiri. Nataka niseme hivi; Sheria hii ukiisoma pamoja na Sheria ya Kazi na Sheria ya *OSHA*, tunachosisitiza sisi kwanza kabisa ni kinga, matibabu yaje baadae. Kama mtu atazingatia kinga, mazingira hatarishi haya inakuwa ni rahisi sana mtu kukaa pale ukafanya kazi bila kuathirika.

Nitakupa mfano, mimi nimefanya kazi katika *International Atomic Energy Agency* kwa muda wa mwaka mzima. Kule kuna miozi hatari, lakini kwa sababu tulikuwa tunazingatia kinga zile, nimekaa mwaka mzima sikuathirika.

Nimefanya kazi ya utafiti muda wa miaka 25 nikiwa Profesa Chuo Kikuu, *chemicals* nilizokuwa natumia mimi nyingine zinasababisha ugonjwa wa kansa, nyingine zinasababisha kupofuka macho, nyingine zinasababisha kuharibika sehemu mbalimbali za mwili, pamoja na zile alizokuwa anazungumza Mheshimiwa Msomi. Kwa muda wa miaka 25, kwa sababu nilikuwa nazingatia miiko na nilikuwa natumia kinga, mpaka leo naona mimi ni mzima hakuna tatizo. Kwa hiyo, tunachosisitiza hapa Sheria ya *OSHA* ifanye kazi, Sheria ya Kazi ifanye kazi na Sheria hii ifanye kazi ili kuhakikisha yale mazingira yanakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene, anasema Sheria inawalindaje wafanyakazi wanaopata ulemavu wa maisha. Ukisoma zile *schedule* kuna yale malipo ya muda na kuna malipo ya pensheni. Kwa hiyo, wafanyakazi wanaopata ulemavu wa maisha kwa mujibu wa kifungu cha 48(4) na (6), watalipwa pensheni na gharama za matibabu hadi mwisho wa maisha yao. Kila kitu kimezingatiwa sawa sawa. Mfanyakazi anapoumia kwa uzembe wa Sheria imlenge mwajili. Anayelipa si mwajiri, kwa hiyo, huyu mwajiri si kwamba ataonewa hapana, ndiyo maana tunasema tathmini zote zitafanywa na Taasisi ya *Director General* akisaidiwa na *assessors*. Kwa hiyo, suala la kusema mwajiri ataonewa halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambazo zimejitokeza ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya anasema, kifungu cha 36, yule anayechelewa kupeleka taarifa kwa muda wa siku 21 anapigwa faini; je, Sheria imeangalia mazingira?

Tunasema Sheria inayopendekezwa imezangatia kikamilifu mazingira ya mwajiri. Aidha, Sheria hii kama zilivyo Sheria nyingine, haziondoi haki ya mwajiri kujitetea mbele ya vyombo vya Sheria kwa mujibu wa Sheria za nchi. Kwa sababu haiwezekani tu unafika hata kama mbele ya *DG*, umechelewa siku 21 faini yako kadhaa; lazima atamsikiliza, hata kama ni mbele ya Mahakama. Huwezi kufika ukaambiwa kwamba, wewe umeua kwa hiyo tunakunyonga; lazima utajitetea.

Anasema maumivu ya kisaikolojia yanampata mume kama mke anapohamishwa bila ridhaa ya mume wake; hii nayo inaangaliwa vipi? Katika kuleta usawa wa jinsia katika sehemu mbalimbali za kazi, hili limezungumzwa sana, ndiyo maana unaweza ukakuta mwanamke anateuliwa kuwa Balozi, mme wake anaamua mwenyewe amfuate kule aliko au asimfuate. Basi vinginevyo, kama tukizingatia yote hayo mpaka tutafikia ile asilimia 50 kwa 50 tunayoitaka itakuwa kazi. Kwa sababu unaweza ukamshauri mwanaume; mwanaume akasema sitaki mke wangu apande cheo. Inawezekana, kwa mfano, nafasi ya kupanda cheo ipo Singida, mme wake yupo Dar es Salaam, tunamwambia ukawe *Regional Manager may be* wa *NSSF* Singida, mme wake anasema kama ndiyo hivyo, bora abaki hapa hapa na ukalani kuliko kwenda kule kuwa *Regional Manager*. Hii nayo itatupa matatizo. Ndiyo tunasema, kama huyu mwanaume atapata matatizo ya kisaikolojia, sisi tumejiandaa sawa sawa kumpa ushauri nasaha mpaka kuwa *rehabilitated* kwa kutumia gharama za Mfuko.

Muswada usimamiwe vyema kuepukana na madai makubwa ya fidia; hili ndilo ambalo tunajitahidi sana kulizingatia na tunashukuru sana kwa ushauri huu. Kifungu namba (2)(a), hakiwahusishi watumishi wa umma wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria hii inahusu wafanyakazi wote wa Jamhuri ya Muungano awe Bara au Zanzibar wote wanahusika, ila ni kweli haiwahusu watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, kama yupo Posta lakini akawa mwajiri wake ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamuhusu, kama yupo Benki Kuu ya Tanzania yupo Zanzibar inamuhusu.

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Juma Killimbah, kwa kutupongeza. Nasema kwamba, Sheria izingatie madhara na aina ya maumivu. Nimesema ukisoma *schedule* namba mbili na kifungu cha tatu ukurasa wa 59, utaona kabisa kinasema; kama yapo ambayo hayakutajwa katika *schedule* hiyo namba mbili basi *DG* anapewa Mamlaka ya kukadiria. Hoja imezingatiwa katika Sheria inayopendekezwa. Sheria izingatie kuwabana waajiri binafsi; tutazingatia ushauri huo na imezingatiwa. Sheria ipige marufuku matumizi ya *X-Ray* kwa watumishi wa migodini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala dogo kwa sababu hata sisi Wabunge hapa kila siku tunapita kwenye *X- Ray*. Kwa hiyo, kama tunapiga marufuku kwenye migodi na hapa tupige marufuku kwa sababu ni *X–Ray* zile zile. Kinachosemwa hapa ni kwamba, ile dozi iliyowekwa pale ni sahihi? Kama ni dozi ambayo haiathiri, inahakikisha usalama wa mali ya mwenye mali *then* hakuna tatizo. Kama ni *overdose* hilo ndilo suala tutaomba *OSHA* waende wakacheki mara kwa mara, kuhakikisha kwamba watu wetu hawapati mionzi hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zambi anasema, malipo yaharakishwe. Hili nadhani Mheshimiwa Makongoro alishajibu. Fidia izingatie kiwango cha kuumia, hili tumeshaeleza katika *second schedule* kwa hiyo ushauri umezingatiwa akatika Sheria. Urasimu uondolewe; ndiyo hasa kiini cha kuleta Muswada huu hapa, kujaribu kuondoa urasimu na tutakuwa na *one stop centre* kama tulivyesema. Kanuni kuweka faini kwa watakaokiuka; limelalamikiwa sana na Waheshimiwa Wabunge, kwa faini ya milioni 50 na milioni 20. Faini hizi ni kubwa sana, hata mimi naziona lakini ukisoma kama ilivyoandikwa inasema hivi: Faini isiyozidi milioni 50 na faini isiyozidi milioni 20. Huyu Hakimu ambaye ndiye anayetafsiri haki kutokana na Sheria tunazotunga Wabunge, atakuwa ni Hakimu wa ajabu; anamwona muuza mgahawa ana wafanyakazi wawili, kacheleweshа kumbukumbu au hakuweka kumbukumbu anamwambia wewe nakupiga faini ya shilingi milioni 20; hata akijiuza yeye mwenyewe hafiki milioni 20! Kwa hiyo, haiwezekani.

Tunategemea hawa Mahakimu wanaotafsiri Sheria katika haki ni watu waadilifu, watatenda haki. Tumeweka hizi kama vile ni kizuizi tu. Vilevile kuna baadhi ya Wabunge walikuwa wanasema chukueni hatua kali; tumeweka hatua kali hapa, tayari mmeanza kusema kwamba zimezidi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, Mahakimu wetu ni watu waadilifu na watatenda haki. Fidia kwa wafanyakazi wa majumbani; Mheshimiwa Makongoro amelijibu. Mawasiliano ya Mfuko na Kamisheni ya Kazi; Mfuko unawajibika kwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kisera kama jinsi ambavyo Kamisheni ya kazi inavyohusika katika Wizara yetu kisera. Kwa hiyo, hawa wote ni kama vile watoto wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na kwa hiyo, watakuwa na mahusiano kwa maana ya kusaidiana katika kutenda kazi.

Muda wa kushughulikia kulipa fidia utawekwa katika Kanuni. Kwa sababu unajua ni vyema hii tukaacha *flexibility* kubwa hapa. Ukiweka katika Sheria inakuwa ni ngumu sana kubadili kutokana na mazingira mapya yanayojitokeza. Ukiiweka katika Kanuni inakuwa ni rahisi kwa sababu watu wanaohusika katika kubadili Kanuni wale ni wachache kuliko mtiririko wa kuja kubadili Sheria hapa Bungeni.

Mafunzo ya mara kwa mara kwa waajiri na wafanyakazi; Mheshimiwa Dr. Makongoro amelijibu vizuri. Kwa nini Muswada unajumuisha Majeshi? Kama mlivyokuwa mmependekeza, tumeshawatoa kama hawahusiki tena. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu uangaliwe, kwa sababu Mfuko huu ni nyeti. Mkurugenzi Mkuu, kama mlivyoshauri Kamati ya Maendeleo ya Jamii, tumezingatia kwamba, isiwe tu Waziri anaamua yeye mwenyewe kujifungia katika Ofisi na kuteua. Apate ushauri wa wadau na hata sifa za Mkurugenzi Mkuu, mlizoziainisha tumezikubali kwamba uadilifu ni mojawapo ya kitu cha kuzingatiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Bodi wawekewe vigezo. Hilo nalo tumelizingatia. Tafsiri ya neno *actually* pamoja na lile ambalo alilizungumzia Mheshimiwa Salim Abdallah Ali, ksudio halisi la Sheria si kutoa tafsiri halisi ya maneno

husika ila ni kutoa tafsri ya maneno hayo yalivyotumika katika Sheria husika. Muda wa ukomo wa Mkurugenzi na Waziri kutoa maamuzi ya migogoro inayoletwa mbele yao. Rufaa na migogoro inayowasilishwa kwa Mkurugenzi au kwa Waziri inatofautiana kimazingira na hata uzito; hivyo hata ukomo wa muda unatofautiana kimazingira na hata uzito. Hivyo, hata ukomo wa muda unatofautiana; itakuwa vigumu kuweka ukomo wa kushughulikia migogoro. Kwa sababu unaweza kwenda kupeleleza masuala kwa mfano migodini, ambayo yana utaalam wake wa hali ya juu na kuna vitu ambavyo kama kuna *chemicals* zimemwagika kuna namna ya kuzi-*tress* zile *chemicals* na kusema wiki moja tunataka majibu. Haiwezekani kwa sababu mambo mengine utakuwa hukuyaangalia sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunasema ni vyema huu muda ukaachwa ili hawa wanaotumwa hiyo kazi waweze kuifanya kwa umakini zaidi. Sehemu nyeti zikiharibika, nadhani nimelieleza vizuri zaidi. Kipindi cha mpito cha matibabu kwa mfanyakazi aliyeumia, Mheshimiwa Naibu Waziri amelijibu. Katika kuweka viwango vya mwajiri kuchangia rushwa, inaweza kusababisha mwajiri asichangie kiasi anachopaswa. Tumesema hivi yeye ataleta taarifa tutamsajili, lakini tutakuwa tunakwenda kucheki, ndiyo maana tunasema kuna mahusiano japokuwa hayakuandikwa; kuna mahusiano kati ya Mfuko huu na Idara ya Kazi. Kwa sababu Idara ya Kazi ndiyo wenye *Labour Inspectors,* watakuwa wanakwenda kukagua na kuangalia kama yale yaliyosemwa ni ya kweli. Tukigundua kama ni uongo, ndipo anapokumbana na faini hizi ambazo ni nzito na vilevile kuzingatia mazingira yake halisi.

Wafanyakazi kunyimwa fedha zao ikiwa ni pamoja na fidia; Sheria inayopendekezwa katika Muswada huu inaweka mfumo mwepesi usiokuwa na usumbufu katika kudai fidia. Makampuni ya nje yatazamwe, hili ni la Mheshimiwa Kumchaya. Makampuni ya ndani na ya nje, yote yanaangaliwa sawa sawa. Wageni hawa wanapofika pale *TIC*, mtu anayewakilisha Wizara ya Kazi yupo anawapa Sheria zetu na kwamba hizi ndiyo Sheria za nchi unapaswa kuzizingatia. Yanayotokea ni ufedhuli tu au ukiukwaji wa Sheria. Tunachoomba tu sisi tupewe taarifa watu wa kushughulika tunao na vyombo vyetu vimeshakamilika, *CMA* ipo, Mahakama ya Kazi ipo kwa ajili ya watu wakorofi kama hao.

Makampuni yanayoajiri wafanyakazi yasajiliwe na yajulikane. Hapa Mheshimiwa Kumchaya, alikuwa na wasiwasi kwamba yapo Makampuni ambayo yanaweza yakajificha yasisajiliwe. Baadae linakuja kuzuka jambo anasema mbona Kampuni hii hatuijui? Nataka niwahakikishie kwamba, tutafanya kazi ya kutosha kuhakikisha kwamba, Makampuni yote muhimu yanasajiliwa.

Mheshimiwa Halima Mdee anasema, Sheria inaendeleza urasimu. Tumesema kwamba, kuna tofauti ya ule mtiririko wa mlolongo wa zamani uliokuwepo. Sasa tunajenga kama vile *one stop centre,* halafu unasema Sheria hii inaongeza urasimu ule ule. Hii inakuwa si kweli. Bahati mbaya tu hayupo na angalau ame-*declare* kwamba, alikuwa anapata mshahara bila kufanya kazi wakati na Katibu Mkuu ame-*note* hiyo na atakaporudi kazini itabidi tufanye mahesabu ili utulipe hela zetu kwa maana ya Serikali.

Waajiri kupeleka taarifa kwa *DG* kutatengeneza mazingira ya rushwa katika kuamua kiasi cha fidia. Taarifa anayopeleka mwajiri itaunganishwa na taarifa aliyopeleka yeye mwenyewe aliyeumia. *Assessors* kazi yao ni kuthibitisha katika taarifa hizi mbili na ndiyo maana tumembana sana mwajiri kwamba, asipopeleka taarifa ndani ya siku 21 anapata adhabu tena kali. Mfanyakazi yeye tumempa nafasi kubwa zaidi, tumesema kwamba, asipopeleka taarifa ndani ya miezi 12 atakuwa amejikosesha haki mwenyewe. Kwa hiyo, utaona mazingira ya rushwa mnayoyahofia hapa hayatakuwepo kwa sababu si taarifa anazopeleka, ndiyo tutakazofanya sisi Mfuko huu uweze kujua ni kiasi gani cha kulipa. Taarifa zile zitakazosababisha ni kwamba, Mfuko utajua kwamba, mahali fulani pametokea ajali ya aina fulani. Watakaotathmini si taarifa hiyo, watakaotathmini ni *assessors* ambao watateuliwa kufuatana na utaalam walionao kulingana na ajali iliyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo michango mingine ambayo iliendelea kujitokeza leo asubuhi. Mheshimiwa Abubakar Khamis alisema, hizi *reasonable cost* hizi hapa, tena tunaotoa mwanya wa rushwa kwamba huyu Mkurugenzi Mkuu anapokadiria na kusema hizi ndizo *costs* ambazo zimekuwa *incurred*, anaangalia sura ya mtu aliyempelekea anasema hivi na hivi. Tumesema hivi, hata katika kulipa hiyo *compensation* yenyewe, hata katika kutathmi hizo *reasonable costs* ziwe za uhalisia wa gharama zenyewe, Mkurugenzi Mkuu akishamaliza kazi yake anapeleka kwenye Bodi ili Bodi ipitie na kupitisha. Kwa hiyo, ile Bodi ndiyo tunaowategemea wafanye kazi hii ya kumdhibiti huyu Mkurugenzi Mkuu katika mambo yake haya hasa yanayohusu fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 48 anasema *DG* amepewa uwezo wa kukadiria maumivu yasiyo ndani ya Sheria, maana *DG* si Daktari; kwa hiyo ni muhimu jukumu hili apewe Daktari. Nasema Mkurugenzi Mkuu kazi yake ni kuunda timu ya wataalam. Kama anaona suala hili linahitaji Daktari atampeleka Daktari. Kwa hiyo, katika timu hiyo atahakikisha Madaktari wamo. Kama linahitaji Mkemia Mkuu, atakuwepo Mkemia Mkuu au mwakilishi wake, kama linahitaji msomi wa aina fulani atakuwepo msomi wa aina fulani ili kuhakikisha haki inatendeka. Yeye kama yeye hawezi kuwa na taaluma zote hizo kwamba, sasa kumetokea ajali mahali fulani anachukua gari anasema kwa hapa wewe umeumia kiasi fulani; haiwezekani. Kwa hiyo, hili limezingatiwa na ndiyo maana tumesema tuachie wataalam wafanye kazi yao.

Kifungu cha 83 wanasema uwekezaji mwingine tutawapa matatizo kwa sababu watendaji maana fedha yote wanaweza wakatumia katika kuwekeza halafu wakakosa za kuwalipa wahanga. Kama mifuko ya hifadhi ya jamii ingekuwa inachukua michango inaiweka; halafu haiifanyii maarifa ya kuiongezea thamani, nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, malipo ambayo wafanyakazi wanachama wa mifuko hii wangekuwa wanalipwa, ingekuwa ni duni sana. Jitihada hizi za uwekezaji ndiyo zinafanya kuweza kuboresha hayo mafao ambayo wafanyakazi wanachama wanalipwa hivi sasa.

Ndiyo maana katika ile Kanuni baada ya kulipa *lump sum payment* ya muda ule lakini Waziri amepewa Mamlaka ya kuweza kuweka *minimum* tofauti na hiyo kuzingatia uwezo wa Mfuko, kuzingatia gharama za maisha na kuzingatia thamani ya fedha. Sasa

tusipoiruhusu hii kuwekeza, tutakuwa tumeufunga Mfuko huu kwamba iwe inapokea inalipa hizo zikiisha basi, ambapo wakizalisha hata uwezo wa kuhudumia walio wengi zaidi, huwezi ukatabiri kwamba kwa mwaka zitakuwa ajali kumi tu. Unaweza ukakadiria ajali kumi zikatokea ajali 1,000 sasa huna uwezo. Sasa kama Mfuko utakuwa haujiendelezi zaidi umebaki na yale makusanyo, itafika mahali Mfuko utakwama. Kwa kuwekeza Mfuko utakuwa endelevu zaidi.

Waziri kuweka *minimum* na *maximum* ni *very subjective*, itamkwe wazi wazi katika Sheria. Hili nimelieleza kwa sababu gani? Kwa sababu ni rahisi kubadili gharama za maisha zinabadilika kila siku. Kwa hiyo ni vyema ikabaki katika utaratibu huo wa Kanuni kwa Waziri kubadilisha. Tutakapokuwa tunatengeneza Kanuni zitatamka wazi wazi. Kwa hiyo, atasubiri mpaka mtu aende, mimi nimeumia aseme wewe utalipwa kwa *minimum* hii hapana. Hii *minimum* itatengenezwa kabla Mfuko haujaanza kazi, baada ya kutathmi mazingira halisi. Kwa hiyo, *minimum* ile au kima cha chini kabisa cha Mfuko huu, kitakuwa kimeshawekwa kuzingatia hali halisi ya maisha badala ya kutegemea shilingi 70,000 kutokana na kima cha chini cha mshahara cha shilingi laki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nina hakika, kwa kanuni ambazo tutazitengeneza, malipo yatakuwa ni bora zaidi kuliko shilingi 83,000 zinazolipwa sasa, bora zaidi kuliko shilingi 108,000 zinazolipwa hivi sasa, kwa kuzingatia mfumko wa bei ya maisha, kuzingatia ushukaji wa thamani ya fedha yetu, kwa kuzingatia mazingira halisi tuliyonayo sasa na upandaji wa maisha.

Mheshimiwa Pindi Chana, wale waliojiajiri wenyewe, je, Mfuko huu unaweza ukawazingatia? Kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Mfuko huu utamhusu kwa sababu kwa sasa hivi tunacholenga katika Mfuko huu ni wale wafanyakazi walioajiriwa. Kama na yeye ana kampuni yake, anafikiri ipo siku anaweza akahitaji msaada wa Mfuko huu, ilimradi tu ajisajiri, akalipa michango yao, atazingatiwa.

Je, Mfuko utazingatia ukubwa wa kiwanda kwa maana ya idadi ya wafanyakazi? Ni dhahiri, ndio maana tunasema kwamba, kutakuwa kuna tathmini inafanywa. Wewe kiwanda chako kina wafanyakazi 10,000, huwezi ukalipa sawa sawa na mtu mwenye mgahawa wa wafanyakazi watano. Hiyo lazima itakuwa tofauti.

Je, mbona Wabunge hatumo? Mheshimiwa Pindi Chana, suala la Wabunge tuliambiwa kwamba kuna utaratibu Wabunge tunaandaliwa ambao hivi sasa upo katika hatua mbalimbali za mchakato. Tukasema sawa, lakini katika sheria hii tumesema sheria hii inatambua mifuko mingine au taratibu nyingine za fidia ilimradi hii ambayo ni sheria mama wao watakaotengeneza taratibu nyingine za fidia wasilipe chini ya kiwango ambacho tutakuwa tumependekeza sisi katika kanuni siyo hizi tu za 70,000, hapana katika kanuni. Kama kanuni itasema kima cha chini cha kulipa ni shilingi 500,000, basi ahakikishe kwamba, Mbunge anayeumia au anayepata tatizo lolote lile ambalo linahitaji kulipwa fidia, isiwe chini ya 500,000, lakini hiyo itategemea kanuni itakavyotengenezwa. Kwa hiyo, tumehakikishiwa kwamba, Bunge nalo linajiandaa kutengeneza utaratibu wake kuhusu fidia kwa Waheshimiwa Wabunge.

Uharaka wa kushughulikia malipo ya fidia; kwa sababu sisi tunaamini *one stop centre* inafanya kazi haraka zaidi, wataalam wote watakuwepo na Bodi itakuwa inakutana mara kwa mara. Muda huu ni mrefu, naomba Mfuko huu uwe chini ya Wizara kama *Agency* na wafanyakazi wake wawe na uwezo. Ukiwa chini ya Wizara unaweza ukaingia katika ukiritimba wa Kiwizara, ndio maana tumeona bora ujitegemee, uwe *autonomous* pale itakuwa ni vizuri zaidi kwa wao kuweza kufanya kazi kama watu huru zaidi.

Je, mfanyakazi akiumizwa na *third party* tunafanyaje? Mfanyakazi akiumizwa na *third party*, kwa kweli hii sheria anayeumia imempa upendeleo wa hali ya juu sana. Tumezingatia ile kanuni ya *no fault principle*. Anapokuja kuripoti kwamba nimeumia, kitu ambacho Mfuko utajali ni kujua kiwango gani kaumia, hawataanza kutafuta ilikuwaje ukaumia, kwa nini hukukwepa, kwa nini hukuondoka, hapana! Kwa hiyo, hii sisi tumeizingatia katika ulipaji wa fidia.

Mfanyakazi akiumia kutokana na uzembe wake pia alipwe tu. Ndio nimesema, hatutauliza maswali mengi, isipokuwa yale ambayo tuliyaweka katika Sheria yale ya kusema mtu anakusudia kabisa kwamba mimi sasa nimechoka na maisha, ngoja nichukue gari hili nigonge ukuta hapa. Anachukua gari, anawasha moto anakwenda anagonga ukuta, bahati nzuri hakufa. Sasa unafanyaje, huyu kaamua mwenyewe. Kwa hiyo, katika masuala kama hayo, Mfuko hautahusika. Kama katika kufanya hivyo, kafanya kwa makusudi kabisa lakini ndio kavunjika miguu yote na mikono yote, kashakuwa mzigo kwa jamii kama jinsi ambavyo mtu aliyejifanya hivyo akiwa kijijini watu hawatasema shauri yake, watakasirika, baada ya siku mbili/tatu wataanza kumjali. Lazima wamtunze, kwa sababu sisi kama jamii bado tunawajibika kumtunza na ndio tumesema kwa yule atakayepata maumivu au vilema vya kudumu, Mfuko itabidi utengeneze utaratibu wa kumjali na vilevile utamtibu. Kwa yule atakayekufa, Mfuko vilevile utatengeneza utaratibu wa kumjali, ndio maana tumesema hayo. Kwa ule uzembe ambao ni wa kawaida, Mfuko hautahusika.

Adhabu ni nini? Akaorodhesha vifungu vingi, akasema mbona sioni adhabu? Adhabu zimetamkwa kama vile vifungu vya 71, 72, 73 mpaka 77, lakini zimeonekana ni kubwa, japo kuwa Wabunge wengine wamelalamika kwamba ni ndogo. Sasa nasema, madam tumesema *"not exceeding…,"* Waheshimiwa Wabunge tungeomba sana mruhusu Muswada huu upite.

Mfanyakazi akiumia, ni muda gani taarifa inapaswa kumfikia *DG?* Hiyo katika sheria imetamkwa wazi wazi. Mheshimiwa Cheyo, Muswada una matatizo kabisa, mimi nadhani nimefafanua vizuri, kwa hiyo utaunga mkono. Mfuko hausemi kila mwajiri atalipa kiasi gani. Kama wengine walivyosema na wewe mwenyewe ukaja kusema, wafanyakazi hawa wapo matabaka mbalimbali, wakati ulipokuwa ukizungumzia juu ya ukali wa faini. Kama waajiri wapo matabaka mbalimbali kwa kuzingatia faini, michango, ndio maana imekuwa vigumu katika sheria kusema asilimia 50 au asilimia 5 kama mchango. Huwezi ukafananisha na *Levy* wanayotoa VETA. Hii inakusanya wanachama wengi zaidi, ambao wengi wao ni waajiri wadogo wadogo. Sasa ukiwaweka kwa *percentage*, wengi wao utakuta umewaumiza sana. Sisi kazi yetu ni kuhakikisha ajira inaongezeka ili wafanyakazi wengi zaidi waweze kuajiriwa. Sasa katika mazingira hayo,

ndiyo maana tumeacha hivi kwamba, tuweze kupata nafasi ya kushauriana na mwajiri huyu kwa kiwango alichonacho kwa maana ya wafanyakazi alionao, tuweze kujua ni kiasi gani aweze kulipa. Hii ni katika kujitahidi kuwa na huruma katika kutekeleza Muswada huu utakapokuwa sheria.

*DG* mbona mamlaka makubwa sana? Yeye ni Polisi, anakwenda kukamata, anakagua na ndiye anaamua nani alipe. Nimefafanua kwamba, katika kulipa haamui yeye, wale wanaokwenda kukagua ambao ndio umewaita Polisi, wanakwenda kukagua na kupendekeza. Wakishapendekeza, *DG* anayachukua yale majina anayapeleka Bodi, Bodi ndiyo inayoamua kukataa, kukubaliana au kupunguza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Cheyo, kwa ufafanuzi huo mimi nina hakika utakuwa umeelewa vizuri zaidi.

Nani ambaye ni *wholly financially dependant?* Mtu ambaye anakuwa *regarded* kama *wholly financially dependant*, katika sheria mbalimbali ametamkwa mtoto ambaye hajatimiza miaka 18, sisi tunam-*regard* kama ni *wholly dependant*, mke wako au mume wako ni *wholly dependant*. Baba yako au mama yako wa umri fulani, hao ni *wholly dependants* au kama ulikuwa na *dependants* wengine, kwa mfano, katika mazingira haya kwa sababu UKIMWI unaua sana, unaweza ukawa na watoto wa ndugu zako ambao umebaki nao ambao hawajavuka miaka 18 na kisheria umeshawa-*adopt* kwamba wewe ndiye mlezi wao, hawa nao ni *wholly dependants*. Kwa hiyo, ukisoma na sheria nyingine, suala la *financially wholly dependant*, halitakupa matatizo sana.

Makadirio yote yatakuwa *approved*. Nimesema yatakuwa *approved* na Bodi. Ibara ya 71, 77, unazungumzia faini ya milioni 50. Unasema kuweka kumbukumbu tu, faini shilingi milioni 20. Yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mahesabu, anasema huko Serikalini kuna matatizo, hivi Serikali italipa hizi milioni zote? Nataka nikuhakikishie kwamba, Serikali ni taasisi mojawapo ambayo inajitahidi sana kutekeleza masuala ya utawala bora. Watakapoambiwa walipe kwa makosa watakayokuwa wamefanya, watalipa kwa sababu sasa hivi kila kitu kipo wazi. Wewe utatusaidia kuwasukuma Serikali walipe, kama watatuletea matatizo tutakuleta wewe Mwenyekiti utusaidie kuhakikisha kwamba wanalipa, lakini tunasema *not exceeding*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kulikuwa na michango kutoka kwa Mheshimiwa Siraju Kaboyonga; anasema, michango ya waajiri kwenye Mifuko katika kuamua kiwango ambacho waajiri watachangia kwenye Mfuko huu ni vyema ikakumbukwa kuwa waajiri hawa tayari wanachangia masuala mengine kama *NSSF, PPF* na *Skills Development Levy*. Ili waajiri wasilalamike juu ya ukubwa wa mzigo wa kuchangia maeneo mengi, nashauri tuwe waangalifu sana katika kuweka viwango vya michango ili visije kulalamikiwa na waajiri. Ni vyema mawazo ya waajiri kuhusu suala hili yakatafutwa na kuzingatiwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kaboyonga, katika maandalizi ya Muswada mzima, waajiri wameshiriki kwa ukamilifu kabisa. La pili, ndio maana tumeshindwa kuweka kiwango, tumesema tutashauriana na wadau katika kuweka viwango vya kuchangia ili kuhakikisha kwamba, hakuna anayeumia, maana unaweza ukaweka kiwango, halafu mtu badala ya kumshawishi awe mwaminifu, unamshawishi

kukwepa. Sasa sisi hatutaki kushawishi watu kukwepa, tunataka kushawishi watu wawe waaminifu ili Mfuko huu uwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho kabisa, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, alilalamika sana juu ya Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora kwamba, wanalalamika sana kwamba wao hawana chama cha wafanyakazi, mazingira yao ya kufanyia kazi ni mabovu. Nataka nikuhakikishie kwamba, hili lilijitokeza vilevile hata katika mchango wa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally wakati wa bajeti yangu. Kama nilivyoahidi wakati ule kwamba nitakuja kukitembelea kiwanda hicho ili kuhakikisha kwamba, tunazungumza na wafanyakazi wenyewe nasi tusikie. Nitakapokuja, nitakuja na wataalam mbalimbali wa Wizara yangu.

Nilikuwa nimetoa ahadi ya kuwatembela Waheshimiwa Wabunge wawili; mmoja akiwa ni Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Manyinyi. Tayari nimekwishakwenda huko, tumezungumza na viwanda vyake vyote na kwa kiasi kikubwa, matatizo yaliyokuwa kule tumeyatatua na nadhani Mheshimiwa Manyinyi ukimuuliza atakuwa shahidi. Sasa shughuli hapa kati kati zilikuwa zimetinga, pamoja na ugeni wa Mheshimiwa Rais. Nadhani baada ya kumaliza Bunge hili, tutakuwa huru zaidi kuweza kutimiza hiyo ahadi. Kama nilivyosema, nitakapokuja kukitembelea kiwanda hicho, nitahakikisha Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Tabora, kwa wale wenye nafasi nao wanashiriki, lakini hasa hasa Wabunge wa Mjini pale Tabora kama wewe Mheshimiwa Mawanne Mchemba, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na Kamati ya Bunge Zima, ninaomba nitumie Kanuni Namba 28(2), inayonipa mamlaka ya kuongeza muda. Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona, tumebakiwa na dakika chache tu ili kufikia saa saba kamili. Nadhani ni busara kwetu tukamaliza kabisa hatua zote za kupitisha Muswada huu ili tutakapokuja jioni saa 11.00, tuendelee na ajenda nyingine ambayo imewekwa kwenye *Order Paper*. Kwa hiyo, nitaongeza dakika 30, kwa hiyo shughuli zetu zitatupeleka mpaka saa 7.30 na ninaamini tunaweza tukawa tumezimaliza hata kabla ya saa 7.30. Kama tutamaliza kabla ya muda huo, basi nitasitisha shughuli zetu za Bunge. Sasa kwa kuwa hiyo itabidi iamuliwe kikanuni, nitaomba tu niwahoji kabla hatuaingia kwenye Kamati.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi wa Mwaka 2008 *(The Workers Compensation Act, 2008)***

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27

Ibara ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 31
Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kupendekeza kifungu cha 35 sehemu ya tatu kimeandikwa *"an employer shall…,"* ndani ya siku saba inatoa mipaka ya muda. Sasa baada ya kutafakari ninakubaliana, lakini ninaomba liongezwe neno "*seven working days,"* kwa sababu siku saba wakati mwingine kunakuwa na siku za sikukuu, wakati mwingine kuna Jumamosi, Jumapili, matokeo yake unaposema mtu apewe mipaka ya siku saba anatakiwa kufanya hilo jambo, unakuta wakati mwingine ni siku tatu, utakuta kuna *Nyerere Day,* kuna Idd. Sasa ombi langu, maeneo yote ambayo yameonesha siku saba, tuseme *seven working days* (siku saba za kazi).

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Pindi Chana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 36

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukumbusha tu, ibara ya 37, sehemu ya pili, nayo ina neno siku saba; tuongeze *seven working days* na kama wataalam watatukubalia, maeneo yote yenye siku saba, tuongeze neno *working days* ili nisisimame tena.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu zote tulizozipita na zilizopo mbele ambazo haziweki *working days*, tutaweka.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 38

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinamhitaji mwajiriwa kuji-*submit* kwa *Director General* mwenyewe ili aweze kupimwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Siyame, ni kifungu cha 38, kifungu kidogo cha ngapi?

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Cha kwanza! Katika hali hii *Director General* atakuwa Dodoma au Dar es Salaam na huyu mwajiriwa yuko Rukwa au Mtwara na pangine hali yake ni mbaya sana, atawezaje ku-*submit himself* kwa kipimo kwa *Director General* katika hali hiyo?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kinataka kuthibitisha kama anayoyasema ni sahihi. Kama akiwa Mtwara, Sumbawanga, Kaliua na aweze kufika; sijui mnajua Kaliua ilipo? Ipo Wilaya ya Urambo na kweli hawezi kufika huko, *Director General* mwenyewe mimi nina hakika atafanya mipango ya kumfikia kwa kutumia wataalam wake au yeye mwenyewe kwenda kucheki kwamba aliyoyazungumza ni kweli na hali yake ni mbaya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, lakini hapo pia kuna neno limeongezwa "*reasonable notice.*" Kwa hiyo, nadhani linazingatia sana umuhimu huo.

Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41

Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 46

**MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, juu ya wasiwasi ambao niliuonyesha na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliuonyesha juu ya kumwachia madaraka Mheshimiwa Waziri, kupitia kanuni atakazotunga kuweka ile *minimum* na *maximum*. Mimi nakubaliana naye kimsingi kwamba, kuweka kima maalum kama ilivyo hivi sasa katika marekebisho yaliyofanyika mwaka 1983 yana matatizo na tukiweka hapa, tuna matatizo. Lakini pia bado nina wasi wasi ule ule kwamba, Mheshimiwa Waziri, anaweza kwa kushauriwa na watu wengine, kifungu ambacho kimewekwa hapa ikawa siyo *reasonable* kama Waheshimiwa Wabunge, tungeshirikiana pamoja katika kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu la ufahamu ni kwamba; je, kwa kuwa sasa Bunge hili linao utaratibu wa kuwa na Kamati ya Sheria Ndogo, ambayo moja ya kazi zake ni kuzingatia kanuni mbalimbali zinazotungwa na Waheshimiwa Mawaziri; je, katika utaratibu huu ambao tunamwachia madaraka Mheshimiwa Waziri, Bunge lako Tukufu linaweza likakasimu madaraka hayo kwa Kamati yetu ya Sheria Ndogo ili kuona kwamba kifungu ambacho kitawekwa kitakuwa *reasonable?*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Namshukuru Mheshimiwa Missanga, kwa kuliuliza tena ili kupata ufafanuzi zaidi. Ni kweli na ndivyo tulivyozungumza hata kwenye Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba, madhari kanuni zote sasa lazima zipite katika hiyo Kamati ya Sheria Ndogo, kwa hiyo, Bunge vilevile litakuwa limewakilishwa. Kwanza, kutakuwa na wadau hawa katika utatu wetu, lakini vilevile na Kamati ya Sheria Ndogo ya Bunge lazima ijiridhishe kwamba, Kanuni hizi zimezingatia masuala muhimu au masuala ya msingi. Kwa hiyo, lazima zitakuja huku.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ni sahihi na labda tu niseme kwamba, kwa kweli hilo lilizingatiwa sana na nadhani Mheshimiwa Waziri utalitekeleza kwa utaratibu huo, ukizingatia tuna ile Kamati tumeiunda chini ya Mheshimiwa George Simbachawene. Mheshimiwa John Cheyo, kifungu hicho hicho cha 46?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kifungu cha 46(4) na (5), katika kifungu hiki kinamtaka mwajiri alipe mwezi wa kwanza wa madai na asipolipa, atapigwa faini isiyozidi shilingi milioni kumi. Pamoja na kwamba, najua tutakuja kulizungumza zaidi baadae, lakini kweli Waziri anaona hii kitu inawezekana? *Is it practicle* au tunatengeneza tu sheria ambayo ni vizuri kuisoma na kuweka ndani ya *Library?*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu kilichoko ndani ya sheria hii, kimewekwa ili kitumike kutatua tatizo. Hakuna kitu ambacho kimewekwa ndani ya sheria hii, kwa maana ya kwenda kukusanya vumbi kwenye maktaba, hapana! Kipindi tulichokadiria hapa na faini tuliyokadiria hapa ya *not exceeding ten million*, baada ya majadiliano marefu ndani ya Wizara na kwa kutumia wataalam katika Wizara nyingine, tumeona ni faini ambayo inawiana kabisa na kosa lenyewe. Kama tulivyosema *not exceeding ten million*, siyo *ten million per se*, hapana!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo nililonalo, ukiweka kiwango *not exceeding two million*, umeshaweka hata kiwango cha rushwa na kwamba, angalau awe anakadiria sana sana hata kuzidishia milioni kumi kama ilivyosemwa katika sheria. Ukiweka shilingi milioni kumi, mtu atasema okay, kwanza hawezi kuanza hata kwa laki ataanza kwa milioni, maana yake nimekupunguzia mara kumi.

Kwa hiyo, kinachonisumbua hapa ni kwamba, kwa kupanua wigo huu unakuwa mkubwa na wale waajiri ni wenye kipato kidogo; kwa mfano, hata kama wewe unaajiri mtumishi unapaswa kutoa ripoti. Akiungua mafuta ya sangara na mkono ukakatika kwa sababu ya yale mafuta yamekuwa ni mengi mno, inabidi wewe ulipe, usipolipa faini yako katika mwezi mmoja, isiyozidi shilingi milioni 10; ukiwa mahakamani, yule hakimu kama ana maadili mabovu na watu hawa siyo kwamba ni wachache ni rahisi sana kuambiwa kwamba bwana, mimi nimekupunguzia badala ya shilingi milioni 10, sasa ulipe faini ya milioni moja. Kama ungelikuwa umepunguza huo wigo, isingeenda mbali hivyo. Ndiyo matatizo yangu tu na itatokea hivyo hivyo kwa 71 baadaye, lakini siyo lazima nizungumze sasa. Wigo ni mkubwa mno Waziri, naomba upunguze.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapata tatizo kwamba, tunadhani Watanzania wote tumezama katika kula rushwa tu na tukifika hapo, tutakuwa sheria tunazozitunga hazitoi adhabu. Tunayo sheria hapa kwa mfano ya kujamiana ile, kifungo ni miaka 30, ni adhabu kali sana. Kwa hiyo, nayo ungesema tu kwamba, inatoa mwanya wa rushwa tena mkubwa kweli kweli. Mzee sema vizuri, usiposema vizuri, nakufunga miaka 30 hapa.

Zipo adhabu kali na nyingi tu hii siyo ya kwanza, ambazo zinategemea msingi wa utawala bora uenee mahali pote. Vinginevyo, tutakuwa tunashindwa kutoa adhabu, hata ukitoa adhabu ya shilingi milioni moja, mimi namwambia bwana kuna adhabu ya milioni moja hapa nipe elfu hamsini zangu. Hivi ni watu wangapi wamekamatwa na rushwa ya shilingi elfu thelathini; wengi tu. Watu wangapi wanakamatwa na rushwa ya shilingi elfu kumi; wengi tu. Kwa hiyo, ule wigo mimi nakubaliana nao ni mkubwa, lakini niseme tu kwamba, tungeacha ilivyo tuone inavyofanya kazi, tutakapohitaji ku-*ammend* baada ya kuona inavyofanya kazi, tutarejea kuleta *amendment.* Kwa sasa nadhani tungeanza na hizi kwa sababu tunataka ku-*set standards*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 47

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 48

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 49

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 50

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 51

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 52

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 62

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65
Kifungu cha 66
Kifungu cha 67
Kifungu cha 68
Kifungu cha 69
Kifungu cha 70

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 71

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 71(1), Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anajibu alionyesha kana kwamba watu wanajiunga kwenye Mfuko, lakini watu hawajiungi. Wanalazimishwa kujiunga kwenye Mfuko, ndivyo *section* hii inavyosema na hii ndiyo inanipa maswali kwamba ni lazima kweli Mfuko huu uchukue watu wote wa nchi hii, ambao wanatoa ajira hata kama ni ajira ya mtu mmoja. Sisi sote hapa tunaajiri madereva na watu wengine na ni lazima tumpelekee na hiyo barua kwa *Director General*, kumfahamisha kwamba, nime-*employ driver A* na nisipofanya hivyo, napata faini ya shilingi milioni 20, *not exceeding twenty million*; jamani *are we real being practical*?

Kwa hiyo, ningependa ajibu; ni lazima si hiari. Watu wanalazimashwa kufanya hivyo, hakuna *option* ambayo ungeweza ukailegeza kidogo hapa Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo msingi wa sheria yoyote; ni lazima hakuna hiari. Ukishasema hiyo ni sheria ni lazima waajiri wote wajisajili na Mfuko huu. Tukishaanza kusema huyu hapana, huyu ndiyo na huyu hivi itakuwa matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hata kama una mfanyakazi mmoja, kiwango chako kitakuwa kidogo sana Mheshimiwa Cheyo; unaogopa nini? Unaweza ukawa *charged* labda shilingi elfu moja tu, ila itakuwa imekuondolea matatizo makubwa sana, ninyi hamjui tu kwa sababu Watanzania walio wengi, hawajui haki zao za msingi. Wewe unamtuma kijana wako kuchunga ng’ombe, anagongwa na nyoka huko anafariki; ndugu zake wanaweza wakakudai fidia. Kwa hiyo, unakuwa umebeba mzigo mzito kuliko huu ambao unaukwepa.

Kwa hiyo, ni afadhali Mheshimiwa Cheyo, wale wachungaji waliopo kule Bariadi uwasajili hapa, uwe umejiondolea mzigo mzito kabisa. Akipambana na majambazi kule, watu wamekuja kuiba ng’ombe wako wamempiga mkuki, wewe unatembea tu kumbe

umechangia shilingi elfu tano tu. Hatujakadiria kiasi, lakini nafikiri kwa waajiri walio na wafanyakazi wachache, michango yao itakuwa ni kidogo sana kwa sababu ni lazima tuzingatie na hali halisi ya Mwananchi. Hatuwezi tukakufananisha wewe na *Williamson Diamonds.*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Waziri hajanielewa; wala tatizo siyo kiwango, tatizo ninaloliona ni vipi sheria hii itakavyotekelezeka? Sasa ametaja jambo lingine ambalo nilikuwa sijalifikiria zaidi kwamba, mchungaji kule kijijini asafiri kwenda kujisajili na asipojisajili anaweza akapigwa faini mpaka shilingi milioni 20, hata wanaotusikiliza wanaona kweli sisi tunafikiria!

Mimi sitaki kufikiria maneno ambayo si ya Kibunge, lakini nafikiri Mheshimiwa Waziri na wewe umenielewa; hii kweli inawezekana au tunatunga tu sheria kinadharia; *is it possible, is it practical!*? Tukishasema ndiyo na tutasema ndiyo, kwa sababu ndivyo ilivyo, uniambia wakati Rais atakapoweka mkono wake, waajiri wote watajisajili na wasipojisajili hawa wote ni *liable* au wanaweza wakalipa faini isiyozidi shilingi milioni 20. Ungeniambia kwamba, labda hii sheria tutaanza kufundisha watu kidogo kidogo wakaelewa na wafikie mahali hapo ningeelewa, lakini tunasema *shall,* tunangoja Mheshimiwa Rais aweke sahihi, kila mmoja wetu atakuwa na hatia inayoweza kutozwa faini ya shilingi milioni 20, ndicho ninachouliza. Tunatunga sheria ambayo inawezekana kutekelezeka? *This is the whole point.*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani pengine na Mheshimiwa Mbunge naye sheria hii hajaielewa sawa sawa; si yule mchungaji ni yule mwajiri. Mchungaji yeye anatembea tu, anayepaswa kusajili ni yule *employer* ambaye ndiyo wewe Mheshimiwa Cheyo. Wewe una upeo wa kutosha kujua kwamba, hii sheria ipo.

Pili, wakati tulipokuwa tukijibu hapa ilikuwa ni kipengele ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri amekijibu kwamba, tutaanza na kuelimisha kwanza, kwa sababu hata baada ya kutiwa saini Muswada huu, bado kuna hatua za kuchukua kuiunda taasisi yenyewe ambayo ni ndefu. *Workers education* ni lazima itumike, kuwafahamisha wananchi kuhusu sheria hii. Kwa hiyo, suala la elimu ni muhimu, lakini mtoa taarifa si mchungaji bali ni mwenye mchungaji.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli tuzingatie suala la waajiriwa, wamekuwa wakilia muda mrefu sana.

Kifungu cha 72
Kifungu cha 73

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 74

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki, nilikuwa nimeandika mawazo ambayo baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Waziri, nilikuwa nataka kupendekeza kwamba mstari wa nne …

**MWENYEKITI:** Mstari wa nne kifungu gani?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mstari wa nne, kifungu cha 74(1), pale mwisho anapotajwa *Director General*, baada ya maelezo ya Waziri kwamba, hatuwezi kuweka viwango, nilikuwa napendekeza kwamba, badala ya *Director General* ingelikuwa *Board* ili kuweka uzito juu ya ile *parcentage* itakayotumika. Kwamba, *Director General* atai-*subject to approval* ya Bodi yake na Bodi itakapo-*approve* basi ndiyo itakapotumika badala ya *Director General* peke yake. Yeye ana Bodi na hili ni jambo zito, kwa nini asilipeleke kwenye Bodi kupata *approval* ya Bodi na halafu ndiyo itumike.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umeipata vizuri pale?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimempata vizuri, ukiangalia majukumu ya Bodi, yote haya yamo. Sasa hapa *Director General* anapotajwa ni ile *final;* sasa yeye kuja kui-*release* hiyo kwamba imefanyika, atakuwa amepitisha kwenye mchakato wa Bodi, kwa sababu maamuzi mengi ambayo yanamtaja *Director General* hapa yeye ni *final*, anakuja kutoa maamuzi ambayo yametolewa na Bodi. Kwa hiyo, litafuata mkondo huo.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyoyasema Naibu Waziri siyo hali halisi iliyojitokeza katika *section* hii kama ilivyo. Naibu Waziri anataka kutuambia kwamba, kila ambalo *Director General* atalifanya, litakuwa limepata *approval* ya Bodi, lakini liko wapi; angalau basi lingekuwa kwenye *preamble*. Kwa sababu *preamble* haisemi hivyo, hapa ukiweka Bodi ndiyo unamwajibisha *Director General* kwenye *approval* ya Bodi, lakini anayoyasema Naibu Waziri ni utaratibu anaoufikiria kuwa ndivyo utakavyokuwa, lakini sivyo ilivyo kwenye sheria.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokisema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba, tunakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, badala ya *Director General* pale tutaweka Bodi, kwa sababu maamuzi yenyewe ni mazito. Pili, hata ukisoma hapa *Subject to provisions of this section, an employer shall be assessed or provisionally assessed by the Director General according to* a *tariff of assessment calculated on the basis of the percentage of the annual earnings of the employer's employees as the Director General may with due regard to the requirements of the Fund for the year of assessment deem necessary.*

Sasa yeye hawezi kufanya *provisional assessment* na yeye huyu akaja aka-*approve* tena. Kwa hiyo, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, hilo tutalizingatia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 75
Kifungu cha 76
Kifungu cha 77
Kifungu cha 78
Kifungu cha 79

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 80

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 81

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 82

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 82 kama kilivyo; katika mchango wangu wa maandishi nilipendekeza tumwondoe Waziri katika ku-*approve Fund.* Menejimenti itakuwa inatunza fedha zake ili kuondoa urasimu, kwa sababu una Bodi na Menejimenti. Sasa unataka kule watakapokuwa wanaweka pesa, waje kwa Waziri kusema a-*approve* na urasimu ule wa Wizara; Katibu Mkuu hayupo, Waziri kasafiri; sasa hizi pesa zinakuwa zinakaa kwenye makasha mpaka Waziri arudi na wakati tuna Menejimenti nzuri na Bodi nzuri; kwa nini tusiachie mambo haya kwenye Menejimenti pamoja na Bodi?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anacho-*approve* Waziri pale siyo kwamba, sasa peleka hela Benki, amesha-*approve* kwamba benki hii ni nzuri, kwa sababu kumeshatokea sasa hivi mazingira tatainishi katika masuala yetu ya fedha. Inapotokea vurugu, anayekuja kuwajibishwa ni Waziri. Kwa hiyo, ni vyema na Waziri naye akawa anajua hiyo benki anayokwenda kuweka inastahili kuweka hela nyingi za umma. Kwa hiyo, ni vyema tukashirikiana wote katika kuamua benki, lakini siyo kwamba watakuwa wakisema sasa Waziri yupo, hayupo wanaweka mamilioni mfukuoni, kule wakiibiwa wasije wakamtaja Waziri wameibiwa

wenyewe kwa uzembe wao. Sisi tunahusika tu katika ku-*approve* benki stahili, ambayo tunadhani hii ndiyo *credible* benki pelekeni.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 83
Kifungu cha 84
Kifungu cha 85
Kifungu cha 86
Kifungu cha 87
Kifungu cha 88
Kifungu cha 89
Kifungu cha 90
Kifungu cha 91
Kifungu cha 92
Kifungu cha 93
Kifungu cha 94
Kifungu cha 95
Kifungu cha 96
Kifungu cha 97

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 98

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anajibu moja ya hoja hapa, ameeleza kwamba, baada ya Mheshimiwa Rais kuidhinisha Muswada huu na kuwa sheria kamili, itachukua muda katika kutengeneza kanuni na mambo yote yale ambayo yanasaidia kukamilisha na kuanza rasmi kwa shughuli hii. Sasa hapa kwenye kifungu cha 98 tunazungumzia kwamba, Rais akisaini maana yake ile sheria ya zamani imekuwa *repelled* ikishakuwa hivyo. Endapo litatokea tatizo pale, baada ya Rais kusaini Muswada huu na kabla mambo mengine kukamilika na kwa sababu sheria hii ya zamani tulishaifutilia mbali, hapa *status* inakuwaje; mfanyakazi anapata haki yake vipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, *concern* ya Mheshimiwa Missanga, *transition period* hiyo inakuwaje, hiyo unayoisema ya kutoa elimu, hebu tusaidie itakuwaje na watu wanaweza wakaendelea kupata ajali?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tutakapotunga Kanuni, ndiyo itatangaza tarehe ya Muswada huu kuanza na wakati tutakapotunga kanuni ndipo ambapo tunafuta zile sheria za zamani, kabla ya hapo sheria za zamani zitakuwa zinaendelea kufanya kazi. Kwa hiyo, atahudumiwa kwa utaratibu wa sheria za zamani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la kwanza

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jedwali la kwanza, nimeona *composition* ile pale, lakini kwa maoni yangu naona kuna mtu muhimu mmoja kaachwa. Katika *composition* ya Bodi, Daktari kwa sababu unazungumzia mambo ya kuumia na mimi sina hakika kama huyu mmoja anayetoka kwenye *occupational safety and healthy authority*, anaweza akawa *competent.* Dokta wa kuweza kutoa ushauri unaostahili katika masuala ya matibabu. Nilitaka nishauri kwamba, katika Bodi hii tuongeze kipengele cha kumuweka Dokta kwa maana ambayo inaeleweka.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sifa ambazo zimeainishwa hapa zimezingatia maeneo mapana zaidi; Madaktari tulikuwa tumewaacha kwenye zile *assessors' boards*, ambazo ndiyo hasa zinakuja ku-*feed* ili hawa sasa waweze kuamua *independently* kuliko kumuweka daktari hapa halafu akaja mwenzie; lazima kwa vyovyote vile watajidai kuiunga mkono lakini kuwaacha hawa *separate* na wale *assessors* wakawa *separate*, inakuwa ni vizuri zaidi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana hofu ya Mheshimiwa Waziri sijui kama ni sawasawa au vipi, lakini nadhani panaweza pakafika mahali ambapo Bodi ile imekwama inataka *experts* ya kidaktari kuamua juu ya jambo lile. Sasa sidhani kama atapendelea *assessors* wale kwa sababu ni daktari. Mimi nadhani hapa mantiki iangaliwe, kwa sababu inaweza ikafika wakati hapa tunataka mtaalamu, tunajua katika Bodi nyingi wapo wanasheria. Mnafika mahali mnasema, bwana hebu Mwanasheria fulani tuambie.

Tutoe mfano hapa Mheshimiwa Chenge, samahani kwa kukutaja jina. Wewe mwanasheria hebu tusaidie, kwa hiyo kunaweza kukatokea *instances* ambazo tunahitaji ushauri wa kiutaalamu na kidaktari. Kuna dhambi gani kama mtu mmoja tutamuweka kwa faida ya kuja kufanikisha shughuli ambayo inakusudiwa kufanyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kuna tatizo katika hilo kweli?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakachofanya badala ya kuongeza idadi ya Wajumbe kwenye ile *amendment* ambayo inasema; *one member from higher learning institutions*, tutahakikisha kwamba, tutakuwa *specific* kuwa mmoja kutoka katika moja ya vyuo vyetu vya Madaktari.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la Pili
Jedwali la Tatu

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la Nne

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jedwali la nne sina tatizo na 1, 2, 3 na 4, lakini ukianza pale 5; *cross reference ya section* 36(1)(a)(ii) mpaka (iii), ukija huku kwenye Muswada 36 hakuna. Sasa hiyo *reference* inakwenda wapi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye *schedule of amendment* kuanzia namba tano siyo 36 tena ni 52(1)(a)(i). Kwa hiyo, ni kuanzia 52 na siyo 36 kumefanyiwa marekebisho.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kwenye *schedule of amendment* naona mkiangalia vizuri mtaipata pale.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi wa Mwaka 2008** ***(The Workers Compensation Act, 2008)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Bunge Zima, imekaa na kupitia muswada wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, kifungu kwa kifungu na kuupitisha pamoja na marekebisho yake. Hivyo, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali na kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hatua iliyobakia ya Muswada huu sasa ni kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuweka sahihi yake na hivyo kuruhusu uanze kutumika kama sheria. Basi niseme ninawashukuru sana kwa ajili ya kumaliza hatua ya kupitisha Muswada huo na kabla sijamaliza shughuli za leo nilalo tangazo dogo.

Waheshimiwa Wabunge, mchana ilikuwa tupitie Azimio la Bunge la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara. Kwa utaratibu uliopo hapa Mezani, nimepokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Spika kwamba, shughuli hiyo sasa hatutaifanya tena jioni. Azimio hilo linahitaji kuendelea kufanyiwa mashauriano zaidi. Kwa hali hiyo, Waheshimiwa Wabunge sitasitisha shughuli za Bunge, nitaziahirisha mpaka kesho saa tatu asubuhi ili kutoa muda wa mashauriano zaidi kuhusiana na Azimio hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba niwatangazie kwamba, shughuli za leo tutakuwa tumeishia hapa, kwa mujibu wa ratiba ilivyojieleza na maagizo ya Mheshimiwa Spika. Sasa ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi, ndani ya Ukumbi huu.

*(Saa 07.36 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 05 Novemba, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*